

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Thelathini na Moja - Tarehe 15 Julai, 2010

(Mkutano Ulianiza Saa Tatoo Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 1 ya mwaka 2009/2010 (*Statement of Re-allocation Warrant No. 1 of the year 2009/2010*).

MASWALI NA MAJIBU

Na. 321

Hitaji la Zahanati Katika Vijiji vya Mpwapwa

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Kwa kuwa, vijiji vya Lupeta, Bumila na Kimagai vilivyopo kata ya Kimagai, Wilayani havina Zahanati na hivyo kufanya wananchi wa vijiji hivyo kufuata huduma ya afya hadi hospitali ya wilaya ya Mpwapwa, iliyopo umbali wa km. Kumi(10) hadi kumi na tano (15).

Je, Serikali imetenga fedha kiasi gani za ujenzi wa zahanati kwa ajili ya vijiji hivyo katika Bajeti ya mwaka 2009/2010?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti ya mwana 2009/2010, Serikali kupitia mpango wa Maendeleo ya Afya ya msingi (MMAM) imetenga jumla ya shilingi milioni 257,800,859/= kwa ajili ya ukarabati, ujenzi wa nyumba za watumishi na ukamilishaji wa ujenzi wa zahanati kwa mchanganuo ufuatao:-

- (i) Ujenzi wa nyumba za watumishi katika zahanati za vijiji vya Nzugilo, Idodoma, Mtera na Ipera - shilingi milioni 150.
- (ii) Ukarabati wa zahanati za vijiji vya Mlunduzi, Mpwapwa Mjini na Winza - Shilingi milioni 45.
- (iii) Kukamilisha ujenzi wa zahanati zilizoanzishwa kwa nguvu za wananchi katika vijiji vya Igoji, Kiegea, Iyenge na Chaludewa - Shilingi 62,800,859.

Pia kupitia mpango wa kuzipatia Halmashauri ruzuku isiyo na masharti (*local Government Development Grant (LGDG)*) zilitengwa shilingi milioni 100,000,000 kwa ajili ya kazi zifuatazo:-

- (i) Ujenzi wa zahanati ya Mgoma shilingi milioni 15.
 - (ii) Ujenzi wa zahanati ya Kizi shilingi milioni 15.
 - (iii) Ujenzi wa kituo cha Afya Mima shilingi milioni 30.
-
- (iv) Ujenzi wa kituo cha afya Mbori shilingi milioni 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Lupeta, Bumila na Kimagai havikutengewa fedha kwa sababu havina miradi ya ujenzi wa zahanati iliyokwishaanzishwa kwa nguvu za wananchi. Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa inaendelea kuhamasisha jamii katika vijiji visivyo na zahanati ili vianzishe ujenzi na baadaye Serikali na wadau wengine wa maendeleo waweze kuchangia katika miradi hiyo. (*Makofi*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza; nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini, nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa zahanati ili ikamilike lazima iwe na watumishi wa kutosha na dawa za kutosha; na kwa kuwa tatizo la upungufu wa watalaam, waganga katika zahanati ni tatizo la muda mrefu, ni karibu la nnchi nzima zikiwemo zahanati za Wilaya ya Mpwapwa; na kwa kuwa hivi sasa wameanzisha Kada Mpya ya *Clinical Assistant*.

Tuna *Clinical Officers* na tuna *Clinical Assistants*. Sasa kwa mpango huu wa kutoa Matabibu Wasaidizi. Je, sasa Matabibu hao wameanza kupewa mafunzo kwa vyuo ambavyo Mheshimiwa Waziri alitutajia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba, zahanati lazima iwe na dawa za kutosha, lakini kwa sababu Bajeti inayotengwa kwa ajili ya kununua dawa ni fedha kidogo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja sasa ya kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kununua dawa katika zahanati zetu?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nimpongeze Naibu Waziri- TAMISEMI kwa majibu mazuri aliyotoa. Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la kwanza la Mheshimiwa Lubeleje; ni kweli tulipitia mitaala ya vijana tunaowafundisha na tukaanzisha *grade* za *assistants* (*Clinical Assistant na Nursing Assistant*) ambazo zilikuwa zimefutwa. Wakati natoa hotuba yangu ya Bajeti wiki iliyopita, nilitamka kwamba sasa hivi tumeishaanza kupata wahitimu na nilitoa hata takwimu kwamba wako 1793 na wengine wanahitimu mwezi huu Julai, 2010 ambao wako tayari kusambazwa katika vituo vyetu. Kwa hiyo, kazi ni kwa Halmashauri kuainisha mahitaji yao na kuomba na sisi tutakuwa tayari kuapeleka. Waweke mazingira ya kuweza kuwapokea kwa maana ya nyumba na mambo ya msingi kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu dawa; Hatuna matatizo ya kutoa dawa, na kila mwaka wakati wa Bajeti yetu huwa tunatoa vituo ambavyo tumeridhika navyo kwamba vianze kutoa huduma na kuvitamka, na mwaka huu nilitamka vituo 99 ambavyo vimeruhusiwa kuanza kufanya kazi kwa sababu tumetenga fungu la dawa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Lubeleje alisimamie hili suala kwa maana ya kwamba wajenge zahanati, watuambie zimekamilika, halafu sisi tutaangalia kiasi gani cha dawa tunaweza tukapeleka huko.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, niwahakikishie, kwa kuwa tunakaribia mwisho mwisho ni vizuri nikawapa nafasi Waheshimiwa Wabunge wengi zaidi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa yeote atakayesimama kwa swali la nyongeza, nitampa nafasi na kwa Mheshimiwa yeote atakayetaka kuchangia *PPP* kama *Order Paper* inavyosema, nitampa nafasi, mshindwe wenye.

Na. 232

Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa

MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.n.y. MHE. JANET B. KAHAMA) aliuliza:-

Septemba mwaka 2009, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipiga kura juu ya kuundwa Shirika Jipyä lenye nguvu zaidi kwa ajili ya wanawake na ambalo liliunganisha Ofisi tatu za Umoja wa Mataifa zinazoshughulikia masuala ya wanawake kuwa chombo kimoja chini ya Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Kwa kuwa hatua hiyo ya Umoja wa Mataifa ni njia muafaka ya kuleta usawa na haki kwa wanawake duniani:-

Je, ni hatua gani zimefikiwa katika utekelezaji wa Azimio hilo la Umoja wa Mataifa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbunge, ningependa kufanya masahihisho kama ifuatavyo:- Kwanza, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa halikupiga kura bali lilipitisha kwa kauli moja Azimio la kuunda chombo kipyä ambacho kitaunganisha taasisi nne za Umoja wa Mataifa na siyo ofisi tatu za Umoja huo.

Pili, chombo hicho hakitakuwa chini ya usimamizi wa Naibu Katibu Mkuu, bali kitakuwa chini ya Katibu Mkuu Msaidizi (*Under Secretary General*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya masahihisho hayo, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet B. Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikao cha 63 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kilipitisha kwa kauli moja Azimio Na. A/63/311 lenye kichwa cha maneno *System Wide Coherence* ambalo lilitokana na majadiliano yaliyofikiwa na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa katika kuzitaka Taasisi za Umoja huo kufanya kazi kwa mwelekeo wa pamoa wenyewe kuleta tija na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili liliangalia vipengele vikuu vitano vilivyo hitaji mageuzi. Lakini hasa kipengele kinachozungumzia uwezo wa Umoja wa

Mataifa kufanikisha azma ya kuleta usawa wa jinsia na maendeleo ya wanawake. Katika kipengele hicho, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa liliazimia yafuatayo:-

1. Kuunga mkono kwa dhati uunganishwaji wa Taasisi zifuatazo za Umoja wa Mataifa:-

Ofisi ya Mshauri Maalum wa Masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake, Divisheni ya Maendeleo ya Wanawake, Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Wanawake na Chuo cha Kimataifa cha Tafiti na Mafunzo kwa Maendeleo ya Wanawake kuwa chombo kimoja kwa kuunganisha majukumu ya sasa ya Taasisi hizo.

2. Kuunga mkono chombo kitakachoundwa kutohana na uunganishwaji wa taasisi hizo kuwa chini ya usimamizi wa Katibu Mkuu Msaidizi ambaye atawajibika moja kwa moja kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.
3. Kumwomba Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuwasilisha kwa majadiliano zaidi katika kikao cha 64 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Rasimu yakinifu itakayotoa mapendekezo ya njozi na malengo ya chombo kipyga, muundo wake, namna kitakavyopata fedha za kujiendesha na pia mapendekezo kuhusiana na aina ya Baraza la Uongozi wa chombo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliwasilisha rasimu kuhusu kuundwa kwa chombo hicho kwa majadiliano na nchi wanachama katika kikao cha 64 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kama alivyoombwa.

Majadiliano hayo yamefanyika na yamemalizika siku ya Ijumaa tarehe 2 Julai, 2010 ambapo Baraza hilo limepitisha kwa kauli moja Azimio Na. A/64.1.56 ambalo pamoa na mambo mengine limehitimisha suala la kuundwa kwa chombo kipyga cha kushughulikia masuala ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa chombo hicho kipyga kinaitwa *UN WOMEN*. Uteuzi wa Msimamizi wa chombo hiki ambaye atakuwa na cheo cha *Under Secretary General* kama nilivyooleza hapo awali, haujafanyika bado.

Hivyo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa amemwomba Naibu wake Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, asimamie chombo hiki kipyga hadi uteuzi utakapofanyika.

Napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Janet Kahama kwa kufuatilia kwa karibu sana masuala yanayohusu haki na usawa wa wanawake duniani.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Ninashukuru sana kupata majibu mazuri ambayo kwa kweli yamenifanya nikose hata maswali ya

nyongeza. Lakini, bado ningetaka kujua. Kwa kuwa Serikali ya Tanzania ilijitahidi sana kuendeleza wanawake mpaka tukaweza kupata bahati sisi tukashika Kituo cha Uenyekiti wakati wa *Beijing Platform* ambao Mheshimiwa Mongella alikuwa ndiye Mwenyekiti; na kwa sababu tumebahatika pia kupata nafasi ya Asha-Rose Migiro kuwa Naibu Katibu Mkuu wa jumuiya hiyo; sasa ningeomba Serikali, kwa sababu kazi kubwa imefanyiika katika kuleta haki za wanawake. Je, Serikali haioni sasa tujitahidi kusaidiana na Dr. Asha-Rose Migiro kuhakikisha tunafanya *lobbying* ya kutosha ili kuhakikisha atakayekuwa kiongozi na mwenyekiti wa nafasi hiyo atoke Tanzania? Ahsante!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tungependa iwe hivyo kwamba kiongozi au mwenyekiti wa chombo hiki awe kutoka Tanzania. Lakini, mambo ya Umoja wa Mataifa yana taratibu zake. Tunaweza tukajitahidi, na ingekuwa kitu cha maana kwetu na cha heshima kuwa na Mtanzania ambaye angeongoza chombo hiki. (*Makodi*)

Lakini, kufuatia taratibu hizi, inategemea sasa matakwa ya Katibu Mkuu kupitisha jambo hili kwenyevyombo fulani vya Umoja wa Mataifa ambavyo ndivyo vinafanya uamuzi. Lakini, hata hivyo, pendekezo la Mheshimiwa Kahama tunalichukua na tutaangalia namna gani tunaweza kufanikisha matakwa hayo.

MHE. CYNTHIA H. NGOYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Na mimi nina swal moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa Maazimio yaliyotolewa na Umoja wa Mataifa kuhusu uundwaji wa chombo hiki ni mazuri na yana malengo mazuri sana kwa wanawake Watanzania.

Je, chombo hiki kitakapoundwa, kiko tayari au waandalizi wa chombo hiki wako tayari kuwashirikisha wanawake Watanzania ili kuibua mambo ya msingi ambayo yanawakwaza wanawake kama vikwazo katika maendeleo yao? Je, hilo, uko tayari kulifanya?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, hiki ni chombo cha kuwaendeleza wanawake.

Kwa hiyo, hapo kitakapokamilika, kwa sababu chombo hiki sasa kimeishaundwa, lakini bado *structure* yake namna gani fedha kitapata kuijendesha bado hilo halijakamilika. (*Makofi*)

Lakini chombo hiki kikikamilika kabisa ni chombo ambacho kitatetea haki za wanawake. Kwa hiyo, mpaka hapo ikifika wakati huo, bila shaka wanawake wa Tanzania watakuwa na kila haki ya kupeleka matatizo katika chombo hiki kutafuta ufumbuzi.

MHE. MGENI J. KADIKA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inayo Kauli mbiu ya Kilimo Kwanza:-

Je, Kauli hii inatofuati gani na Siasa ni Kilimo, Kilimo cha Kufa na Kupona na Kilimo ni Utu wa mgongo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kueleza tofauti kati ya "Siasa ni Kilimo", Kilimo cha Kufa na Kupona' "Kilimo Kwanza", ningependa kutoa maelezo ya utangulilzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi inayotegemea kilimo kwa ajira ya wananchi wake walio wengi.

Huo ndio ukweli ambao umekuwepo na utaendelea kuwepo kwa muda mrefu hadi hapo tutakapokuwa na viwanda vya kupunguza ajira katika kilimo na kuhamishiwa nguvu kazi yetu katika viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli huu ulifahamika tangu uhuru wa Tanganyika mwaka 1961.

Mwaka 1972 Chama cha *TANU* kwa kutambua umuhimu wa kilimo katika uchumi wetu kilitoa Tamko la Siasa Kilimo, ikiwa na maana kuwa *TANU* kama chama cha siasa na wanasiwa wake, waliona hakuna jambo muhimu katika sera zake kuliko kilimo. Ndio maana wakaazimia kuwa siasa ni kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kujibu swal la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, siasa ni Kilimo, ni tamko lililotolewa na Chama cha *TANU* mwaka 1972, lilikusudia kukitumia Chama na Serikali yake kutilia mkazo matumizi ya Kanuni za Kilimo bora kwa nia ya kuinua uzalishaji katika Kilimo hususani kwa wakulima wadogo kwa nia ya kukuza uchumi na kuondokana na umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli mbiu ya Kilimo ni Utu wa Mgongo ya mwaka 1982 ililenga kulikumbusha Taifa kuwa huwezi kuzungumza Uchumi bila kuhusisha Kilimo ambacho kwa wakati huo kilikuwa kinachangia 40% ya pato la Taifa.

Kwa maneno mengine ni kauli ambayo hata leo bado ina maana kwa vile ajira kubwa ya watu wetu iko katika kilimo, ufugaji na uvuvi. Aidha Kilimo cha Kufa na Kupona haikuwa kauli Mbiu bali ilikuwa ni wito wa Rais wakati huo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa kuwaasa watu wote popote walipo walime ili kupambana na upungufu wa chakula uliotokea mwaka 1973/1974.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimo Kwanza upande wake ni tamko lililoeleza azma ya Serikali ya Awamu ya nne ya kuongeza uwekezaji katika Kilimo kwa njia ya Bajeti ya Serikali, Mikopo ya Mabenki na uwekezaji wa wakulima binafsi wadogo, wa kati na wakubwa.

Kauli mbiu ya Kilimo kwanza inatambua nafasi ya Wizara zote, Mashirika, Mabenki na Makampuni binafsi kuchangia utekelezaji katika Kilimo Kwanza katika mipango yao ya Maendeleo kama vile Miundombinu, viwanda, Nishati, Mabenki, Vyama vya Ushirika na sekta kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo hayo tofauti baina ya Kauli Mbiu hizi pamoja na kuwa zote zina lengo moja la kutambua umuhimu wa Kilimo tofauti iko katika msisitizo na wakati gani tamko limetolewa katika mazingira gani ya Kiuchumi na Kisiasa. Kauli Mbiu ya Kilimo kwanza inasisitiza ushiriki wa sekta binafsi katika mazingira ya Uchumi wa soko msisitizo ambao haukuwepo katika Siasa ni Kilimo.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swal la nyongeza.

MWENYEKITI: Husikiki Mheshimiwa.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza kwa kuwa Kilimo Kwanza ndiyo ndiyo Kauli Mbiu ya Serikali ya Awamu ya nne.

Kwa kuwa Mikoa mingi huzalisha matunda nchini Tanzania ikiwemo Mkao wa Tanga, Morogoro, Bagamoyo ambayo inazalisha mananasi kwa wingi na machungwa je Serikali ina mikakati gani kwa hawa wakulima angalau kuwawezesha kupata mashine za kusindika matunda yao ili kutengeneza *juice* na kuweza kupata soko la kuuza nje na ndani ya nchi yetu ili kujikwamua na umasikini?

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Kadika kwamba nchi yetu inazalisha matunda hususani maeneo ambayo ameyataja.

Lakini vilevile napenda kumjulisha kuwa katika maeneo yote hayo Serikali kupitia mpango wa kuendeleza Kilimo kule Wilayani *DADPS* yaani mipango ya kuendeleza Kilimo Wilayani, wananchi wanaweza kubuni miradi katika vikundi mbalimbali ambavyo wanaweza kununua mashine ndogo kwa ajili ya kusindika lakini

vilevile Halmashauri zinaweza zikawasiliana na *SIDO* na kubuni mashine ndogo ambazo zinaweza kuwasaidia katika kuongeza *value* ya matunda yao.

Serikali tunachokifanya ni sisi hatujengi viwanda wala hatununui lakini tunaandaa mazingira mazuri kwa ajili ya uwekezaji na kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kwa mfano pale Morogoro kuna kiwanda cha *UNAT* ambacho kinachukua mananasi na machungwa kwa ajili ya kutengeneza *juice*.

MHE. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba tafsiri iliyotumika ya kuandaa mpango wa Kilimo Kwanza sasa imezingatia Siasa ni Kilimo ya Iringa. Na kwa msingi huo sasa hatutayumba tutaendelea kutumia Kauli Mbiu hii ili Watanzania wote na kila mtu aelewé kuwa hivi ndivyo tunavyo elekea kuliko kubadilika badilika?

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mzindakaya kwamba tutaendeleza Kauli Mbiu ya Kilimo Kwanza. Lakini niseme kwamba Kilimo kwanza kina mahusiano makubwa kabisa na Kauli Mbiu zote zilizopita hatusemi kwamba Kauli Mbiu ya Kilimo Kwanza basi inafuta Siasa ni Kilimo wala hatusemi Kauli Mbiu ya Kilimo Kwanza inafuta Kauli Mbiu ya Kilimo ni Utu wa Mgongo kwasababu Siasa ni Kilimo Chama kilichokuwa kina watawala wakati ule na uongozi wa Serikali kazi yao ilikuwa ni kuhamasisha kilimo kwa mfano Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa anapokwenda kufungua shule yoyote ile au mkutano wowote lazima asisiize kilimo kwamba kiongozi yoyote yule asisitize kilimo, kwa maana ya kuwaeleza wananchi jinsi ya kutumia kanuni za kilimo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii ya kilimo ni uti wa Mgongo vilevile ilikuwa inawakumbusha wananchi kwamba hatuwezi tukaendelea kwasababu kilimo kinachangia 40% ya pato la Taifa. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kwamba tunajali kilimo ili tuweze kukuza uchumi wetu. Kilimo Kwanza kina hamasisha wafanyabiashra binafsi na vyombo vya Fedha viweze kuchangia lakini pia kuongeza Bajeti ya Serikali ili tuweze kuongeza tija na uzalishaji zaidi. Kwa hiyo, vyote hivi ambavyo tumevisema Kauli Mbiu hizi zinakwenda pamoja zote zilizopo siyo kwamba Kilimo Kwanza kinachukua zile zingine hapana kabisa, vyote tunaviendeleza ila inategemeana na wakati na mazingira ya Kisiasa ambapo Kauli Mbiu hizi zinatolewa.

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Kauli Mbiu ya Kilimo Kwanza limepata mwitikio mkubwa sana wa wananchi wa zao la Tumbaku hasa katika Wilaya ya Kahama hivyo kuzalisha zao hilo kwa wingi zaidi na kwa kuwa mwaka huu wakulima wa zao hili Wilayani humo walikopa pembejeo kwa dola wakauza kwa dola lakini wakalipwa kwa shilingi na siyo kwa thamani ya dola. Hali ambayo imesababisha mtafauruku mkubwa hivi sasa katika Wilaya hii. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu utaratibu huu?

NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba unapokopa pembejeo kwa dola na unapouza tumbaku yako kwa dola basi unatakiwa ulipwe kwa dola. Lakini kama hawafanyi hivyo nawaagiza Halmashauri na Bodi ya Tumbaku waweze kukaa na kuhakikisha kuwa suala hili linakwisha kwasababu wananchi wakati mwininge wanaibiwa kwenye *exchange rate* kwamba wanakopa kwa dola halafu wanalipwa kwa shilingi kwa kweli hiyo siyo haki kabisa na kauli ya Serikali ni kuhakikisha kwamba wakulima wale wanapata haki zao kutokana na jinsi walivyowekeza.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ingawa sikusimama lakini nashukuru umenipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwuliza Naibu Waziri kwa kuwa kilimo ni pamoja na uhifadhi, usafirishaji na masoko na haya yote bado ni matatizo kwa wakulima wetu wa Tanzania. Je, Serikali imejipangaje kuondoa matatizo haya kwa wakulima?

MWENYEKITI: Nilidhani swalilako litamchokoza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika mwenyewe ili pamoja na mambo mengine atoe salam za Bunda, Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyomruhusu Mheshimiwa Mbunge kuuliza bila kusimama na mimi naomba kujibu bila kuomba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Kilimo Kwanza limesisitiza umuhimu wa kushughulikia masoko na tunazo mbinu mbalimbali ambazo zinatumwi katika kukuza masoko ya mazao. Moja ni mfumo wa stakabadhi ya maghala. Mfumo huu una wawezesha wakulima wenye kwa kushirikiana na benki kukusanya mazao yao na kuyaweka dhamana na benki inaweza kuwalipa fedha kwa *advance* wakati wakisubiri bei nzuri zaidi ya mazao yao mfumo huu umefanya kazi vizuri katika zao la korosho na umeanza kufanya kazi vizuri katika mazao mengine kama mpunga kule Mbarali lakini siyo kwa maeneo yote, shabaha ya Serikali ni kuendeleza mfumo huu ili kuhakikisha kwamba wakulima wanapata mahali pa kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfumo mwininge unaitwa *Contract Farming* amba ni kilimo cha Mkataba huu unafanya kazi vizuri sana na mfano wake mzuri uko Kilombero. Ambako wakulima wanaomzunguka mwekezaji mkubwa wanalima na wanapata soko pale kwenye kiwanda wanauzma mazao yao na wanajipatia bei kulingana na mkataba waliowekeana baina yao na mwekezaji kuna mfumo wa Vyama Vya Ushirika kununua moja kwa moja na kuna mfumo wa ushindani unaofanywa na sekta binafsi.

Lakini Serikali vilevile haikuwaacha wakulima peke yao kwa mazao ya chakula tunayo Bodi inayonunua kwa ajili ya hifadhi ya Taifa ya Chakula na hivi ninavyoongea sasa taratibu zimeanza katika maeneo yote ambako mahindi yameongezeka ili Bodi hii ianzu kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakumbuka Bunge hili lilitunga Sheria ya kuanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Kazi ya Bodi hii itaanza msimu Bodi ya muda kuiwezesha Bodi hii iweze kukopa na kuanza kazi yake ya kununua mazao. Kwa hiyo, tunalipa suala la masoko umuhimu mkubwa kwa sababu bila ya masoko hakuna kilimo.

Baada ya maelezo hayo na kwa idhini yako sasa napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili kwa ushirikiano mkubwa ambao wametupa kwa muda wote wa miaka mitano. Tumefaidika sana, lakini vilevile ninataka kuwashukuru wananchi wa Bunda kwa kuonyesha nia ya kutaka kunichagua tena. Baada ya maelezo hayo ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

Na. 234

Nyumba kwa Waathirika wa Geita Gold Mine Mpya

MHE. ERNEST G. MABINA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi kujenga nyumba pindi uongozi wa Wilaya ya Geita utakapata viwanja kwa ajili ya Waathirika wa *Geita Gold Mine Mpya*, ambao wanaishi kwenye mahema baada ya kushindwa kesi yao na *Geita Gold Mine (GGM)*.

Je, ni lini nyumba hizo zitajengwa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya wananchi waliokuwa wakiishi katika eneo la *Mine Mpya* Wilaya Geita kushindwa kesi yao na kuhamishwa kwa amri ya Mahakama kutoka katika eneo la leseni ya uchimbaji ya kampuni ya *Geita Gold Mine (GGM)*, Serikali iliamua kuwajengea makazi mapya kwa lengo la kuwaondoa katika mazingira duni yanayowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango wa kuwapatia makazi mapya wananchi hao unaendelea kufanyika. Hadi sasa hatua zifuatazo zimeshachukuliwa katika kukamilisha zoezi hili:-

(1) Serikali imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 60 na kupima viwanja 56 katika eneo hilo.

(2) Mchoro wa nyumba za gharama nafuu zitakazojengwa katika eneo hilo kwa ajli ya wananchi hao umetayarishwa ambapo shilingi 4,715,000/= zitatumika katika kujenga kila nyumba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kiasi cha shilingi 262.040,000 ambazo zitatosha kujenga nyumba 56 za wananchi hao. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali inategemea kuitisha mkutano wa wadau mbalimbali kwa lengo la kuwashawishi kuchagia ujenzi huo.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kutoa shukrani kwa wananchi wa Geita kwa kuwa wavumilivu walipokatazwa kujenga katika viwanja vya Bombambilili.

Wamekuwa wavumilivu na niishuru Serikali kwasababu sasa hivi imeruhusu viwanja hivyo wananchi wavijenge sasa ninawaambia wananchi wa Geita kuwa wako huru kujenga katika viwanja hivyo na ninawakaribisha hata wadau wengine waje wawekeze Geita na Mheshimiwa Magufuli nimpe viwanja ili tuukamilishe Mkoa wetu. Baada ya kuyasema hayo, nauliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Serikali imesema kwamba itatafuta pesa shilingi milioni 262,040,000/- ili kukamilisah ujenzi wa nyumba hizo na Wizara hii tunajua ni kubwa na ambayo haiwezi kukosa pesa hizo badala ya kusubiri wadau kwa nini isichukue katika mafungu yake ikawajengea wananchi hao nyumba ili kuondoa adha wayoipata kwasababu mpaka sasa hivi bado wanaishi kwenye mahema?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Mabina tatizo siyo ukubwa wa Wizara tatizo ni kuwa pana majukumu ambayo yamepangwa na hayatofautiani katika umuhimu na utekelezaji wake.

Tulipokwenda pale mimi mwenyewe nilikwenda *Mine* mpya nadhani tulikwenda na Mheshimiwa Mbunge pia tulikuwa naye hali tulioikuta pale ni kwamba tuliongea na Watanzania wenzetu wa pale. Lakini pia tulimkabidhi kazi DC wa pale Mzee Shelutete, tukakabidhiana jukumu la kwamba kwanza vipatikane viwanja, halafu tupate michoro ya zile nyumba za *Low Cost Housing*, ambazo zitafaa kuwahamisha kutoka kwenye mazingira ya mahema.

Sasa tumejapata *figure* hii ambayo ni shilingi milioni 262,040,000/= katika hili jambo wote tunajukumu nalo. Tumeona kwamba Bajeti ina ufinyu kidogo ni vizuri tukishirikiana na wadau wengine kama *GGM* na Serikali, Halmashauri ya Geita ambapo Mbunge ni Mwanachama wa pale wote tushirikiane kupata ufumbuzi wa jambo hili kwasasabu linatuhusu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kutoa *funds* kwenye Bajeti hii kwa sasa hivi kwa sababu Bajeti yenyewe ni finyu sana lakini ninaamini kwamba sisi watatu wote *GGM*.

Halmashauri ya Geita, ambapo na yeye Mheshimiwa Mbunge Mabina ni mdau, pamoja na Serikali tunaweza tukapata ufumbuzi wa tataizo hili haraka iwezekanavyo. (*Makofii*)

MHE. ESTHER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mimi bado ni mlezi katika Mkao wa Geita na kwa sababu ni nafasi yangu ya mwisho leo kuwahudumia wananchi wa Mkao wa Geita, ninaomba niwalizie kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, wananchi walioelezewa hawa 56 waliokuwa katika mahema na mimi nimeshuhudia nikiwa katika Kamati ya Nishati na Madini, wamekaa kwa muda mrefu sana na leo hii tunapitisha Sheria ya ubia wa Serikali pamoja na makampuni binafsi. (*Makofi*)

Je, kwa kuwa Serikali tunajua uwezo wake ni finyu hivi sasa kwa nini tusitumie kampuni ya *GGM* kusaidia kuwajengea wananchi ambao wameathirika kukaa muda mrefu kwenye mahema? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema siyo wananchi 56, nadhani familia ziko 56. Kwa hiyo, pana tatizo pale ambalo ni kubwa. Lakini limeanzia tangu mgogoro wa kesi ile iliyokuwa inahusisha kijiji cha Mtakuja na baada ya wananchi kushindwa kesi ilikuwa wao wamekwenda pale kwa njia ambayo siyo ya kisheria.

Lakini kwa sababu ya kuzingatia pia mahitaji maalum ya wananchi wale, tumesema Serikali imechukua dhamana ya kuongea na *GGM* lakini pia kuongea na Halmahauri ya Geita kwa sababu na wao ni wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nyawazwa na Mheshimiwa Mabina na Waheshimiwa Wabunge wa Geita wengine naomba nikuhakikishieni tu kwamba suala hili hatulichukulii kwa uchache wake kwa kushirikiana tu na *GGM* wenyewe lakini na sisi pia kama wadau ni lazima tu tuingize mikono yetu humo ili tupate ufumbuzi wa jambo hili.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swalii. Kwanza nawapongeza wananchi wa Geita kwa kupata Mkao na watu wote ambao wanafanya kampeni za Makao Makuu ya Mkao ni dhahiri kabisa kwamba Geita ndiyo inayofaa kuwa Makao Makuu ya Mkao mpya wa Geita. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kuendeleza malumbano. Geita ni Wilaya ya zamani ina miundombinu yote kwa hiyo ni muhimu tu itangazwe kwamba Geita ndiyo Makao Makuu ya Mkao mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya ya Geita ina mgodi na ule mgodi unalipa mrabaha; na kwa kuwa kiasi cha fedha kinachotakiwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo familia 56 ambapo sasa ni karibia miaka minne familia hizo zinaishi kwenye mahema, wamekuwa ni wakimbizi ndani ya nchi yao.

Kwa nini Serikali isichukue sehemu ya *rent* inayotolewa na mgodi wa *GGM* na kuzungumza na Shirika la Umma la *National Housing* wajenge hata kwa kulilipa lile

shirika kidogo kidogo ili wananchi waweze kuondokana na adha hii ambayo wamekuwa nayo kwa kipindi cha miaka minne. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *mine mpya* kama nilivyosema historia yake ipo kwenye madai yaliyokwenda Mahakamani yaliyoanza kule Mtakuja. Lakini wananchi walikwenda pale kwa lengo la ku-protest. Tunaweza tukasema pia katika ujenzi wa hapa Bunge labda kuna wananchi walipewa fidia wakaondoka na wakasema sasa wakae hapa nje Bungeni waweke mahema.

Sasa ni lazima tuseme kwamba pana taratibu za kisheria zilizofuatwa ambazo Mahakama ya Ardhi ya pale Mwanza ikatoa hukumu yake. Kwa hiyo, baada ya kulipwa fidia walikuwa hawastahili. Lakini kwa sababu tatizo lile ni tatizo la msingi linalohusisha Watanzania naomba hili jambo la wakimbizi ndani ya nchi yao mimi nadhani Mheshimiwa Zitto hili siyo sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema Serikali inashughulikia tatizo lile, tumekwenda kwa hatua mbalimbali, hatua ya kwanza ni kuwatafutia viwanja, vimepatikana.

Hatua ya pili ni kutafuta namna ya kupata hizi fedha ambazo kama unavyosema ni shilingi milioni mia mbili sitini na mbili lakini hazijapangwa (*hazipo-budgeted*) hizi pesa zinazotoka kwenye mrabaha zinakwenda kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi mengine ya nchi nzima. Nasema kwa sababu na watu wa Wizara ya Fedha Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee na Mheshimiwa Mkulo walikuwa pale wamenisikia. Mimi nadhani tunakubaliana kimsingi kwamba tatizo hili ni tatizo ambalo kwa kuwa sasa tumeshapata viwanja ambalo nalo lilikuwa ni tatizo, kwa sababu kama unavyojua kwa kuwa wewe ni mdau wa Geita unajua mambo haya, pale palikuwa na uhaba wa viwanja lakini vimeshapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie wananchi wa *mine mpya* na wananchi wa Geita kwamba mimi mwenyewe nilikwenda pale na tutarudi tena tutalipatia ufumbuzi kwa kushirikiana na wadau wote. (*Makofi*)

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi nimewahi kusimama nilimaanisha kusimama kwenye swali Na. 235. Naomba radhi sana.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea na swali ninalofuata.

Na. 235

Utekelezaji wa Mradi wa Umeme – Busega

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI aliuliza:-

Kwa kuwa umeme wa Lamadi, Kalemela, Nyamikoma, Nyakaboja hadi Nyashimo na ule wa Lamadi, Mkula Hospitali, Igalukilo, Malili hadi *Ngasamo Ginnery* na Nyashimo, Nyamatembe, Shighala na Mwanangi, Badugu umekuwa ndani ya mpango wa Serikali kwa muda mrefu:-

- (a) Je, mradi huu utaanza lini na kampuni gani imeteuliwa kutekeleza mradi huo?
- (b) Je, ni fedha kiasi gani imetengwa kwa kazi hiyo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ulishaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2008/2009 kwa wakala wa Nishati Vijiji (*REA*) kutenga kiasi cha fedha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa kupeleka umeme katika vijiji vya Nyamikoma na Kalemela. Mradi huu unakadiriwa kugharimu shilingi 834,8445,000.00 fedha hizi zitatumika kwa ajili wa kilomita 12 za njia ya umeme wa msongo wa *KV 33* kutoka Magu, ufugaji wa *transfoma* ya ukubwa *KV 200* na ujenzi wa kilomita 2 za njia ya umeme wa msongo wa *KV 0.4* katika kijiji cha Nyamikoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo pia zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa kilomita 16 za njia ya umeme wa msongo wa *KV 33* kutoka Bunda, ufungaji wa *transfoma* ya *KV 100* pamoja na ujenzi wa kilomita 1 za njia ya umeme wa msongo wa *KV 0.4* katika kijiji cha Kalemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa kampuni ya kutekeleza mradi huo chini ya ufadhilli wa *REA* umekamilika na tayari taratibu za kusaini mkataba na kamapuni ya *SYMBION Power (T) LTD*, ambayo imeshinda zabuni ziko katika hatua za mwisho. Kazi ya ujenzi inatarajiwaa kuanza mwishoni mwa mwezi Julai na kukamilika mwezi J uni, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AFDB*) inafadhili mradi ujulikanao kama *Electricity V* mradi ambaa unahusu kupeleka umeme katika miji na vijiji vya Mikoa vya Mwanza na Shinyanga na kuboresha huduma za umeme katika maeneo mbalimbali yakiwemo Hospitali ya Mkula, *Ngasamo Ginnery* na vijiji vya Malili na Shighala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo utatekelezwa na Wakandarasi watakaoeuliwa kwa njia ya zabuni na kusimamiwa na *TANESCO*. Zabuni kwa ajili ya kumtafuta mshauri mwelekezi wa mradi huu ilitangazwa mwezi Julai, 2009 na tayari ripoti ya tahimini kwa uteuzi wa Mshauri Mwelekezi (*Technical Evaluation Report*) imepelekwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AFDP*) ili kupata ridhaa (*No Objection*).

Mshauri mwelekezi wa mradi atakapopatikana kazi ya uteuzi wa wakandarasi kwa kazi za ujenzi itafuata.(*Makofi*)

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona tu hamasa ya Wabunge wengi wamesimama wakitaka kuuliza maswali ya nyongeza kulingana na swalii langu hili la msingi. Kwanza naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa hatua iliyofikia, kwa sababu hii ni moja ya ahadi ambazo imekuwa ikizitao na leo hii Serikali imebainisha kwamba mradi huu sasa umeshafikia kwenye ngazi ya utekelezwaji. Ninayo maswali madogo mawili:-

(i) Kwa vile sasa mradi huu umekuwa ni wa muda mrefu na wananchi wamekuwa wakiusubiri sana mradi huu ili waweze sasa kutimiza malengo yao na hasa katika vijiji nya Kalemela na Nyamikoma, Kabita, Nyakaboja na mpaka Nyashimo. Na kwa kuwa Serikali imeshasema tayari Mkandarasi ameshapatikana na mwezi Julai mwishoni Mkandarasi anapaswa kuanza kazi. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwaagiza *TANESCO* waende maeneo haya husika wawaelimishe wananchi kwamba sasa umeme unakuja na kwamba wakae mkao wa kula kwa sababu ahadi yao imetimia? (*Makofi*)

(ii) Kwa kuwa mradi wa *Electricity V* utachukua kidogo muda kama ambavyo imeelezewa hapa, kuna suala la kukamilisha suala la uteuzi wa mshauri Mwelekezi na uteuzi wa Mkandarasi wa mradi huu. Je, Serikali sasa itaona kwamba ijaribu kufanya *fast tracking* ya mradi huu utekelezwe mapema zaidi badala ya kuchukua muda mrefu kama ambavyo imetokea kwa mradi huu wa *REA*.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kushukuru kwa pongezi alizotoa Dr. Raphael Chegeni na pia naomba kujibu maswali ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa kwanza wa Nyamikomo na Kalemela, naomba nimhakikishie na ninaomba pia iwafikie wananchi wa maeneo haya kwamba tumefikia hatua nzuri. Mkandarasi matarajio yetu ataanza kuonekana *site* kuanzia Julai 2010 kama akichelewa itakuwa mwanzoni mwa Mwezi ujao. Lakini kama nilivyosema hata kwenye kitabu chetu cha makadirio mradi huu umetengwa kama ni mionganoni mwa miradi itakayounganishwa na *grid* kupeleka umeme vijijini ukurasa wa 83.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umeshapata *commitment* ya Serikali na ombi la kwamba *TANESCO* wafike mimi nadhani siyo ombi zito, mimi nitamwomba Mzee Kingwe *TANESCO* Mwanza afanye utaratibu kwamba ile miradi ambayo inapata utekelezaji kwa Kanda ile wananchi wapate kutaarifiwa ili wajiveke kwenye mkao wa kula kama walivyosema wakisubiria utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili la *Electricity V* lilikwama kwa sababu kulikuwa na majadiliano, kama unavyojua Africa Development Bank (ADB) wao wana miradi mingi wanayofadhili, sekta ya maji, sekta ya miundombinu, sekta ya Nishati na kadhalika. Mawasiliano yao ni Wizara ya Fedha, walipomaliza masuala yao ya *Financing* ndiyo yakaja masuala yetu ya *Technical Evaluation*. *TANESCO* wamewapelekea

maelezo *African Development Bank* wakarudisha na sisi tunawapelekea tena, kwa hiyo kama nilivyosema tumefikia hatua ambayo sasa tunatarajia kwamba majibu yatakayotoka *African Development Bank* itakuwa ni ridhaa ya *No Objection* na kwa maana hiyo watakavyokuwa tayari sisi kwa upande wetu wa Serikali ya Tanzania wafadhili wakiwa tayari tutahakikisha kwamba miradi hii ya *Electricity V* inapata utekelezaji.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana mwanangu Mgogo kwa kunipa nafasi ya kumwuliza swali Waziri. Kwanza nafurahi sana na kuipongeza Serikali kwamba tayari umeme wa Puge-Ndala Mkandarasi alishafika na alishaanza kuonesha maeneo ya kuweka kambi ambapo nguzo na *Transfoma* zitawekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Bunge lako Tukufu kesho ndiyo linaagwa na tarehe 1 Agosti, 2010 ndiyo tunaacha kazi rasmi. Lakini kwa kuwa Serikali bado itaendelea kuwepo kazini na ninaamini Mawaziri wote na Manaibu Mawaziri pamoja na Rais mwenyewe wataendelea kuwepo kazini.

Je, kuna uhakika gani wa Waziri kwa niaba ya Mbunge wa Nzega ambaye ni Mbunge makini, ambaye haogopi mavuvuzela, kuhakikisha anasimamia utekelezaji wa mradi huo na unakamilika kama ulivyopangwa? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwamba Mheshimiwa Selelii ametupongeza kwa utekelezaji wa mradi huu. Ni kweli ulikuwa umechelewa lakini sasa mradi unaendelea kwa ajili ya kufikisha umeme pale Ndala na ninaamini pia kwenye Kijiji jirani cha Shapera. Lakini mradi huu una wateja wengi sana ambapo inakadiriwa ni kama 360 mpaka 400.

Kwa hiyo, ni mradi muhimu kama ilivyo miradi mingine naomba nimhakikishie tu kwamba katika ukamilishaji wa utekelezaji wa majukumu yetu tutahakikisha kwamba utekelezaji wa majukumu yetu unakwenda bila vikwazo vyovyote na upate kukamilika. Isipokuwa tu kwamba ni lazima nimwambie tu kwa sababu ya *size* ya ule unatarajiwu kukamilika katika muda wa miezi kumi na mbili au kumi na tatu ijayo.

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwa niaba ya wananchi wa Nyang'hwale napenda sasa niage rasmi Halmashauri ya Wilaya ya Geita na nimpongeze sana Mheshimiwa Ikangala Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye ameongoza kwa miaka yote kumi vizuri sana.

Nimpe ushauri wa bure Mheshimiwa Magufuli awashauri wananchi wa Chato wawahi viwanja 1500 Geita vilivyopimwa ili wajenge nyumba katika Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Geita. Baada ya hapo naomba kuuliza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa zabuni ya miradi ya *MCC* imefunguliwa na kwa miradi ya kupeleka umeme kutoka Kalumwa kwenda vijiji vya Vitongo, Ikangara, Nyarubere, Kakora, hadi Nyang'hwale ni wa siku nyingi sana.

Je, Waziri yupo tayari sasa kumshauri Mkandarasi kwa upendeleo kabisa akaanza maeneo hayo kwa sababu ni tatizo la muda mrefu na ikiwezekana afanye hivyo kabla ya tarehe moja mwezi wa nane?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni za *MCC* kama nilivyosema zilikuwa zifunguliwe tarehe 9 zimefunguliwa tarehe 9 Julai, 2010 na Zabuni zile zimefunguliwa kwa *portion* ya tatu ya miradi ya usambazaji *Transmission and Distribution* ambayo inajumuisha Mikoa sita.

Pamoja na kwamba suala la Nyang'hwale ni la muda mrefu, jambo ambao tumewasihi wakandarasi ni kwamba baada ya kuwa miradi ile ya *MCC* ambayo ilikuwa inatarajiwu itekelezwe mwaka jana imechelewa kwa sababu ya taratibu na kadhalika, sasa miradi hii ipate utekelezaji kote.

Ikiwa ni Morogoro, Tanga, Iringa, Mbeya na Mwanza yenye. Pale Mwanza kama unavyojua miradi hiyo inaunganisha maeneo ya Bukoli, Nyarugusu, Rwanagasa mpaka Katoro.

Kwa hiyo, ninakuomba kwa sababu miradi hii Mkandarasi ameshatekeleza na amepewa maagizo kwamba tunakuomba utekelezaji usisuesue naomba uniruhusu nisiseme kwamba atakuwa pale kabla ya tarehe moja mwezi wa nane ambapo najua pana kura za maoni lakini naomba nikuhakikishie kwamba kazi uliyofanya ni kubwa pamoja na Wabunge wenzako wa Geita na Wabunge wote wanaopitiwa na miradi ya *MCC*.

Sisi mmetupa jukumu hili tutahakikisha kwamba pesa za *MCA* zikitoka kwenye *Millennium Challenge Account* mkandarasi aanze utekelezaji bila kusua sua mara moja. (*Makofii*)

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii muhimu, kuwa mwuliza swal la mwisho kwa Bunge hili. Kwanza nawashukuru Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime pamoja na Mkurugenzi na Watendaji wote kwa ushirikiano ambao tumeufanya katika Halmashauri, tumefanya maendeleo makubwa ndani ya Halmashauri hiyo ambayo nimeongoza kama Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa mradi mkubwa wa umeme kutoka Tarime kwenda Itiryo ambao utawezesha wananchi wa vijiji vya Nyamwigura, Nyarero, Nyamwaga, ambapo umeme utapita pale. Je, huo mradi utakamilika lini?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Tarime tuna miradi mbalimbali, nimefurahi kwamba umefanya jambo la kiungwana umekiri kwamba Serikali ya CCM ingawa wewe ndiyo kiongozi wa pale, lakini

tumepeleka maendeleo kwa wananchi wa Tarime. Kwa maana hiyo tunatarajia kwamba watafikiria upya katika uchaguzi unaokuja mwezi wa kumi na moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pana mradi pale wa Itirio ambao ni mradi mzito kidogo kwa sababu napo unajumuisha wateja kupatiwa umeme kama 220. Ipo katika utekelezaji wa miradi yote ya Mara ambayo kwa ujumla nadhani gharama zake ni kama bilioni 4.5 kwa hiyo ni fedha nyingi zimetengwa kwa ajili ya kuunganisha umeme kwenye vijiji mbalimbali vya Mara kutokana na grid ambavyo vingine vinakwenda Bunda kwa Mzee Wasira vingine vinakwenda Rarya kwa Sarungi.

Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie kwamba katika utekelezaji huu Serikali yetu haina ubaguzi mradi huu utafanywa utatekelezwa kwa upana wake na kwa maelezo zaidi hatua za utekelezaji unione baadaye ili nikuambie kwa jana au juzi wamefikia wapi.

MHE. MTUTURA ABDALLAH MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa Wilaya ya Tunduru sasa hivi ina majimbo mawili na jimbo moja la Tunduru Kusini halijapata mradi wowote wa umeme kutoka nchi yetu ipate uhuru. Japokuwa Tunduru sasa hivi tunazalisha umeme wa ziada takribani *KW 100*. Je, Wizara yetu kwa kushirikiana na shirika hili la umeme vijiji haioni sasa umuhimu wa kupeleka umeme ule katika Kijiji cha Mbese ambacho kina hospitali ya rufaa na vile vile kuna vyuo mbalimbali vinavyofundisha wananchi wa Tunduru? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, kwa kuwa hii ni mara ya mwisho ambapo nitasimama kujibu maswali mbele ya Bunge lako hili. Tukufu naomba nitumie fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa niwashukuru wananchi wa Mkuranga kwa ushirikiano wao kwa muda wa miaka mitano hii ambapo nimekuwa Mbunge wao na naomba nitumie fursa hii kuwaambia kwamba natarajia tutaendelea kuwa pamoja katika kulisukuma gurudumu la maendeleo ya Mkuranga kwa miaka mitano ijayo. *Inshallah.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme wa Tunduru hii *figure* aliyonipa Mheshimiwa Mtutura ya *KW 1000* za ziada inanipa tabu kidogo. Kwa sababu nilikuwa najua kwamba pale tulikuwa na matatizo ya *generator* ambazo zipo pale zilikuwa zinasumbuasumbua na ndiyo maana mkakati wa sasa hivi wa muda mrefu wa kuondoa tatizo la umeme Tunduru ni kuleta umeme huu ni kuleta umeme huu wa *gas* kutoka Mtwara kuititia Nangaka kwa Mheshimiwa Mkapa kwenda Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ukishafika pale Tunduru naamini kwa sababu pale pia pana mgao huu wa majimbo tunawajibika kufikisha umeme kule kwingine Tunduru Kusini ambako Mheshimiwa Mbunge amesema umeme haujafika. Lakini naomba niseme pamoja na ziada ambayo Mheshimiwa Mtutura anasema ipo mimi nitawafikishia suala hili watalaan wa *TANESCO* kwa sababu ule mradi bado uko

mikononi mwa *TANESCO* watuangalizie suala lile la ziada lililoko pale lakini pia waangalie gharama za kusambaza umeme kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba tatizo hili linafanana na tatizo la Jimbo jipya la Nyasa kule kwa Mheshimiwa John Komba, ambako nako tutakwenda kwa Mkoa wa Ruvuma. Pia, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa, kwamba nao katika mkakati huu wa Tunduru na Mbanga kule kwa Mheshimiwa Capt. John Komba tutaweka na Namtumbo ili tukamilishe kwa pamoja utekelezaji wa umeme kwa Wilaya hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Maswali yamekwisha, sasa tunaelekea katika matangazo yetu tukianza na wageni wetu waliopo hapa Bungeni ambao kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Dunstan Mkapa ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Biashara hapa Dodoma Ndugu Martha Jashi na Jacqueline Deston. Karibuni sana Bungeni.

Wageni wa Mheshimiwa Zainab Vulu ni Zaynab Mbeyu, Husna Mbeyu na Saida Said karibuni sana hapa Bungeni. Mama yupo anafanyakazi nzuri.

Wageni wa Mheshimiwa Al– Shymaa John Kwegyir ni Haruna Mbeyu, sasa na hawa akina Zainab na Hussna sijui natumaini ndugu moja au majina tu na Said Salehe, Shufaa Said. Ahsante sana karibuni sana. Mheshimiwa Al – Shymaa yupo hapo anawajibika ipasavyo.

Wageni wa Mheshimiwa Athumani Janguo ni Haji Athumani Janguo, kijana wake ambao ni mjasiria mali, karibu sana Haji, yuko Mariam Athumani Janguo, huyu ni binti yake wa kwanza wa Mheshimiwa Janguo, Baraka Chambi Mjukuu ambaye pia ni mtoto wa Mariam, karibuni sana. Zainab Athumani Janguo, Katibu Siasa, Uenezi CCM Marekani. Karibu sana Zainab na tulikuona kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Kizota. Wahida Athumani Janguo mwanafunzi shule ya J. K. Nyerere Dar es Salaam, karibu sana. Amina Omar mwanafunzi mtoto wa shemeji yake Mheshimiwa Janguo ambaye ni Katibu Mkuu UWT Dodoma Mjini. Karibu sana Amina. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje ni wanafunzi 40 kutoka shule ya Kikombo Wilaya ya Mpwapwa wakiongozwa na Mwalimu Mkuu Mama Udoba. Karibuni sana wanafunzi wa shule ya Kikombo shule hii imekuwa ikifanya vizuri sana katika Mkao wa Dodoma na mwanafunzi wa kwanza kwa mwaka huu alitoka kwenye shule hii. Hongereni sana na muendelee kufanyakazi kwa bidii zaidi. Mama Udoba uko wapi? Ahsante sana Mama na hongera sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Idd Azzan ni wajasiriamali kutoka Tandale, Dar es Salaam ambao ni Ashura Said na Anna Cosmas, karibuni sana Bungeni.

Wageni wa Mheshimiwa Paul Kimiti ni Senator ni Wakongo wanaoishi Marekani ambao ni Alangasura, Benton Samba na Jonathan Bushaija. Karibuni Ba Ndugu, karibuni sana Bungeni hapa. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Gaudence Kayombo kutoka Chama Kikuu cha Ushirika Mbanga (MBIFAKU) ni Osmuni Mbepela Mwenyekiti wa Mifaku Karibuni sana na Mbonanei Tilia Katibu wa Bodi karibuni sana. Ujumbe kutoka *Jamii Forum* wamekuja kutembelea Bunge ambao ni Maksensi Mero karibu, Maiki Mushi, karibuni sana na Prisca Ngonyani karibuni sana Bungeni *Jamii Forum*. (*Makofi*)

Ujumbe kutoka *Kill FM Radio* ya Moshi wametembelea Bunge wakiongozwa na Ndugu Exaud Marya karibu sana. Ahsante sana *Kill FM* karibuni sana muongeze matangazo yafike nchi nzima. Namwomba na dada yangu Chonya hebu anyoshe mkono kama yupo karibu sana dada anafanyakazi *Kill FM* kule. (*Makofi*)

Wanafunzi 50 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Makole iliyopo Dodoma simameni. Ahsanteni sana. Karibuni wanangu. Bunge hili ni Bunge lenu pia. Wanafunzi 35 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *CBE Dodoma* nadhani watakuwa *basement*.

Baada ya matangazo hayo naomba niendelee na matangazo kuna wageni wa Mheshimiwa Mwadini Jecha ambao ni Nasra Ibrahim mtoto wake na Devota Deogratius. Karibuni sana vijana wetu. Baba anafanyakazi nzuri na mama pia Mkiwa Kimwanga anafanyakazi Bungeni. Wapo wageni wa Mheshimiwa Zubeir Maulid ambao ni Ndugu Mariam Idris Hamis ambaye ni mdogo wake wa Mheshimiwa, karibu sana Mariam na Hadija Haji Hamis ambaye ni Mjukuu wa Mheshimiwa Zubeir.

Mheshimiwa kumbe una mjukuu Bwana hongera. Karibuni sana Mariam na Hadija hapa Bungeni baba anafanyakazi nzuri sana. Ninaye mgeni wangu Kaka yangu Ndugu Ramadhani Nyagani kutoka Mwanza karibu sana hapa Bungeni amekuja kwa ajili ya kujiunga na Ndugu kule Kongwa kwa ajili ya Misa maalum ya Mkesha wa Kumbukumbu ya kifo cha Mama yangu Marehemu Mdala Kazalina Chonyo ambayo inafanyika kesho kule Kongwa. Naomba Ndugu zangu wa Kongwa tuhudhurie Mkesha wa kesho.

Matangazo ya kazi. Kikao cha Kamati ya Uongozi naomba wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati ya Uongozi leo tarehe 15 mwezi wa 7 saa saba mchana katika Ukumbi wa Spika.

Lipo tangazo kwamba wajumbe wote wa Kamati ya Hesabu ya Mashirika ya Umma mkutane leo Msekwa B saa saba kutokana na kwamba Mheshimiwa Spika, tarehe 21 Januari, mwaka huu, 2010 aliagiza Kamati pamoja na majukumu yake ishughulikie suala la ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kumtaka mkaguzi huyo afanye ukaguzi maalum juu ya gharama halisi na taratibu za manunu zilizotumika katika ujenzi wa nyumba ya Gavana na Naibu wake Mjini Dar es Salaam.

Sasa kazi hiyo imeshafanywa imekamilika kwa hiyo, wajumbe hao wakutane ili kuzingatia Kamati hiyo. Mezani hapa ninayo nakala hiyo. (*Special Report on the construction of two residential Houses of the Bank of Tanzania*) kwa hiyo, mukutane saa saba Kamati ya Bunge ya Hesabu ya Mashirika ya Umma kwa ajili ya madhumuni niliyoyasema hapa.

Mheshimiwa Omari Kwaangw' Mwenyekiti Kamati ya Huduma za Jamii anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii kwamba leo tarehe 15 saa saba mchana katika ukumbi namba 231 mukutane jengo la utawala. Mheshimiwa Kwaangw' ukumbuke na Kamati ya Uongozi inakutana pia.

Mheshimiwa William Shellukindo Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini anawaomba saa saba leo wajumbe wa Kamati hiyo ya Nishati na Madini kukutana ukumbi 219.

Waheshimiwa Wabunge kesho saa nne asubuhi mara baada ya kipindi cha maswali kutakuwa na kikao muhimu sana cha Wabunge wote wa CCM ukumbi wa Msekwa tuna ugeni maalum wakati huo.

Naona kuna baadhi ya wapinzani wanauzu wapi saa nne jamani Ukumbi wa Msekwa. (*Makofit*)

Tangazo la Ofisi ya Bunge inaomba niwatangazieni kwamba wale Wabunge wote ambao wamenunua hisa za Benki ya wanawake wakajisajili rasmi kwa maafisa wa benki hiyo ambao wapo mapokezi jengo la utawala leo tarehe 15 Julai, 2010. Wale Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmenunua hisa katika Benki hii ya wanawake mnaombwa mwende mkajisajili rasmi na Maofisa wa Benki hiyo wapo jengo la utawala mtaelekezwa.

Tangazo linalofuata ni muhimu naomba tusikilizane vizuri kwa ajili ya nyendo zetu zilizoko leo na kuendelea. Waheshimiwa Wabunge kuna nyaraka kadhaa ambazo zimegawiwa humu ndani ya Bunge. Naomba niwatangazieni kwamba hizo nyaraka ni muhimu sana na zimegawiwa humu au baadhi yake ziko katika *pigeon holes* zenu, tunaomba sana mzipitie kila mmoja.

Nyaraka ya kwanza ni tafsiri ya lugha ya Kiswahili ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi ambayo ninayo nakala yake hapa. Sheria ile ambayo kama kawaida ilitungwa kwa Kingereza sasa iko katika Kiswahili. Kwa hiyo sote tuwe na nakala zake na asiyekuwa nayo iko kwenye *pigeonhole* pale kwa ajili ya matumizi muhimu ya siku zijazo.

Kingine ni kwamba ipo Kanuni ya gharama za Uchaguzi za mwaka 2010 kama unavyojua sheria lazima inakwenda na kanuni zake na zimeshatoka na zenyewe ziko *available* tuzipitia katika masunduku yetu kama huna nakala.

Tatu ni kwamba iko amri ya viwango vya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010. Tukumbuke katika sheria ile tulimpa Waziri mhusika mamlaka ya kutangaza viwango vya juu vya matumizi ya fedha katika masuala ya Uchaguzi.

Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge mpitie. Nitumie fursa hii kuwaambia mavuvuzela wote jamani kuna gharama za juu siyo kutumia huko.

Hili ni suala la kisheria, kwa hiyo, kila mmoja anayetaka kugombea katika Uchaguzi huu ni vizuri afuatilie jambo hili ili kujua viwango vilivyoidhinishwa katika matumizi ya gharama za Uchaguzi wa mwaka 2010. (*Makofi*)

Pia iko nyaraka ya nne ambayo ni Muswada ya Sheria ya Ubia wa Umma na Secta Binafsi (*Public Private Partnership (PPP)*). (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kama mtakavyoona kwenye *Order Paper* yetu baada ya muda si mrefu tutaingia katika Muswada wa Sheria ya Serikali unaohusu Ubia Kati ya Serikali na Kampuni Binafsi wa mwaka 2010 (*The Public Private Partnership Bill 2010*). Sasa Muswada huu kama mnavyofahamu siku chache zilizopita Serikali ilitufanya semina hapa Bungeni ili kupata maoni ya Wabunge na Wadau kuhusiana na Muswada huu.

Baada ya maoni yale kuwa ni mengi na mazuri yanayoboresha Muswada ule Serikali imechapisha upya Muswada huo. Kwa hiyo, nakala zilizogawiwa huku ndani na kama hakuna iko kwenye *pigeon holes* ni nakala mpya inayozingatia mapendekezo yenu na marekebisho yenu tumeshagawiwa.

Kwa hiyo, kila atakayetaka kuchangia ni vizuri wazingatie mabadiliko ambayo yamefanywa. Baadhi ya mambo yameshakubalika.

Vile vile kuna *schedule of amendment* ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu sheria hiyo ambayo ni ukurasa mmoja tu na yenyewe imeshagawanywa humu ndani ni vizuri kabla hujachangia ukapitia ili kuona marekebisho yake yanahu nini. Kwa kweli maoni mengi yamezingatiwa. Kama nilivyosema mwanzoni wale wote watakaoomba kuchangia Muswada huu nitawapa nafasi waweze kuchangia.

Baada ya matangazo hayo yote nimepata barua nyingi sana za Wasukuma wanauliza dada yangu Chonyo ameolewa? Nawaambia bado hajaolewa. (*Kicheko/Makofi*)

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Ubia kati ya Serikali na Kampuni Binafsi wa Mwaka 2010
(The Public Private Partnership Bill, 2010)

(Kusomwa Mara ya Pili)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Bila shaka, kwa hali halisi ya leo, utaniruhusu niseme machache kabla ya kuwasilisha Muswada huu Sheria ya Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2010 [*The Public Private Partnership Act of the year 2010*].

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia na mimi pia leo napenda kutumia fursa hii adimu, kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema, kwa kutujalia sote kufikia siku ya leo. Kwa hakika, kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leo ni siku ya pekee kwani leo ni siku ya kazi ya mwisho baada ya kuhitimisha Mikutano 20 na vikao vingi vya utumishi ambao nadhani umetukuka kwa wananchi wa Tanzania kwa muda wa miaka mitano (5) iliyopita. Siku moja iliyobaki (yaani kesho) ni siku ambapo Bunge litaahirishwa na Mheshimiwa Rais na hatimaye kuvunjwa rasmi kwa Tangazo katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr.Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuwa na imani na mimi kwa kunipa dhamana ya kuwa Waziri wa Nchi, kwanza katika Ofisi ya Rais, Utawala Bora na baadaye katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namtakia kila la kheri na fanaka tele na Mwenyezi Mungu azidi kumjalia afya njema, hekima na busara ili aendelee kuiongoza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, pia napenda kutoa shukrani za dhati, kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais muda wote huu na pia kwa kutushauri na kutuongoza vema. Yeye pia tunampongeza kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi, kugombea Urais wa Zanzibar. Tunatarajia mafanikio na ushindi katika Uchaguzi Mkuu na Mwenyezi Mungu atamjalia afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, kwa uongozi wake wa busara na maelekezo yake yaliyowezesha Ofisi yetu kutekeleza majukumu yake kikamilifu na pia kwa usimamizi mahiri wa utekelezaji wa shughuli za Serikali hasa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Dr. Mohamed Ghalib Bilal, kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi, kuwa Mgombea Mwenza. Nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri bila kumsahau Ndugu yangu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushirikiano mkubwa walionipa hasa katika nafasi yangu kama Mnadhimu Mkuu wa Serikali Bungeni. Nawatachia ushindi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana wewe, lakini pia Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa kuliongoza Bunge letu kwa mafanikio makubwa. Nawashukuru pia Wabunge wa Vyama vyote kwa ushirikiano wao. Nawashukuru pia Makamishna wenzangu wa Tume ya Bunge, Katibu wa Bunge kwa ushirikiano na bidii katika utekelezaji wa jukumu letu muhimu la kuwatumikia Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima nikiri kuwa bila ushirikiano wa dhati niliopata kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Peniel Lyimo, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Fanuel Mbonde, Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi zote na Vitengo vyote vilivyopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Watumishi wa Ofisi yangu Binafsi na watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, kazi yangu ya kuongoza eneo la Sera, Uratibu na Bunge katika Ofisi ya Waziri Mkuu, ingekuwa ngumu sana. Nawashukuru sana na ninawataenia kila la kheri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, kwa mara nyingine, nawashukuru tena wananchi wa Wilaya ya Mbulu, kwa kunififikasi katika nyumba hii. Kwa nyakati tofauti, nimewashukuru kwa mapenzi na ushirikiano wao kwangu. Hali hii imeleta utulivu na maendeleo katika Wilaya yetu. Sasa hivi kuna kila aina ya ishara kuwa wataniwezesha tena kurudi katika nyumba hii. Kwa mara nyingine, nawahakikishia ushirikiano, uchapakazi na uadilifu ambao ndiyo jadi yetu. Aidha, naishukuru sana familia yangu, mke wangu na watoto, kwa ushirikiano wa dhati walionipa na uvumilivu mkubwa waliokuwa nao wakati nikiwa nje ya familia nikitekeleza majukumu ya umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Ubua wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2010 (*The Public Private Partnership Act, 2010*) kama ulivyorekebishwa na kuchapishwa upya, sasa Usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada wa Sheria ya Ubua wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, unapendekeza kutunga Sheria ya Ubua wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya Mwaka 2010, kwa lengo la kuweka mfumo wa kisheria na wa kitaasisi wa kusimamia miradi na huduma itakayoanzishwa na kuendelezwa kwa ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wa Sheria, kama ulivytangaza hapo awali, ulichapishwa kwa mara ya kwanza kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 18 Juni, 2010 ikiwa ni Toleo Maalum la Miswada ya Sheria, Namba 4. Muswada ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza tarehe 25 Juni, 2010. Muswada huu ulisambazwa na kujadiliwa na umma (*Public Hearing*) kwenye semina iliyohudhuriwa na wadau wapatao 399, kati yao ni Wabunge 155, ikiwa ni pamoja na Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge za Katiba, Sheria na Utawala pamoja na Fedha na Uchumi. Semina iliyofanyika tarehe 7 Julai, 2010 kwenye ukumbi wa Pius Msekwa, Dodoma. Aidha, wadau wengine waliohudhuria ni pamoja na Wawakilishi wa Sekta Binafsi; Wawakilishi wa Nchi za Nje na Mashirika ya Kimataifa; Wawakilishi wa Wizara, Mikoa, Idara na

Taasisi za Serikali; Wawakilishi wa Taasisi za Dini; Wawakilishi wa Asasi Zisizokuwa za Kiserikali na za Kiraia na Wawakilishi wa Vyombo vyta Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada unaowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu ulijadiliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi jana tarehe 14 Julai, 2010. Napenda kuzishukuru sana Kamati za Kudumu za Bunge za Katiba, Sheria na Utawala na Fedha na Uchumi, kwa mwongozo na maoni yaliyotolewa. Aidha, nazishukuru Kamati za Kudumu, kwa kuratibu vyema semina ya Wadau. Serikali imefarijika sana kwa fursa ile kwa kuwa imewezesha kupatikana kwa maoni na mapendekezo ambayo yamesaidia ipasavyo kuboresha maudhui ya Muswada huu. Kwa niaba ya Serikali, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na Wadau wote walioshiriki katika kuboresha maudhui ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukweli kwamba mfumo wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi umekuwepo kwa miaka mingi katika kutoa huduma za jamii kama vile Afya na Elimu, bila ya kuwepo mfumo wa kisheria na kitaasisi wa kuratibu na kusimamia utekelezaji wake, ni dhahiri kuwa suala hili ni jipya kwa sababu imechukua sura mpya ya kuhusisha makampuni binafsi ya nje na ya ndani. Ndiyo maana tunaanza na ni faraja kwa Serikali, bila shaka na Bunge, kwamba wananchi kupitia wawakilishi niliowatajaa awali, wameshiriki katika mchakato wa maandalizi ya Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, hakuna Sheria yenyе mfumo mahsusini inayosimamia miradi ilioanzishwa na kutekelezwa kwa ubia wa aina hii. Pamoja na kutokuwepo na mfumo wa kisheria na kitaasisi wa Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, mafanikio fulani yamepatikana katika kusimamia na kutekeleza ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma kama vile Benki ya Taifa ya Biashara (*NBC*), *NMB*, Benki ya *CRDB*, Kampuni ya Bia Tanzania, Kampuni ya Sigara Tanzania, Kampuni ya Sukari ya Kilombero na Kampuni ya *Saruji Wazo Hill*. Kwa upande mwingine, Asasi mbalimbali za Kidini zimeshirikiana na Serikali kutoa huduma za elimu, afya na maji kwa miaka mingi. Hata hivyo, kukosekana kwa mfumo madhubuti wa kisheria na kitaasisi, kumesababisha baadhi ya mashirika yaliyobinafsishwa kutofanya vizuri kwa mfano, Shirika la Reli Tanzania; Kitengo cha Upakuaji na Upakiaji Makasha katika Bandari ya Dar es Salaam; Shirika la Ndege Tanzania; Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Jiji la Dar es Salaam; Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (*TANESCO*) na pia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria inayopendekezwa kutungwa, inakusudia kuweka mazingira ya kuvutia sekta binafsi kushirikiana na sekta ya umma katika uwekezaji wa miradi na huduma za ubia. Sambamba na Sheria hii mpya, Sheria mbalimbali zitafanyiwa marekebisho ili ziweze kuwiana na Sheria inayopendekezwa ikiwa ni pamoja na Sheria ya Uwekezaji Tanzania, Sura 38 na Sheria ya Manunuzi ya Umma Sura 419. Aidha, ili kuimarisha utekelezaji na usimamizi wa Sheria

inayopendekezwa, Kanuni na Miongozo itakayoweka mazingira wezeshi ya kuendeleza na kuimarisha ubia huu itaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada huu, ni kuwasilisha mapendekezo ya kutunga Sheria ya Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya Mwaka 2010 kwa nia ya kuweka mfumo wa kisheria na wa kitaasisi wa kusimamia, kutekeleza, kuendeleza, kuratibu na kutathmini miradi ya ubia itakayoanzishwa baina ya Serikali na Sekta Binafsi. Pamoja na mapendekezo hayo, Sheria hii inakusudia kuanzisha Kitengo cha Uratibu wa miradi ya ubia kwenye Wizara yenye dhamana ya Uwekezaji kitakachoshughulikia masuala yote ya uhamasishaji na uratibu pamoja na kufanya uchambuzi wa awali wa miradi na huduma za ubia. Vilevile inapendekezwa kuanzisha Kitengo kwenye Wizara yenye dhamana ya fedha kitakachoshughulikia masuala ya fedha (*fiscal risk allocation*) na kuidhinisha miradi kwa ajili ya utekelezaji. Hii ikiwa na maana kwamba Kitengo kwenye Wizara yenye dhamana ya fedha ndicho chenye uamuzi wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni kama ifuatavyo:-

1. Kuweka misingi ya kisheria, kanuni na taratibu za uendeshaji na usimamizi wa miradi na huduma za ubia kwa kutambua haki na wajibu wa wadau muhimu, yaani sekta ya umma na sekta binafsi. Kanuni, Taratibu na Miongozo itahusisha maeneo yafuatayo:-

- (a) Kuainisha aina ya miradi ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi;
 - (b) Uanzishwaji, uchambuzi na upitishwaji wa miradi ya ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi;
 - (c) Mgawanyo wa athari (*optimal risk allocation*) kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
 - (d) Mchakato wa ununuzi utakaoweka bayana utaratibu ulio wazi na wa kiushindani utakaotumia Sheria ya Ununuzi ya Umma;
 - (e) Kujenga uwezo wa kufanya majadiliano; na
 - (f) Kuandaa mazingira wezeshi ya upatikanaji wa rasilimali ili Sekta Binafsi ishiriki ipasavyo katika miradi hii, kwa kubainisha mfumo na vyanzo vya rasilimali, fursa katika miradi hii, uhamasishaji, kugharamia washauri waelekezi, kufanya upembuzi yakinifu na kutoa ushauri wa uchaguzi wa miradi (*transaction advisors*).
2. Kuainisha mfumo wa kitaasisi wa uendeshaji na usimamizi ambapo:-
- (i) Wizara, Idara, Taasisi na Serikali za Mitaa, zitahusika katika utekelezaji wa miradi hii ya ubia; na

(ii) Kuanzisha Vitengo vya Ubia (*PPP Units*) kwa ajili ya uratibu na uchambuzi wa masuala ya fedha.

3. Kuainisha misingi ya mikataba ya ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

4. Marekebisho ya Sheria ya Uwekezaji, Sura ya 38 ili Sheria hiyo itambue kuwepo kwa Idara ya Uratibu wa Miradi na shughuli zote za Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tano. Sehemu ya Kwanza, inahusu masuala ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Sheria inayopendekezwa, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya baadhi ya maneno na misamiati iliyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili, inahusu kuanzishwa kwa Kitengo cha Uratibu wa Ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi katika Wizara yenyeye dhamana ya Uwekezaji, kitakachoshughulikia masuala yote ya uhamasishaji na uratibu pamoja na kufanya uchambuzi wa awali wa miradi na huduma za ubia. Vilevile, sehemu hii inapendekeza kuanzishwa kwa Kitengo kwenye Wizara yenyeye dhamana ya Fedha kitakachoshughulikia masuala ya fedha na kuidhinisha miradi kwa ajili ya hatua za utekelezaji. Aidha, majukumu ya wadau muhimu ikiwa ni pamoja na Mamlaka za Udhibiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara za Kisekta, Serikali za Mitaa na Wabia wa Sekta Binafsi yameanishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, inatoa mapendekezo ya masharti kuhusu ushiriki wa wabia wa umma na binafsi katika kuanzisha, kusimamia, kutathmini na kuratibu miradi na huduma za ubia wa sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne, inapendekeza masuala ya jumla ambayo yanajumuisha usimamizi, ufuutiliaji na tathmini, mgongano wa maslahi, uwezeshaji wananchi na adhabu kwa wale watakaovunja Sheria hii. Aidha, inatoa Mamlaka kwa Waziri kutunga Kanuni za kuwezesha utekelezaji wa Sheria hii kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano, inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uwekezaji, Sura ya 38, ili kuainisha majukumu ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania katika kuendeleza miradi na huduma za ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Philip Marmo. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia uchambuzi wa Muswada huu, karibu sana Mheshimiwa kwa niaba ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. PINDI H. CHANA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa maelezo kwa niaba ya Kamati, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu, kwa kunipa kibali cha kuwa Mbunge kwa kipindi cha miaka mitano. Vilevile niishukuru sana familia yangu, watoto na mume wangu, kwa kunivumilia kwa huduma nyingi nilizonazo kwa kipindi hicho cha mika mitano. Zaidi sana nawashukuru wanawake wote wa Mkoa wa Iringa, Wanyalukolo wote wa Mkoa wa Iringa na Njombe, ninawaambia Jumatatu tarehe 19 mwezi Julai, 2010 tutakuwa pamoja wakati nachukua fomu. Sitachelewa kama walivyoniagiza na hivyo nasema ahsanteni sana kwa vigelegele ambavyo wameandaa. Aidha, ninawashukuru sana Wabunge wenzangu ambao kwa heshima waliweza kunipa kibali cha kuwa mwakilishi katika taasisi mbalimbali kwa niaba ya Bunge ndani na nje ya nchi ya Tanzania. Vilevile ninashukuru sana Serikali ya Chama Tawala, kwa kuweza kutuongoza vema Watanzania kwa kipindi hiki cha miaka mitano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, nianze sasa kwa kusema kwamba kwa mujibu wa Kanuni ya 86(v) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2007, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Muswada wa Sheria ya Ubina baina ya Serikali na watu au Kampuni binafsi kupitia mkataba maalum wa mwaka 2010. Maoni haya ninayawasilisha kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuipelekea Kamati yangu kazi ya kushughulikia Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007 na kuelekeza kuwa tushirikiane na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, tarehe 7 Waheshimiwa Wabunge wote na wadau mbalimbali walikutana katika semina mahsus kwa ajili ya kuchambua Muswada huu. Kikao hicho kilifanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa ambapo maelezo yalitolewa. Aidha, ufanuzi kuhusu namna ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership*) yalitolewa pamoja na kuelezea chimbuko la Muswada ulio mbele ya Bunge hili. Katika semina iliyowakutanisha Wabunge, Serikali na wadau wa ubia unaopendekezwa, hoja, maoni mbalimbali yalitolewa na kupatiwa ufanuzi kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa sehemu kubwa ya michango ya Waheshimiwa Wabunge na wadau walio wengi, ilihitaji kufanya marekebisho ya Muswada husika. Kutokana na usikivu wa Serikali ya Awamu ya Nne, Muswada huu ulichapwa upya, tarehe 10 Julai. Tunaipongeza Serikali kwa usikivu, umakini na kujali maoni ya wawakilishi wa wananchi na wadau waliota mapendelekezo ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe fursa hii pia kuwashukuru sana wadau waliotoa maoni yao na kusaidia kuuweka Muswada huu katika sura ya sasa. Wadau hao walitoka Asasi zisizo za Kiserikali, Asasi za Kidini yaani *Faith Best Organization*, wanataaluma mbalimbali, mashirika ya maendeleo pamoja na Idara na Taasisi za Serikali. Uratibu huu wa kukutana na wawakilishi kutoka Taasisi za Serikali na wadau mbalimbali kwa pamoja umesaidia kwa kiasi kikubwa na unahitaji kuendelezwa katika uchambuzi wa Miswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, Muswada tunaoujadili leo, ulichapwa tena ili kuzingatia maoni na mapendekezo yaliyotolewa, jambo lililosababisha Kamati mbili za Bunge, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Fedha na Uchumi kukutana tena jana tarehe 14 Julai, 2010 ili kujadili na kutafakari madhumuni na mambo mengine ya msingi yaliyohusu Muswada huu. Katika kipindi hicho, Mheshimiwa Philip Marmo, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, alifafanua kwa kina madhumuni, maudhui na sababu za Sheria inayopendekezwa. Aidha, Mheshimiwa Waziri alirejea maoni yaliyotolewa wakati wa semina ili kufafanua vifungu na dhana mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maelezo yaliyotolewa, wajumbe walipenda kujiridhisha kuhusu namna mapendekezo hayo ya marekebisho ya Sheria yanavyoweza kuboresha utekelezaji wa Sheria husika kama alivyoeleza mtoa hoja. Aidha, Kamati ilitafakari kwa kina na kutaka kujua kama mapendekezo hayo yanakidhi mahitaji ya kimsingi kuhusu utungaji na urekebishi haji wa Sheria pasipo kukiuka Sheria Mama yaani Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nafurahi kutoa taarifa kuwa, mapendekezo ya Serikali kwa ujumla yamezingatia mambo yote muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maudhui na shehemu za Muswada, kama alivyoeleza mtoa hoja muda mfupi uliopita, Muswada ulipowasilishwa kwenye Kamati baada ya Kusomwa Mara ya Kwanza, ultajwa kuwa na Sehemu Kumi na Moja na kwamba unapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria mbalimbali Kumi na Moja kama zilivyotajwa na mtoa hoja. Mionganini mwa Sheria hizo ni Sheria ya Gharama za Uchaguzi (*The Election Expense Act*) Na. 6 ya Mwaka 2010, Sheria ya Mawasiliano ya Electroniki na Posta (*The Electronic and Postal Communications Act*) Na. 3 ya Mwaka 2010 na Sheria ya Uchuguzi (*The National Election Act*) Sura ya 343. Katika kikao cha tarehe 5 Julai, 2010 mtoa hoja pia aliwasilisha Jedwali la Marekebisho na kutoa ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara ya pili sasa Serikali inaleta mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Gharama za Uchaguzi na Sheria ya Mawasiliano ya Electroniki na Posta tangu Bunge lilipopitisha Sheria hizi. Mara ya kwanza, ilikuwa ni tarehe 17 Aprili, 2010 ambapo katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho, Serikali ilipendekeza kubadilisha Sheria hizi pamoja na Sheria nyingine. Jambo la msingi kuhusu mapendekezo haya ni azma ya Serikali ya kuboresha Sheria hizo na kuweka sawa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla marekebiso ya Sheria zinazopendekezwa yanatokana na nia njema ya Serikali ya kusimamia Sheria za Bunge kwa ufanisi. Kamati imeridhika kuwa dhamira hii ni njema na inapaswa kuungwa mkono. Jambo muhimu

kuzingatia ni jinsi marekebisho yanayopendekezwa yanavyoweza kuondoa upungufu unalegwa. Kwa maeleza hayo, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati, baada ya maelezo ya kina yaliyotolewa na mtoa hoja, Wajumbe walipata fursa ya kuhoji masuala mbalimbali ambayo yalipatiwa majibu katika Kikao cha Kamati. Pamoja na hayo, Kamati ina maoni na ushauri kuhusu matumizi ya lugha, maoni ya jumla na ushauri kuhusu Ibara mbalimbali za Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya lugha na sarufi, katika kikao cha Kamati, Wajumbe walitoa ushauri uliopokelewa na Serikali na kusababisha Muswada huu uwe katika hali hii pamoja na Jedwali la Marekebisho. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema, (Mb), Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa umakini mkubwa katika kufanya kazi hoja zilizotolewa na Kamati wakati wa kuchambua Muswada huu. Usikivu na ushirikiano wake umesaidia kuboresha mapendekezo ya Serikali kuhusu Marekebisho ya Sheria mbalimbali kama zilivyobainishwa muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maudhui ya Muswada, kwa ujumla Kamati ina maoni kuwa Muswada huu utawezesha Sheria zinazobadilishwa kuwa katika Sura ya Kutekelezeka kwa ufanisi zaidi kwa kuondoa upungufu uliojitekeza wakati wa utekelezaji wake. Aidha, mapendekezo ya Serikali yatawezesha Sheria husika kusomeka kwa maana iliyokusudiwa na Bunge sambamba na kuendana na mabadiliko ya fedha na ongezeko la uvunjifu wa Sheria. Kamati inashauri kuwa marekebisho haya yaende sanjari na kuimarisha usimamizi wa Sheria hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na maoni hayo kwa ujumla, Kamati pia inatoa maoni yake katika maeneo mbalimbali ya Muswada wa Sheria uliowasilishwa. Mojawapo ya maeneo hayo ni Sehemu ya Tatu ya Muswada huu hususan Ibara ya 6, inayopendekeza marekebisho ya Kifungu cha 96(3) cha Sheria ya Madini na 14 ya Mwaka 2010. Ni maoni ya Kamati kuwa mapendekezo haya yamezingatia ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati Bunge lako Tukufu lilipoipitisha Sheria Namba 14 ya Mwaka 2010. Aidha, mapendekezo ya Serikali yatasaidia kuboresha Sheria ya Madini na kuweka mazingira bora ya Kibiashara katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sehemu ya Nne ya Muswada huu, mapendekezo ya Serikali yanalenga kuifanya Marekebisho Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366. Kamati ina maoni kuwa ufanuzi unaofanywa wa Ibara ya 8 hadi 16 za Muswada wa Sheria tunaoujadili, utarahisisha Sheria husika pamoja na kuzingatia haki za msingi za Mwajiri na Mwajiriwa. Pamoja na hivyo, Kamati inashauri kuwa mara zote Serikali inapopendekeza marekebisho ya Sheria iongeze umakini katika kufanya hivyo ili kuepuka kasoro zinazoweza kusababishwa na marekebisho ya Sheria iwapo mapendekezo hayo yatapitishwa na Bunge.

Meshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sehemu ya Sita, Saba, na Tisa, Kamati iliridhika na marekebisho pendekezo kwa kuzingatia maoni kuwa kuwianisha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya Mwaka 2010, ni jambo la msingi ambalo litawezesha utekelezaji na usimamizi wa Sheria kuwa rahisi na wenyewe ufanisi. Aidha, kutokana na usikivu wa Serikali ya Awamu ya Nne, hoja nyingi zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa majadiliano ya Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge na Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge, kuhusu Madaraka ya Msajili wa Vyama vyta Siasa zimezingatiwa katika mapendekezo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Ibara ya 23 inayopendekeza marekebisho katika Kifungu cha 9 kuhusu tamko la gharama watakazotumia Wagombea, kama sote tunavyofahamu, katika Mkutano wa Kumi na Tisa, Bunge hili lilifanya marekebisho yaliyolenga kuongeza siku kutoka Tano (5) hadi Saba (7). Katika Muswada huu, Serikali pia inapendekeza kurekebisha Kifungu kinachohusu muda wa kutoa tamko la gharama kutoka siku tano (5) kabla ya uchaguzi hadi siku saba (7). Ni maoni ya Kamati kuwa mapendekezo haya yamezingatia sana hali halisi na mazingira ya utekelezaji wa Sheria. Hata hivyo, napenda kusema kuwa ni wazi mapendekezo haya yalizingatia majadiliano yaliyoyokuwa kila mara ndani na nje ya Bunge jambo ambalo linapaswa kupon gezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sehemu ya Tisa (9) na Kumi (10) ya Muswada huu ambapo Serikali inapendekeza kuifanya marekebnisho Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamalaka za Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288. Kamati ina maoni kuwa iwapo Bunge litapitisha Sheria inayopendekezwa, itasaidia sana kukabiliana na hali inayolalamikiwa. Uzoefu umeonyesha kuwa kuna malalamiko kuhusu Watendaji wa baadhi ya Halmashauri nchini, kutekeleza au kubadilisha miradi mbalimbali pale Mabaraza ya Madiwani yanapokuwa yamevunjwa. Jambo hili si jema na ni kinyume na misingi ya kuwapa nguvu wananchi kuji amilia mambo yanayowahusu kwa kupitia Wawakilishi wao. Kamati inaipongeza Serikali kwa mapendekezo haya yanayolenga kudhibiti uanzishaji mradi mpya au ubadilishaji wa mradi wowote ulioanzishwa kabla ya Baraza kuvunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 42 kama ilivyowasilishwa katika Jedwali la Marekebisho kwenye kikao cha Kamati, inalenga kuongeza umri wa Askari kustaafu. Kamati ina maoni kuwa mapendekezo haya yanaonesha usikivu wa Serikali kuhusu maoni ya Wabunge katika Mikutano ya Bunge ili yopita. Ni kweli kuwa umri wa kustaafu kwa Mujibu wa Sheria za awali ulisababisha kuwapoteza Askari wazoefu na wenyewe nguvu pale wanapostaafu. Napenda kuliomba Bunge lako Tukufu likubali mapendekezo haya ili kuliwezesha Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji kuendelea kuwatumia Askari wenyewe uzoefu wa kutosha na nguvu katika kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu, naomba nikushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niwasilishe maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Jaji Frederick M.

Werema, Mwanasheria Mkoo wa Serikali pamoja na wataalamu wa Ofisi yake kwa ushirikiano na ufanuzi walioutoa kwa Kamati yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru sana na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa umakini na michango yao ya kina wakati Kamati ilipochambua Muswada huu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti, Mheshimiwa Ramadhani Athumani Maneno na Makamu wa Mwenyekiti. (*Makofi*)

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Sephen J. Galinoma, Mheshimiwa Rajab H. Juma, Mheshimiwa Riziki O. Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Abubakar K. Bakary, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbiri, Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshima Salim Yussufu Mohamed, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu na Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru.

Vilevile napenda kuwashukuru Watumishi wa Ofisi ya Bunge wakiwemo Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Athuman Husseini na Elihaika Mtui, chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashilila kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Pindi Chana kwa kusoma maoni ya Kamati. Wasiomfahamu vizuri Mheshimiwa Pindi Chana, ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi. Chombo kikuu chenye maamuzi mazito na nyeti ndani ya Chama cha Mapinduzi. Natumaini salamu zako kwa akina mama wa Iringa zimefika salama, tunakuombea kila la kheri.

Sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ili atoe maoni ya Kambi hiyo kuhusu Muswada huu. Namwona Mhandisi Mnyaa. Karibu sana Mheshimiwa na baada ya Mheshimiwa Mnyaa, uchangiaji utaanza na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo ajiandaye. Mheshimiwa Mnyaa.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI – OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Waziri Mkoo, Sera, Uratibu na Bunge, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, Ofisi ya Waziri Mkoo, kuhusu Muswada wa Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa mwaka wa 2010 (*Public Private Partnership Act, 2010*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria utakaosimamia ubia wa watu au kampuni binafsi katika miradi ya Serikali, *Public Private Partnership Act, 2010* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(vi), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa namna ya kipekee, niwapongeze Waheshimiwa Profesa Ibrahim Haruna Lipumba, Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wananchi *CUF*, Mheshimiwa Juma Duni Haji na Maalim Seif Sharif Hamad, Katibu Mkuu, wote kwa kuchaguliwa kwa asilimia isiopungua 99% kugombea nafasi za Urais wa Jamhuri ya Muungano na Urais wa Zanzibar. Naamini kuwa Watanzania, kama kutakuwa na uchaguzi ulio huru, haki na wazi, watawapa ridhaa ya kuongoza Taifa letu ili na wenzetu wapate fursa ya kuwa Mawaziri Vivuli na sisi tupate fursa ya kutekeleza yale tuliyokuwa tukishauri kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano iliopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Dr. Mohamed Gharib Bilal na Dr. Mohammed Ali Shein, kwa kuchaguliwa kwao kuwa wagombea kwa tiketi ya CCM katika nafasi ya Urais wa Jamhuri na ile ya Zanzibar. Kwa kuwa, Dr. Shein ni mtu anayetoka Jimboni kwangu na kwa kuwa ameahidi kuleta siasa za ustaarabu, sitegemeli kuona vurugu za aina yoyote Jimboni Mkanyageni na itakuwa kielelezo halisi cha ahadi yake ya siasa za ustaarabu na kwa vile sote ni ndugu, naamini tutashindana kwa hoja, sera na sio matusi wala kukashifiana. Nawatakia kila la kheri, nawaomba Watanzania watupatie ridhaa timu ya *CUF* ili waone mabadiliko zaidi katika kuleta maendeleo ya nchi yetu na waone shilingi ya Tanzania itakavyodhibitiwa ili thamani yake isianguke ovyo ovyo kutokana na Sera sahihi za kiuchumi za Chama cha Wananchi *CUF*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kupitia Muswada wenyewe, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake. Pia pongezi za kipekee kwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu, kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuufanya marekebisho Muswada huu na kuupa sura ambayo kwa kiasi chake ni tofauti na ulivyokuwa hapo awali. Kambi ya Upinzani, imefarijika sana na kuleta kwa Muswada huu kwani sasa hivi ni takribani miaka sita toka tuanze kutoa ushauri kwa Serikali juu ya umuhimu wa kuwepo na utaratibu wa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutekeleza majukumu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa Taasisi za Serikali tayari ziliikuwa zimekwishaingia katika mfumo huu wa *PPP* bila ya kuwepo kwa Sera wala Sheria. Kwa bahati mbaya, wabia hao wamekwishailetea Serikali hasara kubwa sana, aidha, wabia hao kutokana na mikataba ilioingiwa, hawataki kufanya marejeo mikataba hiyo. Mfano ni mkataba wa *Songas* na *TPDC* na *TANESCO* kwa upande mwingine *IPTL* na vilevile *KIA*. Tunaitaka Serikali ieleze katika hili, tunaendelea kupoteza? Kambi ya upinzani inapenda kujua, mbali na Mahakama, Serikali itafanya utaratibu gani kuhusiana na suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali iwe makini na kujifunza makosa yaliyotokea nyuma, mfano mzuri ni *Richmond*, Shirika la Reli n.k. Kwa hivyo, Kambi ya Upinzani inashauri kuzitumia vyema ofisi ya Balozi zetu kutupatia ushauri na taarifa kamili za makampuni ambayo tunataka kuingia nayo ubia kwa njia hii ya *PPP*. Ushauri kama huu pia ultolewa katika Maazimio ya Bunge katika sakata la *Richmond*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba sasa kupitia kwenye baadhi ya Vifungu ambavyo tunaona vinatakiwa kutolewa ufanuzi au kuwekwa sawa ili kuondoa dhana nzima ya kudurusu majukumu katika utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ya Muswada inahusu uanzishwaji wa Kitengo cha Utaratibu wa Ubia na Kitengo cha Fedha. Kifungu cha 4(1) kinataja kuanzishwa kwa chombo kinachoratibu ndani ya *TIC*. Lakini kwa Sheria ya hivi sasa, *NDC* ndio inayoingia mikataba na Makampuni ya nje, mfano ni mradi wa Ngaka, lakini Sheria hii haitamki popote wajibu wa *NDC* katika suala hili la *PPP*. Aidha Kifungu cha 4(5) kinasema, nanukuu;

“The Minister shall prescribe by regulations the scope, type and value of projects which the local government authorities may undertake under this Act.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona, kwa kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, ni Serikali zenyenye mamlaka kamili na pia Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (*D by D*), inatakiwa iheshimiwe. Hivyo kutunga kanuni zinazozibana Halmashauri, inakuwa sio sahihi na hili linaondoa dhana nzima ya ugatuaji wa madaraka. Suala la msingi ni kuwa Kitengo cha Uratibu ndicho kinaweza kuangalia mustakabali mzima wa jinsi ubia utakavyofanikishwa katika azma ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 8(2) kinahusu *identification*, naomba ninukuu:-

“The private sector, shall play the role of identifying and implementing public private partnership projects by:

- (a) carrying out feasibility studies;
- (b) mobilizing resources;
- (c) risks sharing;
- (d) monitoring ...”

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Kambi ya Upinzani inaona wajibu wa *identifying* ni wajibu wa Serikali. *PPP* wanaweza waka-carry out feasibility study lakini *identification* ya maeneo na mambo mengine, iwe ni juu ya dhamana ya Serikali, wasiachiwe hao watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 11, kinaeleza kuwa “*Contracting Authority*” itakuwa na wataalam katika nyanja zote husika (*Negotiation Team*) kulingana na kazi watakayoingia nayo ubia na sekta binafsi baada ya makubaliano kufikiwa. Kambi

ya Upinzani inaona kuwa ni vyema kupeleka makubaliano hayo kwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa ushauri na baada ya hapo ndiyo uende Kitengo cha Fedha (*Finance Unit*) ili utekelezaji uendelee. Kwa njia hii, tutapunguza urasimu ambao unaonekana dhahiri kuwepo katika Kitengo cha Uratibu (*Co-ordination Unit*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 14 cha Muswada kinasema kuwa, kila mkataba kabla ya kusainiwa inatakiwa upelekwe kwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa ushauri. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kungekuwepo muda maalum kwa Mwanasheria Mkoo kutoa ushauri kulingana na makubaliano hayo badala ya kutokuelezwu ushauri utolewe kwa muda gani. Ikumbukwe kwamba kabla ya mabadiliko ya Muswada huu zilitolewa siku kumi na nne, muda huo ulionekana mdogo kwa ofisi ya Mwanasheria Mkoo kupitia makubaliano kwa umakini, lakini pia kuiachia Ofisi ya Mwanasheria Mkoo bila kikomo cha muda, ni jambo linaloweza kuleta urasimu usio wa lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 27 kinachohusiana na adhabu, kuwa mtu yeoyote atakayeenda kinyume na mkataba adhabu yake imeelezwa kuwa ni fedha za Kitanzania zisizozidi shilingi million tano au kwenda jela kipindi kisichozidi miaka mitatu. Kambi ya Upinzani inaona kuwa adhabu utolewe kulingana na kosa na thamani ya mradi husika kulingana na thamani ya fedha kwa mradi husika (*exchange rate*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Eng. Mohammed Habib Mnyaa, nakushukuru sana kwa hotuba yako uliyoitao na hasa pongezi maalum kwa wagombea wa Uchaguzi Mkoo, nafasi za juu kabisa za nchi yetu kule Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nitambue uwepo wa Naibu Spika, ambaye karibu wiki nzima hatukuwa naye, Mheshimiwa Anne Makinda. Niwajulishe tu kwamba amesharudi hapa Bungeni na tuko naye.

Sasa kama niliyosema, uchangiaji unaendelea na tunaanza na Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na Mheshimiwa Dokta Anthony Diallo, ajiandae. Mheshimiwa Hamad Rashid.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia Muswada huu. Pili nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuwasilisha vizuri na hasa kwa uchambuzi wa kina alioufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, nataka niende tu moja kwa moja kwenye Muswada na zaidi ninaenda kwenye *Part II* ya Muswada. La kwanza katika hili, ninataka kusema tu kwamba kutokana na uzoefu ambao nimeupata, nimeona kwamba

moja ya tatizo kubwa la Watanzania ni kwamba sisi wenyewe zile rasilimali zetu hatuzijui na mfano mzuri ni mradi wa Ngaka ambapo *NDC* wameingia ubia na kampuni moja kutoka Australia. *NDC* ilikuwa inafikiria kwamba inao mkaa wa mawe wenyewe kiwango cha tani kama milioni 92, lakini kwa sababu wenyewe hawakuwa na fedha za kufanya *feasibility study*, walipokuja wataalamu wale kufanya *study* wakakuta kuna mkaa wenyewe kiwango cha tani milioni 500. Sasa utakuta wameingia ubia kwa 30% kwa kuelewa kwamba kiwango cha rasilimali iliyopo ni tani milioni 92. Ilipofanywa *feasibility study* ambayo ilitumia kama dola 5,000,000 wakagundua kwamba kuna mkaa wenyewe kiwango cha tani milioni 500. Kama rasilimali hii ingekuwa *NDC* wanaijua wao wenyewe mapema, wasingweza kukubali kuingia kwenye ubia kwa asilimia ndogo hiyo waliyoingia. Sasa hili ni tatizo moja la msingi ambalo ningeomba Serikali iliangalie katika suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ambalo vilevile ni la muhimu, ni la taasisi ambazo zimewekwa kufanya kazi hii. *Tanzania Investment Centre*, kazi yake kubwa hasa kwa kweli ni kutafuta wawekezaji na kuwaratibu lakini sina hakika kama kutakuwa na utaalamu wa kutosha pale wa kuweza kufanya hii kazi ya kuchambua miradi. Kwa hiyo, ninapenda kushauri kwamba chombo ambacho kisheria kimekuwa kikitamkwa hapo nyuma ni *NDC*, lakini tunayo *Commission* ya Mipango hivi sasa, nilifikiria kwamba kwanza Serikali inge-*identify* maeneo ambayo miradi ikifanyika basi nchi itabadilika kiuchumi, kwa mfano, mpaka leo Tanzania tunazalisha umeme usiozidi *Megawatt* 1000 wakati mahitaji ni kama 2000 lakini umeme huo huo tungeweza kuzalisha na tukauza nje tukapata fedha. Kwa hiyo, *focus* yetu ya kwanza kama tuna-*encourage private partnership*, ni maeneo gani ambayo yataiondoa nchi katika tatizo la msingi la kuweko na vyanzo vya kutosha vya umeme. *Study* hiyo ingefanywa ili tukawaambia wawekezaji, tunataka uingie hapa ili tuiondoe nchi ilipo, vinginevyo tunaweza tukapata wabia wa kuingia katika miradi ambayo *impact* yake kiuchumi haionekani haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara. Barabara inayotoka Dar-es-Salaam mpaka ikafika Kigoma, ningesema ni *priority number one*. Tungehakikisha kwamba barabara hiyo imepata mwekezaji na ikafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni bandari zetu za Tanzania mfano bandari ya Dar-es-Salaam, Tanga, Pemba na kadhalika. Tungezipa *priority* zile *areas* ambazo tukiwekeza basi *impact* yake kiuchumi itaonekana haraka. Sasa haya yanataka kufanyiwa *feasibility study* za haraka na tuone hasara ya kuwaachia wageni kufanya *feasibility study* wao wenyewe kwa sababu *information* zile ambazo zitawapatia mapato hawatatupatia sisi. Nchi yetu inaweza ikakuta kuna mkataba wa miaka 20 au 30 na watu wanaondoka, hatutapata rasilimali hata kidogo kwenye nchi, hili ni jambo la muhimu sana kuliangalia hivi sasa. Sasa Kifungu hiki kinasema Serikali itafanya upembuzi yakinifu na kadhalika, lakini mara nyingi usoefu umeonesha kwamba Serikali haitengi fedha za kutosha za kufanya kazi hiyo na mfano huo nilioutoa wa Ngaka, ni jambo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni suala la muda. Wawekezaji hawa wangependa sana kujua *time frame*, kwamba mimi ninapopeleka maombi yangu Serikalini, ni lini nitapata majibu ili niweze kufanya kazi zangu? Sasa haya kwa bahati

mbaya katika Sheria imekuwa ni kimya hakuna popote inapoeleza. Ninafikiri kwa wenzetu wengi, kwa mfano nchi kama Ghana, unajua kabisa leo nimepeleka *application* yangu, kesho nitapata majibu, kesho kutwa nitafanya hiki, kuna programu toka siku ya kwanza mpaka siku ya mwisho unaopata *project* yako. Mimi ninafikiri huo ndio utaratibu ambao ungeweza kutusaidia kuondosha urasimu huu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, ni kuzitumia hizi Balozi zetu. Tunaweza tukapata *bogus companies* nyingi hapa Tanzania, kama hatufanyi utafiti wa kutosha kujuu ni kampuni gani inayotaka kuwekeza. Kwa hivyo, jambo la kwanza kampuni inapoleta *application*, ziarifiwe Balozi zetu na zipewe *time frame*, kwa sababu tuna uzoefu wakati mwingine unawenza kupeleka taarifa Ubalozini na yeze akakaanazo tu vilevile hafanyi chochote na wao wapewe *timeframe* ya kuweza kufanya utafiti kujuu hiyo kampuni inayokuja kuwekeza, kweli ina uwezo wa kufanya kazi hiyo na sio kutupotezea muda tu hapa. Maana wanaweza kuja watu wengi wakutupotezea muda tu kwamba mimi nina hiki, nina hiki, kumbe wanapoteza muda tu ni ma-*bogus* hawana lolote. Kwa hiyo, ni vizuri tukawa na uhakika, yule anayekuja kuwekeza basi kweli anazo rasilimali za kuwekeza na ana uzoefu wa kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la kujifunza, pengine sasa hivi tunaanza na ndio maana tumeweka taasisi nyingi za kufanya kazi hii. Mimi ninafikiri Serikali ichukue muda kidogo, itafute nchi ambazo zina uzoefu, kama Mauritius na wengineo, wao ni taasisi gani wameziweka kufanya kazi hii? Vinginevyo huu msururu wa kupeleka Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mwanasheria Mkuu, ni mzunguko mrefu sana kwa mwekezaji ambaye anataka kuingiza *billions and billions of money*, anawenza akaona aah, nyie mnampotezea wakati na akaenda mahali pengine, watu siku hizi, haya mambo yanawahiwa sana. Sasa mimi ninaomba sana vilevile hilo nalo lizingatiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho zaidi ni Kanuni. Uzoefu hapa Bungeni unaonesha tunapitisha Sheria nyingi, lakini Kanuni huwa zinachelewa sana. Tuna bahati mara hii Kanuni hii ya *Election Expenses* imetoka mapema na kwa sababu ya uharaka wenyewe lakini zipo Sheria nyingi sana ambazo zimepitishwa na Bunge hili na bado Kanuni zake hazijawa tayari. Hili nalo ni jambo la muhimu sana. Nina hakika kuna watu wengi sana wanapenda kuwekeza katika nchi, lakini taratibu zetu za kisheria, tunachelewa sana katika utekelezaji wake. Ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri, suala la Kanuni, najua sasa hivi tunaingia kwenye uchaguzi hapa katikati, lakini Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ipo na inafanya kazi, mimi ninafikiri ingeendeleza kufanya kazi ya kutunga Kanuni ili Kanuni hizo ziweze kwenda pamoja na Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DR. ANTHONY M. DIALLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniruhusu na mimi nichangie kwenye Muswada huu. Kwanza, nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kuruhusu Ilemela kuwa na Halmashauri ya Manispaa, tunashukuru sana.

Pia kwa kuanzishwa kwa Mikoa miwili inayotokana na Mkoa wetu wa Mwanza upande mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kuchaguliwa kugombea tena na Makamu wa Rais kwa kuchaguliwa kugombea Zanzibar. Vilevile napenda kumpa pongezi sana Dokta Bilal kwa Mgombea Mwenza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niende moja kwa moja kwenye Muswada. Muswada au tuseme Sheria hii imechelewa sana. Kama walivyotangulia wenzangu, Sheria hii tangu tuliponza *PPP* ilitegemewa kuwa imeshaletwa na ingekuwa inafanya kazi. Lakini hata hivyo nikiingalia kwa ujumla inavyoonesha imekuja kwa haraka sana, ina makosa mengi ukiacha haya mengine yaliyoingizwa kwenye *schedule* ya *amendment*, kuna makosa mengi. Mfano *Part II*, kile Kifungu cha 4(3)(i), mimi ninadhani walikuwa wanamaanisha *trade and marketing* ya *goods* na *services* maana ukiacha *trade and marketing* ina *hang*, inakuwa kidogo inatatanisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 5(a)(ii), mimi ninadhani hii dhana ya mradi wa ku-*provide value for money*, hii ni *terminology* ya *auditing* ambayo sidhani kama imeingzwa sahihi hapa. Mimi nilidhani ni kuangalia mradi kama *economically up feasible*, sio una-*provide value for money*, ile ni *terminology* ambayo haitakiwi kuwa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 5(a)(iii), nadhani *transfer appropriate technical, operational and financial risks*, mimi nilidhani neno dogo tu au fupi la kusema una-*provide*, unaonesha wazi wazi itakavyo-share benefits na risks. Hilo neno sidhani kama linaleta maana yoyote, ni kama kuna *shared benefits* au kuna *shared risks* ambayo mbele kwenye Muswada pia nimeona wamerudia lile, lakini huku haliko, halikuoneshwa wazi wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 5(b) kinasema:-

“Examine the request for proposal to ensure conformity with the approved feasibility study”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mikataba ya biashara mambo ya *approval* na nini, nadhani hapa mnaleta dhana ya Serikali, mnadhani ni *agreed feasibility study*, kwa sababu *you are talking of two partners* ambao wanaingia kwenye mkataba wa kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kama nilivyosema kuna maneno mengi sana yamerudiwarudiwa, sehemu nyingine kama suala moja linarudiwa sehemu tatu na linakuwa kama linaji-*contradict*, mfano suala la *feasibility study* huwaga sana wanaingia watu ubia, nani analipia *feasibility study*, kwa sababu *feasibility study* ina *cost* pesa sio jambo ambalo unaweza kulifanya kirahisi. Kwa hiyo, kwanza *agreement* ambayo ilitakiwa ni ile wata-share vipi utengenezaji wa *feasibility study* na hiyo ingeonyeshwa waziwazi lakini sasa hivi inavyooneshwa *approved authority* itatengeneza *feasibility*

study halafu *contract parts* watengeneza *feasibility study*. Sasa upande wa *private*, mimi nadhani kuna mgongano hapo ambao mnaweza kuutoa ieleweke tu kwamba *feasibility study* itatengenezwa kulingana na mlivyokubaliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu kingine ambacho naona ni marudio au kina utata kidogo, ni Kifungu cha 15(1) na (2). Mimi nadhani hii nani afanye *procurement* inategemea watakavyokubaliana kwenye mradi kwa sababu kuna teknolojia mfano kwenye mambo ya *manufacturing*, kuna teknolojia nyingine ni *preparatory* yule ambaye anaingia ubia huenda ndiyo anayeifahamu sasa ukimwambia kwamba lazima mkataba ufuate *Procurement Act*, sidhani kama itawezekana kwenye ule mkataba wa maelewano itaonyesha jinsi gani *equipment* itakuwa *procured*, lazima kuwepo na hiyo *flexibility* la sivyo kwenye maeneo yenye teknolojia ya hali ya juu, tutakuwa tunapata matatizo au watu watakuwa wanavunja Sheria ambapo itakuwa tabu kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nilikuwa naomba walielezee vizuri kwenye huu Muswada suala la *confidentiality*. Kuna mikataba mingine inahu su teknolojia ambayo ni *sensitive* na wakati mwingine ina thamani kwa yule anayeuleta ule mradi. Sasa kwa utaratibu wetu na urasimu wetu, wanaweza kukuzungusha *in the process* mtu mwingine akapata *access* na hiyo *feasibility*, kwa hiyo, ikawa rahisi sana kukukwepa kwa kutumia maandiko, wakaingia ubia na mtu mwingine. Sasa hili suala ni vizuri likaainishwa vizuri kwamba atakapo-*prove* kwamba mradi wake ambao aliuleta, wakakubaliana, siri imevuja na ikasababisha akose, inatakiwa iwe wazi ili kuweka imani kwa wale ambao watapenda kuingia ubia na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda niunge mkono hoja na nikijua kwamba mwanzo wa hii Sheria kabla haijaingia kwenye utekelezaji kuna maeneo mengi sana kama niliyoeleza yatarekebishwa. Serikali inatakiwa kupewa pongezi kwa hilo, ahsanteni sana. (*Makofî*)

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada huu wa Ubia kati ya Wadau Binafsi na Serikali katika kuwekeza kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukushukuru wewe, nashukuru pia Wenyeviti wengine ambao kwa kipindi chote mmeendelea kutuongoza vizuri, Naibu Spika na Spika katika Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuwapongeza sana wanawake wenzangu wa Mkoa wa Ruvuma, Mbanga, Namtumbo, Tunduru, Songea Vijijini na Songea Mjini, kwa kuendelea kushirikiana na mimi katika kuleta maendeleo yetu binafsi pia maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru na kupongeza Serikali, Muswada huu umekuja pamoja na kwamba kila mmoja ana muono wake, mimi nafikiri umekuja kwa muda muafaka kwa sababu tunahitaji uwekezaji katika nchi yetu, lakini hatuhitaji tu wawekezaji kutoka nje, tunahitaji pia wawekezaji kutoka ndani. Kwa hiyo, ninaimani kwamba wawekezaji pia wa ndani wameshajenga uwezo, kwa hiyo, Muswada huu utakuwa na manufaa kwa wote, wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye kile Kifungu cha 4 chenyeye uratibu wa Muswada huu na kazi ambazo zitafanyika katika ubia kati ya Serikali na wadau binafsi. Ninaomba Serikali itoe mafunzo kwa wataalamu ambao watakuwa katika Kitengo cha Uratibu na ikiwezekana waende wakapate uzoefu katika nchi ambazo zimefanikiwa kutengeneza *PPP*, wajaribu kwenda nchi ya India, Malaysia, China, hao wote wamefanya vizuri sana katika miradi ya *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile waweze kujaribu kuona ni namna gani Serikali itawawezesha wale wawekazaji wazawa wanaotaka kuwa na mifumo ya uwekezaji katika nchi na kuingia ubia na Serikali inakuwaje? Kwa hiyo, kama wataweza kuwasaidia wazawa pia wakaenda kuona maeneo haya basi wafanyabiashara wa Kitanzania pia watanufaika na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu kile cha 4, kuna suala zima la utekelezaji wa mradi wenyewe. Utekelezaji wa Muswada huu utakuwa na manufaa sana kama wazawa watapewa kipaumbele. Katika miradi hii, kuna ujenzi ambao unafanyika katika barabara kubwa, bandari na mambo mbalimbali ambayo kwa kweli yanahitaji mitaji mikubwa na kadhalika. Kwa hiyo, ni vizuri sana wazawa pia wakashiriki lakini vilevile watapewa kipaumbele wataalam wazawa. Sasa hivi tuna ma-*Engineer* wengi tu wanafanya kazi nzuri, tuna wasomi wengi tu wanaweza kufanya kazi nzuri, kwa hiyo, wataalam wazawa pia wapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie Kifungu kile cha 28(2)(c) na (e), kuna suala zima la kuangalia namna gani kutakuwa na *link* kati ya Halmashauri zetu na Wizara ambazo zinatekeleza Muswada huu. Tumejifunza katika miradi mingine kama vile mawasiliano, wawekezaji wanafanya mawasiliano na *TIC* wanapoenda kwenye Halmashauri hawana makubaliano yoyote na Halmashauri zetu na suala hili linaleta migongano mikubwa sana. Kwa hiyo, katika utungaji wa Kanuni, tunaomba kweli Mheshimiwa Waziri azingatie, kutakuwa na mahusiano ya namna gani kati ya Halmashauri na Wizara, kati ya Halmashauri na hawa wawekezaji na inapendeza sana wawekezaji wanapofika kwenye Halmashauri wajaribu kuzitambua na kuzithamini Halmashauri zetu. Sasa hivi Serikali yetu imeshaamua kupeleka madaraka kwa Halmashauri, kwa hiyo na wawekezaji nao wathamini mchango wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile kuna suala zima katika kile kipengele cha (e) cha kuwezesha wananchi, hili ni jambo muhimu sana. Kama wananchi watakuwa

wanawezeshwa kwenye hii miradi maana yake ni kwamba wananchi nao wataifurahia miradi hii na matokeo yake hapatakuwa na ugomvi wala hapatakuwa na suala lolote ambalo litaweza kuzuia utekelezaji mzuri wa miradi hii. Sisi sasa hivi tunajitahidi sana kuwaelimisha wananchi na kuwaambia kwamba wageni watakaokuja ni vizuri wakaelewana na wananchi, katika mpango tuna miradi ambayo tunaitegemea kule Namtumbo ya *uranium*, miradi kama hii ndiyo itasaidia sana. Lakini vilevile tuna masuala ya makaa ya mawe, tuna masuala mazima ya barabara, kwa hiyo, tunategemea kwamba Serikali itatunga kanuni zenyehuakika na kuwawezesha wananchi waweze kufaidika na kunufaika na miradi hii mikubwa ambayo itatumika katika Sheria hii ya Ubia kati ya Serikali na Wabia Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho Mheshimiwa Waziri, nimshauri kwamba Sheria hii inabidi itangazwe sana ikibidi itafsiriwe kwa haraka ili wananchi waweze kunufaika nayo. Kwa hiyo, ni vizuri Sheria hii ikatangazwa ndani ya nchi na nje ya nchi. Kwa sababu tunahitaji wawekezaji, tunahitaji kuwatangazia wawekezaji kwamba sasa hivi Serikali yetu ina Sheria ya Ubia kati ya Serikali na Wawekezaji Binafsi kwa maana hiyo watakuja wawekezaji wengi, lakini tusipoitangaza, haitakuwa na maana yoyote ile. Lakini vilevile tunahitaji kuitangaza sana kwa sisi wenyeWE Watanzania wazawa, hatuhitaji kila kitu kifanywe na watu wageni, wazawa pia tunahitaji kufahamu vizuri lakini pia kushiriki katika utekelezaji wake. Sheria hii ni nzuri, itaweza kuleta wawekezaji wengi, ajira zitaongezeka, uchumi utapanda na maisha bora kwa kila Mtanzania yatawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta Sheria hii kwa wakati amba ni muafaka na sisi tuseme tu Kanuni zikija mapema na Sheria hii ikipita mapema, tutaitangaza sana hasa wakati wa kampeni. Namshukuru Mheshimiwa Waziri lakini vilevile nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono Muswada huu wa Sheria, ahsante. (*Makofit*)

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri na kwa kweli Serikali nzima, kwa kuuleta Muswada huu mbele ya Bunge letu Tukufu ili tuujadili na hatimaye kuupitisha. Ni Muswada mzuri, tunauhitaji na kwa kweli umechelewa, lakini Waswahili walisema chelewa ufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika mambo nitakayoyajadili, nitazungumzia tu masuala ya ujumla na ya hapa na pale. Nianze na mahali pa kuanza kuzungumza na mwekezaji binafsi. Pamoja na kwamba kitu cha kwanza kiwe ni mradi lakini vilevile jambo ambalo tunapaswa sisi kama Serikali, sekta yetu ya umma ambayo itaingia katika mahusiano na sekta binafsi, ni kiwango cha *investment* inayohitajika. Kama mradi unahitaji mathalani dola milioni 100, sasa tunaanzia hapo, hizi dola milioni 100 sisi kama

Serikali tunaweza kuchangia kiasi gani, pale ndipo inapokuja hoja. Kwanza suala la msingi, je, tunazo dola milioni 100 kama Serikali kuziingiza katika mradi huu? Jibu likiwa hatuna, sasa tuangalie sisi kama Serikali tunaweza kuingiza kiasi gani pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalokusudia kusema ni jinsi ambavyo tutagawana hizi hisa zinazokwenda kwenye mradi ambao tunataka kuingia ubia na sekta binafsi, iwe ni ya nje au ya ndani. Pale ndipo tunapopata uwiano sasa wa kile tunachokiita *controlling shares*, ni nani baina ya hawa wawili katika kuingia huu ubia atakuwa na hisa za ku-control ile kampuni na hapa ni vizuri Sheria ika-address suala hilo, kwamba hawezi kuja mwekezaji ambaye ana hisa zaidi ya 51, 60, 70 halafu sisi kama Serikali tukaja tena tukasema tunataka tuwe na *controlling power* kwenye kampuni hii, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii Sheria lazima ifike mahali iseme *proportion za joint venture* hizi zikishakuwa kwenye *share* za namna fulani, *ownership* ikiwa kuanzia 51% and above kwenda kwa mtu mwingine au iwe mwekezaji wa ndani au wa nje, yule mwenye *shares* nyingi ndiyo anakuwa na *controlling power* za hiyo kampuni. Sheria hii iseme na ikishasema hivyo sasa Sheria nyingine ambazo inabidi ziendane na marekebisho ambayo ni lazima ni pamoja na Sheria za Ukaguzi wa Nje wa Kampuni inayoundwa, Sheria ya Manunuzi ya Umma na vilevile Sheria zetu za Kazi. Jamani bado baadhi ya sisi wafanyakazi, tunadhani kwamba tunapokuwa wafanyakazi tuna haki zaidi kuliko Mwajiri na kwa maana hiyo tunaweza tukajikuta tunakaribisha wawekezaji hapa, halafu tatizo kubwa linatoka kwa wafanyakazi wanaosema wao ni Watanzania na kampuni hii iko Tanzania lakini tunasahau kwamba ni kampuni iliyoko Tanzania, tumekaribisha mwekezaji, awe wa ndani au wa nje. Kwa hiyo, tujenge utaratibu wa sisi wafanyakazi kuheshimu kwamba tumeajiriwa, mwajiri anahaki zake na wafanyakazi tuna haki zetu na hata kama kuna matatizo baina ya Waajiriwa na Mwajiri zitumike taratibu za kazi kumpa haki yake kila anayestahili. Mwajiri apate haki yake na Mwajiriwa apate haki yake kwa mujibu wa mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, kuna hili suala la kuunda Kitengo hiki kinaitwa *unit* itakayoshughulikia mambo haya, ambacho kitakuwa kwenye Wizara ya Fedha. Mimi nashauri kwamba *unit* hii ingefanywa iwe *unit autonomous* kwa maana halisi ya *autonomy* kwa mfano kama vile ilivyo Benki Kuu *is an autonomous institution* ndani ya Wizara ya Fedha, ina mamlaka yake kamili, inafanya kazi zake *responsible to the Minister for Finance. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiki Kitengo cha kushughulikia mambo ya uwekezaji, ukishakiweka ndani ya Wizara ya Fedha halafu ukakiweka chini ya mfumo wa *bureaucracy* ya Wizara ya Fedha, hatuendi. Hakutokuwa na *efficiency* kwa sababu hiki ni kitengo cha kufanya mambo ya biashara. Huku Wizarani ni mambo ya kirasimu wa Kiserikali, hatuwezi kwenda, tengeni kitengo hiki, kiwekeni nje, kipeni mamlaka, kifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala limezungumzwa hapa kwamba tunapozungumzia wawekezaji tuiswatazame wa nje, tuwatazame na wa ndani, ni kweli lakini njia ya kuwapata wawekezaji wa ndani ni katika hii mikataba ya *joint venture* tutakapokuwa tunaingia, tuweke nafasi mahsus i nayoonesha dhahiri kabisa kwamba wakati fulani kampuni hii tunayounda, tutaipeleka kwenye *stock exchange* na ukai-list pale ndani ya nchi yako au hata nje ya nchi yako, ndipo unapoipa ile kampuni nafasi ya kuwa *owned* na watu wengine zaidi na ikiwezekana kama ni Watanzania twende kule *stock exchange* tukanunue *shares* kwenye hii kampuni ambayo tunaipenda sana. Hiyo ndiyo njia peke na rahisi ya kuwafanya Watanzania waweze kushiriki katika *ownership* ya hizi kampuni na sio kupiga kelele tu tupendelee wananchi, tutawapendeleaje? Tuipeleke kwenye *stock exchange*, kule ni sokoni, wewe una hela za kununua *shares*, nenda sokoni, kama kampuni iko *listed* utanunua na utakuwa *owner*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niendelee kusema kwamba kuna maeneo mengi katika Sheria hii yanasema yule *partner* wa nje au wa ndani atafanya *feasibility study*, *contracting authority* itafanya *feasibility study*, sijui nani mwingine atafanya *feasibility study*, *feasibility study* hizi ni ngapi na ndiyo maana mpaka leo hii bado tunafanya *Environment Impact Assessment* ya mradi wa Soda Ash, kule lake Natron. *Environmental Impact Assessment* ya mradi muhimu sana kwa uchumi wa nchi hii? Nchi hii ina *import Soda Ash* kutoka Kenya na mahali pengine. Tunayo *Soda Ash* wenye kama Tanzania ambayo tukiichimba na tukiitumia *tuta-save foreign exchange*, tukiiza nje tutapata *foreign exchange* lakini hatuitumii bado tunafanya *Environmental Impact Assessment* mpaka lini? Sasa haya ndiyo matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo humu ndani ya Sheria linasema ili mkataba utiwe saini lazima *legal opinion* ipatikane kutoka *Attorney General (AG Chambers)*. Nasema sawa lakini kuna uzoefu umeonyesha hizi *legal opinion* kutoka kwa *Attorney General* pamoja na heshima zote, *Attorney General* uko hapa, kule ofisi kwako kaka unahitaji kuongeza *efficiency*, *legal opinion* zinachukua muda kutoka, *by the time* inatoka muda umepita. Kwa hiyo, ni sawa kupata *legal opinion* lakini suala la *speed liangaliwe*. Hivyo hivyo tuzingatie kwamba hawa wanaokuja kuwekeza tukitaka sisi kupata *legal opinion* yetu tuju na wao wana *legal opinion* ya *Lawyers* wao, kwa vyovyyote wao hawawezi kuingia kwenye mkataba bila kupata *legal opinion* lakini hii ya kwetu nayo tuipate, isipokuwa *speed* lazima iwe kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nazungumzia juu ya *ownership* na *proportion* zile katika haya tunayozungumza hapa, katika taratibu za uwekezaji na *joint venture*, kuna eneo ambalo linajulikana kama *technical* na *management agreement*. Kwa maana unaweza kuingia mkataba wa kuendesha kampuni yako na kampuni ya nje, kwa utaratibu tu wale wanakuletea wataalamu pamoja na *management*, sasa hili nalo kwa sababu tunazungumzia *Private Public Partnership* basi nalo tungeliweka wazi katika huu

Muswada, eneo la kupata utaalamu wa utawala na uendeshaji. Tunalichukuliaje na tutalifanyaje kwa sababu litakuwa linaleta *expertise* pamoja na utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ukaguzi wa kampuni, kwa mfano uzoefu umeonesha tulipokuwa na *TRL* wakati *RITES* ilipokuwepo na huu ndiyo uzoefu, tuuchukue, tuutumie kwa mambo yaliyokuwa yanajitokeza. Zilikuwa zinakuja hoja kwamba 49% ni hisa ya Serikali na 51% ni hisa za makampuni ya nje, kwa nini *CAG* asiende kuikagua kampuni hii? Kulikuwa na hoja hiyo na ilikuwa inatolewa kwa nguvu zote. Lakini hii ni kampuni ambayo ile *ownership* yake iko kwenye *private sector*, sasa ili tusipate matatizo, tutoe uamuzi hapa Bungeni wakati tunazungumzia hii Sheria kwamba ni wakati gani *CAG* ataruhusiwa kukagua kampuni ambayo Serikali ina hisa? Je, hizo hisa ziwe za kiasi gani ili *CAG* akague na zisipofikia hapo hatuna haja ya kubishana, ni Sheria tu iwe wazi na dhahiri kabisa, itatuondolea matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo kwa upande wa *Public Procurement Act* itamgusa nani? Maana kama kuwepo kwa Serikali, Serikali ina hisa 5% halafu unasema fuateni *Public Procurement Act*, haiwezekani! Wale wengine wana hisa 95% na wao wana *interest* ya ku-safeguard kampuni yao, watakuwa na taratibu zao za manunuzi ambayo pengine ni *more stringent* kuliko hizi za *Public Procurement Act*. Kwa hiyo, hiyo ni lazima Sheria hii i-address issue hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, wananchi wote kwa ujumla wetu, ni lazima tukubali kwamba kuna kiwango Serikali inaweza kafanya mambo na kuna kiwango Serikali haiwezi kufanya mambo yote ndiyo maana ni lazima *Private Sector* ya nje au ya ndani ya nchi au zote zishirikiane na Serikali. Kwa hiyo, wananchi tusitazame utaratibu huu katika hali ya hasi lakini tuutazame utaratibu huu katika hali ya chanya kwa sababu ni utaratibu mzuri unaisiaidia Serikali kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema mathalani leo hii tunazungumzia juu ya *congestion* ya Jiji la Dar es Salaam, tunahitaji *fly overs* Dar es Salaam, hizi *fly overs* zinaweza kujengwa kwa urahisi tu na *private sector* ili mradi kuwe na mfumo unaoruhusu hawa *private sector* kukutoza tozo, wewe ukitaka kukaa foleni pita barabara za chini lakini kama unataka kukwepa foleni panda juu ya *fly overs* unazunguka unakwenda, lakini ni lazima ulipe tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya ni mambo ambayo ni lazima tuyaelewe na mwisho wa siku jamani tuheshimu hii mikataba, ukishakosea wakati wa kusaini mkataba ndiyo ulishakuwepo huo huwezi tena kumu-*embarrass* yule *investor* kwamba ooh, huu ulikuwa mkataba mbaya tuuvunje na bahati mbaya wafanyakazi wengine ndiyo wanakwenda huko kusema kwamba tuuvunje, tunamtoa huyu kiongozi. Tusifanye hivyo kwa sababu tunajenga uhusiano unaoweka kivuli cha nchi yetu katika ramani ya ulimwengu, ulimwengu unatutazama, kwa hiyo, tunapofanya mambo tufanye kiulimwengu ili ulimwengu utuheshimu na uheshimu kwamba unapoambiwa kwamba nenda Tanzania kawekeze, wenzetu wanafuata Sheria, wale ni waungwana hata mkishindwana mtakaa mezani kumaliza tofauti zenu. Ndiyo maana ya Muswada huu,

tunaweka mambo yote kisheria tukishindana, tushindane kisheria, tuachane kwa amani na siyo kwa ugomvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, naomba nitoe matangazo mawili madogo, kwanza, Mheshimiwa wa Kambi ya Upinzani Bungeni anawaomba Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwamba wakutane leo saa 10.00 jioni katika ukumbi wa Chifu Kasusura, namba 219.

Lakini pili nilisema Mheshimiwa Naibu Spika amekuwa hayupo wiki nzima na tunamkaribisha tena, sina hakika kama Wabunge wote mnafahamu kwa nini hakuwepo lakini ni kwa sababu alipata msiba wa kaka yake aitwaye James Makinda. Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote tunakupa pole sana kwa msiba huu ambao ulikupata. Mwenyezi Mungu alitoa, ametwaa, Amin.

Baada ya Mheshimiwa Vita R. Kawawa, tutahamia Kambi ya Upinzani ambapo Mheshimiwa Said Amour Arfi atatangulia na atafuatiwa na Mheshimiwa John M. Cheyo na Mheshimiwa Zitto Kabwe ajiandae.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Muswada wa Sheria ya Ubia kati ya Serikali na Kampuni Binafsi yaani *PPP Bills, 2010*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ilivyo ada na mimi naomba nichukue fursa hii, kuwashukuru wananchi wa Wilaya ya Namtumbo, kwa kunipa fursa ya kuwa Mbunge wao kuwawakilisha katika Bunge na vikao mbalimbali. Kwa kuwa kipindi hiki sasa kimekwisha, naomba nitumie fursa hii pia kutangaza rasmi kwamba nitachukua fomu kuomba tena uwakilishi wao Bungeni ili kuendeleza uongozi shirikishi wa mawazo yao, naamini kwa pamoja tutasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naiunga mkono hoja hii, Muswada huu umekuja wakati muafaka, kusema kweli ili ku-*unlock Tanzania potentials* kulihitajika kuwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kuwe na *Private Aspirations* na *Government Aspirations* ambazo zinahitaji kuwa katika uwanja mmoja yaani *level of playing field*. Lakini *PPP needs to have a win frame work* na hivyo Muswada huu ukiwa Sheria naamini kabisa tutafikia lengo hilo kama ambavyo wenzangu wamechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema Muswada huu umefika wakati muafaka? Mwezi Aprili pia tulipitisha hapa Sheria mpya ya Madini ambayo ina kipengele cha *Free Carried Interest*, kipengele ambacho kinataka Serikali kuingia ubia na miradi ile mikubwa ya madini. Lakini nchi yetu ni maskini, hatuna uwezo wa ku-invest katika *explorations* za madini, lakini tukiweka mikakati ya kuwezesha kwa mfano *STAMICO* kuwa na uwezo wa kufanya wenyewe *prospective* na kujua madini

yaliyokuwepo yaani tuliyonayo katika ardhi yetu halafu wakati tunapotaka kuingia ubia na makampuni ya nje, tunajua kabisa ni kitu gani tulichonacho chenye thamani ya kiasi gani, hivyo tunapoingia ubia na makampuni haya basi tuwe tuna uwezo kama alivyosema Mzee wangu pale katika zile *proportional* za *ownership* tunaweza tuka-*negotiate* vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tuna maeneo mengi ya madini na kuna *prospective* nyingi zinaendelea lakini tunataka kuja kuingia ubia na maeneo hayo yako *very remote*, wawekezaji watahitaji kuweka *investment* ya mradi lakini pia wawekezaji watahitaji kuweka *infrastructure* katika mradi husika. Sasa tutakapokaa mezani tusigemee moja kwa moja kwamba na sisi tunaweza kuwa na *share* kubwa katika miradi hiyo. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba lazima tupange mikakati ya *ku-budget* ili kuziwesha taasisi zetu ambazo zitakwenda katika maeneo mbalimbali tulijojaaliwa na Mwenyezi Mungu tuweze kuwekeza, kufanya *prospecting*, kujua tulichonacho na thamani yake na kama kuna makampuni yanataka kuja kuwekeza tuna *negotiate* pale kwenye uwanja ambao tutakuwa tuko sawa kwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kushawishi mukutano mkubwa wa kiuchumi duniani kuja kufanyika Tanzania. Kwa miaka 20, *World Economic Forum* imekuwa ikifanyika South Africa lakini kwa mara ya kwanza imefanyika nje ya South Africa yaani Tanzania. Lazima tukubali Rais wetu aliiona *opportunity* hiyo na alishawishi kwa kuhakikisha mukutano ule unakuja kufanyika Tanzania. Hiyo ilikuwa ni fursa nzuri ambayo imeonyesha mahusiano mazuri duniani kati ya Serikali na makampuni binafsi yaani *Private Public Partnership* kwani mukutano ule ulijumuisha viongozi mbalimbali wa Serikali, *Organisations* na Makampuni mbalimbali duniani na ultipa faida sana japo kuna baadhi ya Watanzania waliubeza. Lakini kwa kweli mukutano ule umefungua ukurasa mwengine wa kuongeza fursa za uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu za haraka haraka kwa siku zile nne za mukutano ule kwa Wajumbe wale 1000 walitumia mamilioni ya dola kwenye hoteli, chakula, usafiri, magari na ndege za kukodisha ambazo fedha hizo zilibaki hapa nchini na kuongeza pato la fedha za kigeni hapa nchini. Lakini pia wageni wale waliporudi makwao wamekuwa Mabalozi wetu. Ninachajaribu kusema hapa ni kwamba kuna faida kubwa sana ya ubia wa Serikali na makampuni binafsi kwa kuongeza uchumi wa kibashara na shughuli za kijamii na mapato kwa Serikali na watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, sina budi kuiunga mkono hoja hii, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Vita R. Kawawa na sasa naomba nimwite Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa John M. Cheyo ajiandae.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye kwa fadhila zake ameniwezesha mpaka leo kuweza kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Mpanda Kati kama mwakilishi wao na niwashukuru pia kwa ushirikiano mkubwa ambao wamenipa katika kuzifanya kazi zangu. Lakini pia niungane nawe kumpa pole Mheshimiwa Naibu Spika kwa kifo cha kaka yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya ubia kati ya Serikali na watu binafsi, ni dhana nzuri ambayo inaweza ikasaidia sana katika kuleta maendeleo na mabadiliko makubwa sana katika yale ambayo Serikali kama Serikali imeshindwa kuyatekeleza kutokana na uwezo wa Serikali yetu jinsi ulivyo. Sina matatizo na dhana hii, ni dhana nzuri ambayo imeleta mabadiliko makubwa sana katika maeneo mengi duniani na tunapaswa tuige mfano, lakini nina mashaka makubwa sana katika maeneo kadhaa ambayo nitahitaji nipate ufanuzi ili niweze kujiridhisha kama dhamira ya kuwa na Sheria hii ni njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo nalionna ni katika eneo la kilimo, eneo hili linanipa mashaka makubwa sana kwa sababu Serikali haishughuliki na kilimo yaani hailimi, Serikali ni mdhamini tu wa ardhi ya Watanzania wote. Sasa itaingiaje ubia katika eneo hili la kilimo? Hili linanipa mashaka makubwa sana na inawezekana Sheria hii ambayo tutaipitisha hapa ikawa ndiyo filimbi inapulizwa sasa ya kuuza ardhi yetu kiholela. Nina mashaka makubwa juu ya suala hilo. Jana usiku ujumbe amba umeongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda umeondoka kwenda Marekani kwa ajili ya kunadi ardhi yetu, jambo hili hatukubali na kinachongojewa ni kuitishwa kwa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni lazima lakini tuangalie sasa ni namna gani tunawasaki Watanzania wenye. Japan ambayo inatuletea Mcchele karibu kila mwaka, hakuna Mzungu anayelima Japan, wanalima wenye Wajapan, wanazalisha ziada mpaka wanatoa misaada katika nchi kadhaa za Afrika. India ambayo ni nchi kubwa kuliko Tanzania, inajitosheleza kwa chakula kwa kuwatumia watu wake, lakini sisi hatuna mikakati yoyote ya makusudi ya kuweza kujitosheleza kwa chakula kwa kuwatumia Watanzania wenye ambao watazalisha chakula cha kutosha. Sasa tunafikiria kumleta Mmarekani aje alime Mpanda wakati tunayo ardhi na watu wapo lakini kwa sababu hatuna mipango madhubuti mpaka sasa nchi yetu inaendelea kuwa tegemezi na ombaomba na tunashindwa kujitosheleza kwenye chakula na wala suala la kuwaleta wageni halitusaidii kama nchi. Wawekezaji hawa watakuja watalima, watazalisha ziada na kitakachopatikana na faida watakayoipata wataipeleka kwao. Ni lazima sasa Serikali iangarie inawasaki Watanzania. Hofu niliyokuwa nayo kubwa sana ni kwamba natarajia Sheria hii tunaipitisha lakini sheria hii baadaye itatuletea matatizo makubwa sana kama hatukuwa makini katika suala la ardhi pamoja na kwamba wamesema huko mbele kwamba Sheria zilizopo zitazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia upo mpango wa kuziletea Sheria mbalimbali zifanyiwe marekebisho, kwa hiyo marekebisho yatafanywa kutokana na matakwa ya wakubwa kwa sababu hata hili linasukumwa na *World Bank*, wala tusijidanganye siyo dhana ambayo tumeifikiria sisi Watanzania kwa maslahi ya Tanzania, ni dhana ambazo zimetumbukizwa ndani ya vichwa vyetu na Wazungu kwa jinsi wanavyotaka wao. Hii haiwezi kutusaidia hata kidogo, ni lazima tuwe waangalifu sana hasa katika maeneo ambayo yatatuletea migogoro sisi wenye kwa wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi inayokusudiwa kuuzwa Mpanda, ni zaidi ya *square kilometre* 4,000 kwa maana ya makazi ya Katumba na Mishamo. Lakini Watanzania ambao hawana ardhi ambao tayari wameshapeleka maombi yao kwenye Serikali kwamba ardhi hiyo ambayo ilikuwa ni makazi ya Wakimbizi wapewe wao, Serikali haitaki kuwapa Watanzania inakwenda kumtafuta Mmarekani kuja kumpa ardhi ya Watanzania na kwamba wageni na wawekezaji wana nafasi kubwa katika nchi hii kuliko wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kunapokuwa na mgongano kati ya mwekezaji na mwananchi, mwananchi ana haki ya kwanza na si vinginevyo na kama mtaendelea kuwakumbatia wawekezaji na wananchi mkawapuuza mnaanzisha chanzo cha kuleta mifarakano na migogoro katika nchi yetu. Hao wawekezaji mtakaokuja kuwapa ardhi kule kwa ajili ya kilimo wakati wafugaji hawana ardhi, kutakuwa na misuguano kati ya wafugaji na hao wawekezaji. Wafugaji ambao wamekuwa ni tatizo kubwa katika nchi yetu lakini ni Watanzania hatuna mahali pa kuwapeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapendekezo yao, wafugaji wameomba yaliyokuwa makazi ya Katumba na Mishamo wapewe wafugaji lakini leo ardhi hiyo wanapewa wawekezaji na kibaya zaidi hata hao wanaokwenda Marekani ambao jana usiku wameondoka Dar es Salaam gharama zao zinalipwa na hao hao Wamarekani, kuna nini? Eti wanakwenda kuthibitisha kwamba ile ni kampuni ambayo si ya kitapeli, basi, ndiyo kinachowapeleka kule. Lakini Baraza la Madiwani limevunjwa, wanaondoka, *delegation* inapewa kibali wanakwenda Marekani, kuna nini? Kwa hiyo, mimi mashaka yangu makubwa ni katika eneo hilo la ardhi kwa maana ya kilimo, labda nipate maelezo ya kutosheleza ndipo nitakapounga mkono Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo pia nina mashaka nalo ni utalii, tunafanyaje? Serikali imepewa dhamana tu ya kusimamia hii raslimali ya Watanzania, sio mali ya Serikali, wao ni walinzi tu. Sasa mnapotaka kuleta wawekezaji kufanya ubia, mnafanya ubia kwa kitu gani ambacho siyo cha Serikali?

Ni kwamba mnakuja sasa kuwapa mbuga zetu, au watakuja kujenga mahoteli katika mbuga zetu au ni kitu gani ambacho mnakusudia katika eneo hili la maliasili kwa maana ya utalii? Haya maeneo mawili nahitaji nipate maelezo ya ziada ya kuniridhisha mimi na Watanzania hasa eneo la ardhi. Ardhi ni tatizo kubwa! Naomba Mheshimiwa Waziri anileze kuhusiana na huo ubia ambao wanataka kuingia katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine sina matatizo nayo ni kwamba, kweli tunahitaji kuwepo na ubia, kuwepo na maelewano lakini pia ambayo yataziangatia maslahi ya nchi yetu. Tuna uzoefu wa kutosha sana wa kuingia katika mikataba mibovu na sasa tunapaswa tubadilike. Wale tunaowapa dhamana ya kuingia mikataba kwa niaba ya wananchi wa Tanzania watangulize maslahi ya Watanzania kwanza, na sio maslahi yao. Vinginevyo tutabakia kuwa walalamikaji kila baada ya mkataba kuwa umeshasainiwa. Sasa ni nani anayesimamia maslahi hayo ya Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini na nina matumaini makubwa sana katika mabadiliko makubwa yaliyotokea katika kipindi cha karibuni, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali itatimiza wajibu wake katika kusimamia na kulinda maslahi ya Watanzania. Yale yote ambayo tumekuwa tukilalamika huko nyuma, yalisababishwa pia na kutokuwepo na umakini katika Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kwa sababu mikataba yote ambayo tunailalamikia leo ilipitia katika ofisi yake. Sasa nina matumaini makubwa sana kwamba, hao watakaopewa dhamana hiyo watatanguliza maslahi ya Taifa letu kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho, ni muda tu, kwamba mikataba yote hii ni lazima ipate maoni ya kisheria kutoka *AG Chambers*, lakini hawakuwekewa muda. Je, itachukua muda gani au kwa kadri atakavyoona Mwanasheria Mkoo? Kutoa maoni, atatoa, vinginevyo mikataba hiyo itakaa kwa muda mrefu sana na suala la utekelezaji wake litachelewa na hiyo tija ambayo inatarajiwa kupatikana kutokana na kuwepo kwa Sheria hii itakosekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana na niwaambie tu wananchi wa Jimbo la Mpanda Kati kwamba, ninarudia kusema tena sitawaangusha, siwasaliti na nitakuwa tayari kuwatumikia kama watakuwa wameridhishwa na utumishi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Arfi ingawaje hujasema kama tarehe 19, Julai itakuwaje.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu ambaeo uko mbele yetu. Awali ya yote nataka kuwapongeza sana wana CCM kwa kufanya Mkutano mzuri na kumchagua Rais Jakaya Kikwete kuweza kuendelea kugombea katika kinyang'anyiro hiki cha Urais. Pia nawapongeza Mheshimiwa Dr. Bilal na Dr. Shein kwa nyadhifa ambazo wamepata.

Lakini pia nitumie nafasi hii kuwapongeza wale wanaojaribu kutokea Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Prof. Lipumba atakuwa anajaribu kwa mara ya nne sasa, na pia Mheshimiwa Hamad. Tusiwabeze hawa watu, hawa ndio majasiri wa kuweza kujua kwamba pamoja na matatizo ya uchanga wa demokrasia yetu, na yale ya kikatiba katika nchi yetu, lakini bado wanataka kuonesha kwamba wataweka ushindani madhubuti ili wananchi wapate kuchagua huyu au yule. Mimi ninaona hawa watu wanahitaji kupongezwa sana kwa ujasiri wao na Mungu awasadie wafike pale ambapo wanataka kufika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninataka kuchukua nafasi hii kweli kuomba uchaguzi huu uwe wa amani. Hili ni jambo la maana sana katika sehemu hii ya Afrika. Tanzania inaweza kujivunia kwamba angalau tumeweza kuonesha kwamba tunawenza

kuwa na mfumo wa vyama vingi lakini tukaendelea kuwa marafiki. Mimi sina adui katika Chama cha Mapinduzi.

Ninatumaini na wao mimi sio adui yao. Kwa hiyo, tuhakikishe tunafanya uchaguzi ambao tutashindana kwa hoja badala ya matusi, mapanga na vitu vingine visivyoofaa. Mimi nina hakika inawezekana kabisa na wale ambao wanajiandaa kutumia nguvu ya fedha, basi Sheria ichukue mkondo wake na mara moja turudi katika hali ambayo tunaweza kupata kuchaguliwa kwa njia ya hoja na siyo fujo na fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hii ni mara ya mwisho, ninataka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge wanaonisikiliza kwamba, mimi nikiwa katika Bunge hili nimekuwa na wakati mzuri sana, na nimejifunza mengi sana kutoka kwao. Nawashukuru sana kwa ushirikiano wao kwanza, kwa kuendesha *Public Accounts Committee (PAC)*. Siyo kazi rahisi, hasa pale ambapo una wajumbe wawili tu wa Kambi ya Upinzani na wengine ni wa Chama cha Mapinduzi. Hata hivyo, kila tunapoleta mambo yetu hapa, tumeweza kuonesha kwamba fedha ya Serikali haina Chama, ni fedha yetu sisi wote na matumizi yake ni lazima yaende vizuri. Ninawashukuru sana kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano pia ndio umenipeleka katika Bunge la Afrika (*PAP*) na kule shahidi yangu ni Mheshimiwa Mongella, tumefanya kazi nzuri na ni matumaini yangu kuwa tutakaporudi tena mtanipa nafasi hiyo ya kuweza kuendelea kupeperusha bendera ya Tanzania kule katika Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, katika utangulizi lakini sio kwa umuhimu, ninataka kumshukuru sana mke wangu Elizabeth kwa kunivumilia na kuilinda familia yetu ninapokuwa na shughuli za wananchi. Kwa watu wa Bariadi ninataka kuwahakikisha kwamba mimi nipo na ninamshukuru Mungu bado ananipa afya njema. Tumefanya mambo mazuri na tutaendelea. Wanaopiga kelele kwamba Mheshimiwa Cheyo harudi, ninawaambia kwamba sasa ninarudi kwa nguvu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme kwamba dhana ya kushirikiana kati ya Serikali na watu binafsi ili kuleta maendeleo ni ya maana sana na sio mpya ingawa tumekuwa tunaifanya bila ya kuwa na sheria na mwongozo ambao ungeweza kutusaidia. Sasa ni matumaini yangu kwamba, kwa kuwa sheria hii imekuja sasa itumike vizuri ili kuhakikisha kwamba, tunapoingia mikataba hii tunahakikisha ni mikataba ambayo haiingizi Serikali katika matatizo makubwa zaidi. Ninasema hili kwa sababu nchi hii tumekuwa rahisi sana kuingia katika mikataba na watu binafsi, lakini kujitoa katika mikatakaba hiyo imekuwa ikiigharimu sana Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tumeingia Mkata pale *Kilimanjaro Airport* ambapo Serikali ilikuwa inalipwa dola 1000 kwa mwaka. Sasa tukitaka kutoka inatubidi tulipe dola milioni 56. Kwa hiyo, hali hii inatufilisi kama nchi. Tumeingia katika Mkataba na *RITES* katika reli, tunataka kutoka tutatoka kwa mabilioni ya fedha. Ninaweza kuendelea kutaja mikataba mibovu ambayo ni pamoja na mikataba ya madini, gesi na yenewe tuko katika matatizo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi wito wangu wa kwanza kabla hata ya kuangalia hapa kwamba sheria inazungumzia juu ya *coordinating unit*, *I think tungeweka umuhimu zaidi juu ya negotiating unit. Negotiation* juu ya kuweza kujadili mikataba, mimi naona kwamba ndiyo umekuwa udhaifu mkubwa sana wa Serikali yetu.

Sijui kule kwa wale ambao wanapewa nafasi ya kuangalia hii mikataba, na sisemi hili mbele ya ndugu yangu AG, lakini ni vizuri akajua kwamba kama ni Idara au Wizara yake ndiyo inawasaidia hao kufanya *negotiation*, basi hapo ni sehemu ambapo tunahitaji kuweka umuhimu wa kufundisha watu wetu, kuchagua watu wasiokuwa na tamaa kwa sababu ukiangalia baadhi ya mikataba ambayo tumeingia unaona imekuwa ni ulafi zaidi kwa wale watu ambao waliingia ile mikataba, na kutokuwa na uzalendo na kuona kwamba hiki sio kitu changu na hivyo wanatoa vitu kwa wawekezaji na kubakiza ziro au kidogo sana kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningependa tuweke umuhimu mkubwa sana katika kuhakikisha kwamba Sheria hii ina *unit* au sehemu yenyewe wataalam wenye uzalendo ambao kweli wanajua namna ya kuweza kuzungumza juu ya mikataba hii. Nchi hii tumekuwa na dhana ambazo ni potofu kwa muda mrefu. Kwa mfano, katika upande wa madini watu wanafikiria kwamba wewe ukiwa na madini kama nchi, huna thamani.

Lakini tunampa mtu leseni ya kwenda kututhibitishia kama kweli tuna dhahabu na ni kiasi gani. Siyo kwamba, kama nchi hatujui kama tuna dhahabu, tunajua tuna dhahabu lakini hatujui ni kiasi gani na kama kinaweza kikatengeneza pesa na vitu kama hivyo. Lakini mtu yule akiishapata ile dhahabu na kuthibitisha pale Serikali inasema hii ni *proven potential* siyo mali.

Mimi ninaona hii ni dhana potofu kabisa kwa sababu ukiishapata *proven potential*, wewe unacheki. Tunajua kwa mfano sehemu ya Bulyanhulu wale waliothibitisha kwamba kuna dhahabu walikwenda kuuza hiyo *right* yao kwa dola za Marekani milioni 348 na Serikali haikupata chochote na bado walipokaa kwenye meza karibu kila kitu kinakwenda kwenye kampuni tu. Ndiyo maana sisi ambao tumekuwa tunasema Serikali ipate *shares* zaidi kwa madini, gesi, sasa tuna *uranium*, mafuta kwa sababu vile ni vyetu tumepewa na Mwenyezi Mungu anayekuja kuvigundua haimfanyi viwe vyake, bado ni vyetu.

Kwa hiyo, tunapaswa kuwa kwenye meza moja, halafu tusiogope kwa kusema hatuna fedha, fedha zipo. Ukishatambua kwamba hapa kuna dhahabu, wanavyofanya Wazungu wanakwenda tu pale Toronto wanakusanya pesa kwa kuweka dhamana dhahabu yetu iliyo ardhini. Ndiyo maana ukiangalia hata mahesabu ya kampuni hizi unakuta uhusiano kati ya fedha wanayowekeza wao na ile wanayokopa kutohakana na dhamana ya mali ya Tanzania iko kwenye asilimia laki tatu na ushee, ndiyo *equity ratio*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kama hii inaonesha wazi kwamba hatujapata ujanja wa namna ya kutumia raslimali zetu kuweza kutafuta mitaji. Wale ambao tunakubaliana nao kama *partners* tunawapa mtaji wa bure halafu unakwenda kukopa nje. Kwa hiyo, mimi ninafikiri tunahitaji kujifunza zaidi katika dhana hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia lingine ni kwamba, nimefurahishwa na Serikali kwamba imetoa ile *automatizity*. Ile sheria ya kwanza ilikuwa inasema Waziri asipokubali katika muda wa siku hizi, basi itakuwa imekubalika kwamba atakuwa ameshakubali. Mimi ninaona hii ni mbaya na tungejifunza pia kwa mikataba ya madini.

Kulikuwa na *clause* katika baadhi ya mikataba ya madini inasema Gavana asipokubali kufungua akaunti ya nje ya kampuni katika muda wa siku 10, kampuni itaendelea kufungua akaunti hizo, na tumepoteza fedha nyingi. Mimi ninashauri kwa sababu hili ni jambo ambalo ni jipy, tusiwe na uharaka, twende polepole hata *pilot project* ifanyike kidogo tuone inafanya nini kwenye sekta hii ili tujifunze. Ninafikiri baadaye hapatakuwa na sababu ya kwanini sheria hii isimamiwe na Ofisi ya Waziri Mkuu, sheria hii inapaswa moja kwa kusimamiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nimeona mchango wa *TIC* ni mdogo sana, tuna-create unit huku, tuna unit nyingine ambayo inaendelea. Sioni ni kwanini hii coordinating unit isiwe karibu zaidi na *Tanzania Investment Centre* kuliko kuonekana kana kwamba ni ka-unit ambako kako tofauti. *Tanzania Investment Centre* ina uzoefu, wameshaangalia feasibility studies nyingi na mambo mengine. Kwa hiyo, kuangalia vitu vidogo vidogo halafu unashindwa kuvihusisha hatutapata faida. Ni vyema tuanze kwa sababu kuna faida nyingi za uhusiano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. (*Makofî*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia Muswada huu wa *Public Private Partnership (PPP)* ambao una lengo la kuhakikisha sekta binafsi inashirikiana na Sekta ya Umma kwa maana ya Serikali, Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma katika kuendesha miradi ambayo Serikali pekee haiwezi kuifanya. Kama jinsi ambavyo Wabunge wengine wamezungumza, hili ni jambo jema kwa sababu Serikali peke yake haiwezi kufanya kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini roho yangu ni nyeusi kidogo kutokana na jinsi ambavyo jambo hili limekuja. Ni jambo jema, limezungumzwa muda mrefu sana na limetakiwa muda mrefu sana, lakini nikiuangalia Muswada jinsi ulivyo, naona kama bado unachelea sana, yaani siuoni kama ni Muswada ambao utatusaidia kulifanya jambo hili jema liweze kutekelezeka vizuri. Nina mashaka kwamba tunaleta huu Muswada kwa sababu tu Wazungu wamesema ni lazima uje, wamezuia misaada na kusema kwamba, mionganoni mwa mambo ambayo hayajatekelezwa ni *PPP* kana kwamba, wao ndio wanaonekana wanasukuma zaidi suala hili.

Pamoja na kwamba tumelizungumza sana, tumelitaka sana na lina faida sana, lakini ilipaswa sisi wenyewe kujiridhisha ni aina gani ya *PPP* ambayo tunaitaka. Kwa hiyo, kama nilivyosema hapo awali, pamoja na kwamba jambo hili ni zuri, lakini roho yangu ni nyeusi sana kwa jinsi ambavyo tunalipeleka. Nimeusoma huu Muswada zaidi ya mara tatu sioni ni vipi ambavyo Muswada huu unaweza ukasaidia kuifanya tasnia hii ya

ushirikiano wa Serikali na Sekta binafsi kuwa ni bora na uweze kutusaidia. Naona kama vitu vimekwenda haraka haraka sana kwa maandalizi ya Muswada wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa tulilonalo Tanzania ni *Contract Management* kwamba tunaingia *contracts*, whether *contracts* ni nzuri au ni mbaya, maana yake kuna wimbi kubwa sana sasa hivi la kusema mikataba mibovu, mikataba mibaya ni wimbi kubwa na la muda mrefu, lakini tatizo kubwa tulilonalo ndani ya nchi yetu ni kwamba, baada ya kuingia mikataba ni nini kinafuata? Ni kitu gani ambacho kinatufanya tuhakikishe kwamba wale *contracting parties* wanatekeleza wajibu wao wa kimikataba? Ndiyo tatizo kubwa sana ambalo tunalo. Sasa tunakwenda kwenye *PPP*, tunasema *Tanzania Investment Centre* ndani yake ndiyo kutakuwa na *unit* kwa ajili ya *PPP*. *Tanzania Investment Centre* kazi yake ya kisheria ni kuleta wawekezaji, kuwatafuta wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, halafu unawapa jukumu la ku-coordinate utekelezaji wa hiyo miradi ya kiuwekezaji. Hapa kuna *conflict of interests*. Haiwezekani, mtafute wawekezaji awalete, awape *incentives*, huyo huyo ndiyo asimamie kuhakikisha kwamba ile miradi inafahamika.

Mimi nilikwenda Malaysia, Malaysia ni moja ya nchi ambayo tunaitolea mifano sana kwa upande wa *PPP*. Naamini kabisa katika maandalizi ya Muswada huu Serikali imeliangalia hilo kwamba imeambiwa kule Malaysia Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo ambayo inasimamia miradi ya *PPP*. Maana yake *coordination unit* ya *PPP* Malaysia iko ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu wa Malaysia. Lakini Ofisi ya Waziri Mkuu wa Malaysia, Waziri Mkuu wa Malaysia ni *executive*, Waziri Mkuu wa Tanzania sio *executive*.

Sasa sijui kama hatukutaka kufikiri sana au tulikuwa tuna haraka kwa kuwa tunajua *TIC* iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, basi tukaenda tukasema kwamba tuiweke chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *It is completely wrong*. Bado Ofisi ya Waziri Mkuu inaweza ikawa ndiyo inaratibu kwa ujumla miradi hii yote ya *PPP*. Kwa sababu anayesema kwamba anataka kujenga barabara hii kwa *PPP* sio yule mwekezaji, sisi ndio tuna-*identify* maeneo ambayo tunayataka, halafu tunatangaza tenda kwamba tunataka eneo hili tulifanye kwa kupitia njia ya *PPP*.

Mfano mzuri sasa hivi ni mradi ambao *NSSF* wanataka kufanya wa kujenga barabara ya *eight lane* kuanzia Ubungo mpaka Chalinze. Sasa ile itakuwa ni *PPP*. Lakini ni *PPP* ya ndani kwamba Serikali yetu ya umma ya ndani inajenga barabara, itatoza tozo likirudisha *investment* yake, barabara ile inakuwa mali ya Serikali.

Kwa hiyo, Serikali mnakaa mnasema kwamba kivuko hiki tunakitaka, hatuna pesa, tutafute pesa za Kampuni za watu binafsi ndio wanakuja watu wanaingia mkataba mnakubaliana baada ya miaka mingapi, watakuwa wamerudisha *investment* yao na faida kidogo na ule mradi utakwenda Serikalini lini. Maana yake miradi yote ya *PPP* ni kwamba baada ya muda itarudi kwenye Serikali, itakuwa ni mali ya umma. Kwa hiyo, ile ni *financing* tu, njia ya kupata fedha kwa ajili ya hiyo miradi.

Sasa jambo hapo la kuangalia, kwa mfano sisi tulikuwa tuna *Consolidated Holdings*, kabla ya hapo tulikuwa tuna *PSRC*, tuna *NDC*. *Consolidated Holdings* pamoja

na *PSRC* ya zamani wana uzoefu wa muda mrefu sana wa *privatisation* licha ya kwamba kuna matatizo mengi kwenye *privatisation*. Kama nilivyoeleza, ni suala la *Contract Management*. Juzi hapa Waziri wa Viwanda na Biashara walifanya utafiti na kugundua viwanda vingi sana ambavyo vilibinafsishwa havijafanya kazi na wala Serikali ilikuwa haijui kama havijafanya kazi na Serikali, imeamua kuvirudisha kwenye mikono ya Serikali.

Sasa ule uzoefu ambao ulijengwa kwenye *PSRC* mpaka *Consolidated Holdings* uzoefu ule ungeweza kutumika na hii *unit, autonomous unit* kama Mheshimiwa Kaboyonga alivyosema kwamba ni lazima chombo ambacho kinaratibu shughuli hizi kiwe *autonomous*, inakuwa ni Shirika la Umma ambalo halifanyi faida. Kazi yake ni kuangalia mikataba na kuisimamia na kuhakikisha kwamba baada ya muda, yule mtu anapata fedha zake na mali ile imerudi kwenye Serikali kama jinsi ambavyo mikataba itakavyokuwa.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria tujaribu kuangalia upya hili eneo la *Tanzania Investment Centre* kuratibu na tuunganishe *financing part* na uratibu pamoja na kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo itakuwa inaangalia kwa ujumla, lakini *answerability* ya kile chombo, *autonomous* kiwe chini ya Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba masuala ya uangalizi na masuala ya *financing* yanakwenda kwa pamoja. *Alternatively*, kama jinsi ambavyo Kambi ya Upinzani Bungeni ilivyozungumza ni *National Development Corporation*. Nchi nyingi zinafanya miradi hii kwa kupitia *National Development Corporation* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rwanda ni mfano mzuri sana ukiangalia na kusoma magazeti ya Kimataifa. Unakuta kila wakati wanatangaza tenda wao kwa ajili ya *PPP* kupitia Mamlaka yao ya Maendeleo. Wao wanaita Mamlaka ya Maendeleo, hawaiti Shirika la Maendeleo, sisi tunaita Shirika la Maendeleo. Kwa hiyo, tungeweza kufanya hivyo kupitia *NDC* mimi nachelea kukubali na ukiangalia ukurasa wa name pale *functions* za ile *coordination unit*, nachelea sana kukubali kuiweka chini ya *Tanzania Investment Centre, Tanzania Investment Centre* waendelee na kazi ya kutafuta wawekezaji wa ndani na wa nje na kuwapa *incentives*. Uratibu wa miradi ya *PPP* ufanywe na chombo kingine kuondoa hiyo *conflict of interest* ili iweze kutusaidia.

Mheshimiwa Kaboyonga alizungumzia suala la *CAG* ku-audit na suala zima la Mashirika ya Umma ambayo hisa za Serikali ni kidogo. Suala kimsingi *CAG* kwenda kwenye yale Mashirika kwenda ku-audit hapana, suala ni kwamba *audited accounts* za yale Mashirika lazima zije kwenye Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma ili Bunge kama chombo cha wananchi kiweze kujua mali zao zilizoko kwenye Mashirika zinakwenda namna gani. Sio suala la *CAG* kuingia kwenye Kampuni.

Kwa mfano, *TBL* Serikali ina hisa asilimia nne tu. Kwa hiyo, haiwezekani *CAG* akaenda kulazimisha kukagua chombo ambacho *Private Persons* na watu wengine wana-own 96%, hapana. Lakini ile mali ya Serikali, ile *investment* ya Serikali ile ya asilimia nne inakwenda namna gani, inapata faida, inapata hasara na vitu kama hivyo. Hilo ndilo jambo ambalo tulikuwa tunalihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kwa mara nyingine tena niwatakie Watanzania uchaguzi mwema. Vyama vya Siasa vimeanza michakato tayari, wakati wa hotuba yangu kwa Wizara ya Miundombinu, niliwapongeza Chama cha Wananchi *CUF* kwa uteuzi wa Prof. Ibrahim Haruna Lipumba pamoja na Maalim Seif Shariff Hamad na Mheshimiwa Juma Duni kama mgombea mweza wa Prof. Lipumba. Chama cha Mapinduzi kimemaliza mchakato wake, wamemteua Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Dr. Shein kuwa Wagombea wao, nawapongeza sana, lakini nawapongeza zaidi kwa uteuzi wa Dr. Mohamed Gharib Bilal kama mgombea mwenza kwa sababu ile ni *assets* sana kwa Tanzania, ni mmoja wa *nuclear physits* tulionao wachache sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii ina *nuclear physits* watatu tu na ni mmoja tu ambaye yuko ndani ya nchi, mwingine anaishi Canada na mwingine anaishi Marekani. Inawezekana hata wameshachukua na uraia wa hizo nchi maana hatuna *dual nationality*. Kwa hiyo, kulikuwa kuna kitu ambacho hatukitumii kwa kweli. Dr. Bilal ilikuwa ni *asset* ya nchi ambayo hatuitumii. Kwa hiyo, napenda kumpongeza yeye binafsi kwa uteuzi ambaeo ameupata kwa mgombea wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nirudie kusema kwamba jana nilizungumza hapa na Mama Anna Abdallah akadhani kwamba nataka wazee waondoke, hapana. Mimi naheshimu sana wazee, wazee ni hazina, hekima ya nchi ni lazima waendelee kutupa uongozi na kadhalika. Nilichokuwa nakisema ni kwamba ndani ya nchi yetu tuna tatizo la jinsi gani ambavyo tunawaandaa vijana kuja kuwa viongozi, jinsi gani ambavyo tunaanza kuwapa *responsibilities* vijana ili waijue nchi yao, waijue historia ya nchi yao watakpopata mamlaka ya nchi waweze kuongoza nchi iwe kwenye *self hands*. Ndiyo kitu ambacho nakizungumzia.

Kwa hiyo, tunapokuwa na wimbi kubwa la vijana ambaeo ndio *majority* katika nchi hawaandaliwi, maana yake tuseme ukweli zamani wakati wa mfumo wa Chama kimoja miaka ya 1970 ile kulikuwepo na *Tanu Youth League*. Ilikuwa inaandaa watu kuja kuwa viongozi. Viongozi wengi ambaeo tunaowaona hivi sasa ni ambaeo wameandaliwa.

Lakini baada ya Mfumo wa Vyama Vingi, hatuna chombo chochote cha kuwaandaa vijana waje kuchukua *responsibilities* za nchi, hatuna. Wachache ambaeo tumepata fursa ya kuingia kwenye Mabaraza kama haya tukajifunza kuhusu nchi yetu, tukaijua nchi yetu ni bahati tu, lakini kuna wengi sana.

Leo, kesho na kesho kutwa anaweza akatokea mtu anauza madawa ya kulevyaa kapata fedha akaenda kwenye Jimbo akahonga akawa Mbunge akaingia hamna *vetting* akawa Waziri au nani ambaye hana hata historia ya nchi, haijui!

Kwa hiyo, nilichokuwa nakizungumza ni hicho kwamba wazee mtusaidie mkishakuwa mmetufikisha hapa, maana yake lazima mkumbuke na nyie wakati tunapata uhuru mlikuwa vijana mkapewa nchi mkiwa vijana, kwa hiyo, ni lazima ifikie wakati muwaandae vijana wa kizazi cha sasa wapambane na changamoto za sasa. Kuna changamoto ambazo wazee wa sasa hamtaweza kupambana nazo, lazima mtuandae sisi

tuweze kuzichukua na ndiyo hoja ambayo nilikuwa naizungumza jana na naomba nieleweke hivyo.

Sisemi tuwaondoe wazee Bungeni, haiwezekani, tunawahitaji, tunahitaji busara zenu, tunahitaji hekima zenu, tunahitaji mwongozo wenu, lakini tunawahitaji mtushike mtuonyeshe njia ili mtakapokuwa mmeondoka mhakikishe mmekaa pembeni kwenye *retirement* na nchi yenu inakwenda vizuri. Hilo ndilo ombi ninalolitoa na naomba wazee kwa kweli wale ambao wameamua kujiondoa kugombea tunawapongeza sana, Mheshimiwa Mzindakaya, Mheshimiwa Kimiti wote wale ambao bado, sawa tuendelee. Lakini mjiandae basi ili mtuachie tuweze na sisi kuchangia katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nawatachia Watanzania uchaguzi mwema nawa-*encourage* vijana nendeni mchukue fomu za Udiwani, Ubunge tujae humu ndani tuitumikie nchi yetu, tujifunze kuhusu nchi yetu na tuiongoze nchi yetu tuipeleke hatua mbele zaidi ya hapa ambapo tumefikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Kabwe Zitto, lakini sikubaliani nawe na hoja yako ya mwisho kwamba nchi haina mpango wa kuwaandaa vijana. Hivi wewe huoni Spika na Naibu Spika wananiandaa hapa! (*Makofi/Kicheko*)

Sasa namwita Mheshimiwa Magalle John Shibuda atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya.

MHE. MAGALLE J. SHIBUDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii na mimi niweze kuchangia hoja hii ya ubia baina ya Serikali na watu au Kampuni binafsi. Awali ya yote naomba kukumbusha tu Serikali kwamba ubia uanzie kwa Watanzania wenye kwa wenye kuweza kuwa na fursa za kutumia rasilimali za Tanzania. Naomba nijielekeze kwa wafugaji. Naiomba Serikali itambue kwamba wabia wanaotoka nje wakipiga kelele kwamba wanahitaji kulipwa fidia, Serikali hutoa fidia haraka sana.

Sasa naomba kuikumbusha Serikali wabia kwa Ustawi na Maendeleo ya Jamii ya Tanzania, wafugaji waliodhulumika, Serikali ifanye utaratibu wa kuwalipa pesa zao. Naomba Serikali itambue kwamba wafugaji walishiriki kikamilifu katika kudai uhuru wa Tanganyika na vivyo hivyo wanaweza wakakasirika wakatunyima ridhaa ya kuwa na madaraka chama chochote kinachohitaji kushika dola. Kwa hiyo, niliona nianze na hili niwakumbushe Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, naomba sasa nijielekeze kwenye hoja hii. Kwanza, naomba ubia ujenge kanuni ambazo zitahakikisha kwamba maslahi ya kujenga ujamaa na kujitegemea yanakuwa ndani ya mkondo wa safari ya nchi yetu. Vile vile nashauri kwamba kanuni ziwape wabia wa maelekezo ya kuwapatia manufaa

wazalendo, wabia kutoka nje tusiwapendelee kwa kila kitu kwa hofu ya kwamba tutakosa wawekezaji. Ni heri uchelewe lakini ufike salama.

Vile vile napenda kusema kwamba kanuni hizo ziwe fursa za kujenga maridhiano. Mikataba inapokuwepo, basi mikataba hiyo isifungwe moja kwa moja kwamba kama kuna makosa, hakuna kujenga maridhiano ya kusahihisha. Kwa hiyo, nashauri kwamba kanuni zilinde maslahi hayo. Vile vile, napenda kutambua ya kwamba kama alivyosema mwenzetu Mheshimiwa Zitto kwa kweli *Contract Management* isimamiwe na tuhakikishe inakuwepo. Tusiwe watu wa kila siku tunahubiri kama wahubiri wa Kiinjili au wa madhehebu, naomba tufanye vitu kwa vitendo. Vile vile tukiwa na ulinzi wa kanuni pamoja na sheria tutahakikisha kwamba usalama wa rasilimali zetu unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtenda mema hulipwa mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba nipo hapa nahitimisha miaka mitano, lakini wanasema kwamba, “Aliyekujenga amekutia rutuba” ni lazima inaanzia kwa familia yako. Kwa hiyo, nachukua fursa hii kumpongeza mke wangu Sakina pamoja na watoto wangu nikianzia na Allen John Shibuda, Edwin John Shibuda, Stanley John Shibuda na John Shibuda *Junior* na *Princess* Hellen Shibuda ambao wote ni watoto wangu. Nawapongeza sana kwa uvumilivu, poleni kwa upweke, lakini napenda kuwashakikishieni wanangu na familia yangu, mke wangu, nawapenda sana. Vile vile nawapenda ndugu zangu wote madada wa kiukoo, kaka, binamu, wajomba, kila mtu anayenihu nampenda sana na panapo majaliwa basi tutaendelea kusaidiana kadri ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, vile vile napenda sasa nitumie nafasi hii kutoa pongezi maalum kwa Baraza la Madiwani Maswa linalomaliza muda wao, Wenyeviti wa Vijiji, Kata, vile vile nawapongeza Makatibu wa Matawi, Kata na Viongozi wote wa Chama cha Mapinduzi, Viongozi wa Madhehebu yote na nawapongeza wazee wangu wote akina mama na vijana ambao daima mmekuwa mkinipa upendo na daima mmekuwa ngome kongwe ikipigwa radi haipasuki kwa jinsi mnavyonipenda niendelee kuwa Mbunge wenu wa Jimbo la Maswa, lakini sasa tuna majimbo mawili tutaendelea kushirikiana.

Vile vile naomba nitumie fursa hii kumpongeza Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuidhinishwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea wa Kiti cha Urais wa Tanzania. Nashukuru, naringa sana kwamba niliyemwachia baada ya mimi kujiondoa kwa sababu nimeahirisha amechaguliwa kwa kishindo. Kwa hiyo, upeo wangu wa maamuzi uko sahihi, lakini napenda kutoa angalizo mwaka 2015 natumaini mtani wangu huyo ndio atakuwa mshenga wangu wa kunipigia debe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, natumia fursa hii kumpongeza Dr. Mohamed Gharib Bilal kwa kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza na vile vile napenda kumpongeza Dr. Shein kuwa mgombea wa Zanzibar, nawapongeza wote. Ni vyema nikatumia fursa hii pia kuwapongeza wananchi wa Maswa kwa jinsi wanavyonipenda na

ridhaa wanayonipigia kila siku kama nitakwenda Jimbo gani. Lakini napenda kutumia nafasi hii kuwaasa waliopewa bakshishi na watu wanaotaka kuwa wagombea wa majimbo, Jimbo la Magharibi au Mashariki msiwe na wasiwasi kuleni kwa sababu ni msimu wa wajinga ndio waliowao. “Kiendacho kwa mganga hakirudi.” Kwa hiyo, naomba niwaambie: “*Kisembamite kitashogaka.*” Maana yake, kiendacho kwa mganga hakirudi.

Ndugu zangu hakuna kesi yoyote mtakayoshtakiwa kwamba mlikula pesa za mtu. Wale wanaotoa pesa na hongo subirini niwaambie mtapata kizunguzungu cha kuliwa pesa zenu kwa sababu kura hazitatosha.

Vile vile napenda kutumia fursa hii kuwatahadharisha kwamba msichague mtu ambaye anakuja tu kwa jina la kwamba nataka Ubunge lakini ana historia ya kudhulumu, mapunjo au mtu ana historia ya kuwa na tabia ambazo ni hulka ya wizi, *u-master key*, spana malaya, matendo ambayo ni dhuluma na dhihaka na fedhuli kwa jamii. Kwa hiyo, nawaomba muwakatae wote hao na mimi nitaungana nanyi kuwatetea kwa jambo lolote litakalojitokeza. Maswa kataeni, waambieni hatudanganyiki, kwa sababu Maswa haiwezi kuwa maficho ya viongozi wabovu. Kwa hiyo, kumbukeni *SHIRECU* ilidhulumika, tukaliwa, tukafilisika ndiyo maana ushirika hauendi. Kwa hiyo, naomba palipo na mivumo ya kwamba fulani hafai ni mwizi mnyimeni kura hata kama namna gani.

Vile vile napenda kuwahakikishia Viongozi wa Kata na Matawi kwamba mkiwakataa hata kama ni Kiongozi wa CCM lakini hana sifa za kuwa Mbunge tumnyime kura kwa sababu hatawakata majina yenu wakati wa kupendekeza kipindi kijacho cha kuwa wagombea.

Vile vile napenda kutumia nafasi hii kuwataarifu wananchi wa Maswa kwamba Tume ya *IGP* ya Wizara ya Mambo ya Ndani inakuja kukagua dhuluma zilizotendeka kwa wananchi. Iko Maswa hivi sasa, kwa hiyo, karibuni kwa Ofisi ya Mbunge na pia nawakaribisha watu wote ambao wanajua walidhulumika. Vile vile napenda kuipongeza Serikali, itamtuma Msaidizi wa Mwanasheria Mkuu na Mkurugenzi wa Mashtaka, wanakuja Maswa kukagua Magereza, yejole yule anayejua kwamba kuna ndugu yake au rafiki au jirani au Mtanzania aliyeonewa, njooni haraka ili tuweze kuhakikisha tunasafisha. Operesheni Chakaza karibu nitaitangaza na nitajua nitakwenda kugombea jimbo gani msiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapiga kelele amba ni wajarismali wa uongo na uhondo wa kupumbaza masikio naomba kuwaambia kwamba Maswa hatudanganyiki wala siasa msiwachague kwa sababu hawana utu, wanatafuta dhamana za kuwa Wabunge lakini hawana ujasiriamali kwa maslahi. “Bundi akiigiza sauti ya njiwa mjue huyo analeta kilio”.

Kwa hiyo, hao wanaotoa misaada ni sawasawa na bundi wanaoigiza kuwapenda. Walikuwa wapi wakati tunatafuta michango ya shule, ujenzi wa hospitali au wamesaidia yatima wangapi? Kwa nini hivi sasa wanakuja na porojo za pesa? Wakataeni hao ni mashetani na mvua haitanyesha kama mtawachagua. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia nafasi hii kumpungeza Katibu wa Jimbo la Maswa Bi Ziada Khamis kwa kazi kubwa alizofanya kwa maslahi ya wananchi wa Maswa. Ni mwanamke jasiri alionyesha kwamba wanawake wanaweza kuwa Makatibu wa Majimbo. Ninaomba atakapoomba Udiwani wa Patapenda, basi akinamama mpeni kura zote za ndio kwa sababu hilo ndilo pambazuko jipya la akinamama kuhakikisha wanalinda maslahi ya haki.

Naomba Bi Ziada Khamis apewe kura zote kwa sababu ye ye ana uzoefu wa kujua nini kinahitajika aende kwenye Baraza la Madiwani akawatetee wanawake na kila eneo ninalopewa *lunch*, naomba kuwaambia kwamba mnadhulumika. Mimi nitakuwa Maswa kuanzia Jumapili na napenda ku wahakikishia kwamba ahadi zangu zote zinatolewa na zitakamilika kwa hundi mtakazopewa na maeneo mengine nitatoa pesa taslimu na vile vile kwa watu ambao ni wa madhehebu ambao hawachangiwi na Mfuko wa Jimbo naahidi nitatekeleza.

Kuanzia tarehe 19 mpaka 21 Julai nategemea kati ya tarehe hizo nitatangaza kwamba nitagombea Mashariki au Magharibi. Lakini napenda kuwaambia wananchi wangu wa Jimbo la Mashariki ninawapenda na msiwe na mashaka, hakuna tapeli atakayekuja Mashariki nitashirikiana nanyi tuamue ni nani kama mtapenda mimi niende Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wananchi wa Magharibi pia naomba kuwatahadharisha sitakubaliana na dhuluma na shida ambazo mmekuwa mkizipata hasa wakulima za zao la pamba na korosho na mazao mbalimbali kwamba angalieni kuna matapeli wameleta pesa za bandia msikubali, angalieni kwenye minada yenu na masoko yenu msidhulumike. Mimi napenda kuwaambia wananchi wa Magharibi kwamba mimi ni mtoto ambaye nimezaliwa N'gong'o Maswa. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi kwamba Shibuda atakwenda wapi, lakini mimi ni mtoto wa Wilaya ya Maswa. Nahitaji Maswa kwa ujumla iendelee bila ubaguzi wowote.

Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi wa kwamba Shibuda atakwenda wapi. Lakini mimi ni mtoto wa Wilaya ya Maswa, nahitaji Maswa kwa ujumla iendelee bila ubaguzi wowote. Kwa hiyo, napenda ku wahakikishia kwamba kama nitakuwa Mashariki, basi Magharibi nitashirikiana nao. Kama nitakuwa Magharibi na najua Magharibi mnanipenda sana, Mashariki kila siku mnanipigia simu, sasa tukae tufanye uamuza wa busara, uamuza mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, natoa shukrani na naunga mkono hoja na naona mafundi cherehani wa uongo wasiendelee kushona mapambo ya uongo. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Huyo ni Mheshimiwa John Shibuda akichangia hoja ya *PPP*.
(*Kicheko*)

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hasa katika siku hii ya leo ambayo ni siku ya mwisho kwa kazi zetu. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuweka kuwa hai na kutusaidia katika kazi zetu. Lakini pia napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru akina mama wa Mkao wa Ruvuma kwa Wilaya zote tano, lakini vilevile sio kuwashukuru tu kwa ushirikiano walionipa na kuniongoza wakati wote na kunisadia na hivyo kufanya Mkao wetu kuwa katika Mikoa ambayo imefanya vizuri. Taarifa ya kazi nimeandaa wataipata na wengine watakaopenda kujifunza kutoka Ruvuma karibuni taarifa ipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio rahisi kufanya kazi miaka mitano usimguse mwenzako kwa namna moja au nyingine. Kwa hiyo, kwa wale ambao wanaona nilitenda mazuri, basi sifa hizo na zirudi kwao na kwa Mwenyezi Mungu na kwa wale ambao niliwakosea, basi wanisamehe kwa kuwa na mimi ni binadamu katika utendaji wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Amani Karume kwa kuachia uongozi kidemokrasia kwa sababu ukishakaa kwenye uongozi mtu unapenda kuendelea. Lakini yeye ametuvusha kiasi kwamba tumefanya mabadiliko kwa uzuri kabisa na hii ndiyo hali ya amani na utulivu wa Tanzania. Hayo yote yamefanyika chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, tunampongeza. Tunampongeza Dr. Shein, Dr. Bilal na hali kadhalika tunawapongeza wote waliokuwa katika ule msafara, tunaamini mafanikio bado yapo kwao kwa kuwa kila umivu lina mazuri yake. Ninaamini watafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umekuja kwa wakati mzuri sana na hasa kipindi hiki ambacho tunatarajia kustaafu hapa Bungeni. Lakini niseme tu kitu kimoja ili kufanikisha Muswada huu, itategemeana sana na jinsi ambavyo wahusika au wadau wakuu wa Muswada huu watakavyokuwa wanaushughulikia. Mimi ni mdau katika masuala ya taka pale Dar es Salaam ambaye shughuli zao zinafanyika kama vile lengo la Muswada huu. Kwa bahati nzuri *ILO* tunawashukuru sana wamekuwa mstari wa mbele katika kulisukuma suala hili la *Public Private Partnership* na mimi nimehudhuria pia katika kozi zao mbalimbali. Kwa hiyo, naona ni Muswada Mzuri sana.

Lakini napenda kulenga zaidi katika maisha ya watu wa kawaida katika jamii yetu na katika Serikali za Mitaa kwa sababu huko ndiko kwenye watu wengi ambao ni maskini ambao wanaweza kutengeneza ajira kwa kutumia matatizo mbalimbali yanayotuzunguka. Lakini kwa kushirikiana na Serikali, hili limeweza kufanyika katika suala zima la uzoaji wa taka Dar es Salaam na maeneo mengine ambayo waliiga mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti kitu nilichojifunza ni kwamba wakati mwingine Watanzania hatupendi sana kujivunia mafanikio yetu. Wakati tunaanza zoezi la uzoaji wa taka Mzee Keenja alikuwa mmojawapo wakati ule kwa kweli Jiji lilibadilika kwa sababu nakumbuka nilipata wageni kutoka Norway vijana fulani nikawaauliza mnaonaje Dar es Salaam? Walichonijibu wakasema tunaona hali yake sio safi, lakini baada ya muda Jiji lilibadilika na likawa zuri kwa usafi. Wakandarasi wale kwa kuambiwa kwamba utachukua eneo fulani ili uweze kufanya kazi na hela utakusanya mwenyewe kwa kiasi

fulani wakafikiri ni kazi rahisi. Wakachukua mikataba mikubwa mikubwa wengine wakakopa wakajua kwamba watapata hela nyingi za kutosha.

Kwa bahati mbaya sana msukumo wa kuwashauri wananchi waweze kulipia taka ulikuwa ni mdogo na wakati zote Makandarasi wanachukuliwa kama ni watu ambao wanaingiza hela nyingi sana kiasi kwamba ule usaizidi katika shughuli yenyewe katika ya usoaji taka unakuwa ni mdogo na matokeo yake Jiji linazidi kwenda chini kiusafi.

Lakini pia niseme kwamba kuna mambo mengi makubwa tunayapanga humu ndani, lakini mambo yanayohusiana na taka kidogo hatuyapatii uzito unaostahili. Tunasema kwamba kila mtu awe na choo. Inakuaje Majiji yetu yanapangwa hayana choo, tunatumia *flying toilets*? Kwa maana ya kwamba Jiji kama halina dampu la kutupa taka la uhakika, kama halina uwezeshaji wa taka wa uwezeshaji ni sawa na mtu anayeishi bila ya choo, lakini ule mradi haueleweki vizuri unakwenda vipi? Mimi ninafikiri kwamba kwanini maeneo mengine yanapewa kipaumbele kwa mfano barabara inaeleweka kabisa kwamba kuna kodi zitakusanya zitatengwa pesa na watu wataambiwa wafanye kazi hii na analipwa kwa kazi hii. Lakini kwenye hii ya taka ambayo tayari Makandarasi wa Tanzania wote wamekaa pale msaada hauonekani moja kwa moja.

Nikagundua kwamba yale mambo mazuri tunayofanya sisi na yanayotuhusu sisi wenyewe hatuyapi msukumo na kujivunia. Hivi kweli angekuwa mgeni amekuja kufanya kazi ile angepewa mikataba ambayo inayumbayumba vile? Angekuwa hasaidiwi? Kwa vyovyyote vile tungesema tukifanya hivyo huyu Mkandarasi ataacha au huyu mwekezaji ataacha. Lakini inapokuja suala la *local*, halipewi uzito unaostahili. Kwa misingi hiyo, nasema kwamba hata Muswada huu hatujapata nafasi nzuri ya kuupitia, lakini kwa sababu tutarudi tena hapa Bungeni, tutauita tena kama tutaona una mapungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaloona ni kwamba hebu tutengeneze mazingira ambayo tunakuwa na hali ya kutengeneza mikakati yetu sisi. Sasa hivi tuna wasomi wengi tu wanahitaji ajira, lakini wanahitaji watu wa kuwasaidia kutengeneza hata vijikampuni na wawezeshwe katika kuwasaidia kufanya ile kampuni iweze kufanya kazi. Kuwatengea maeneo inawezekana na sio lazima wote wawe ni waajiriwa. Kuna watu ambao wako tayari kutumika kama *think tanks* lakini kwa kujitolea. Wapo wengi! Kwa hiyo, ninachofikiri ni kwamba mbali tu ya kuitisha hii Sheria tuangalie pia jinsi gani tutatengeneza *think tanks* katika *levels* za Mikoa za kuweza kusaidia hasa vijana wetu tuweze *ku-tap opportunities* kuanzia huku kwenye maeneo ya maisha yetu ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimegundua nchi hii ina utajiri mkubwa sana wa watu. Nimejifunza katika Kituo chetu cha *Better Life Tanzania*, akina mama wale ambao walikuwa ni wa maisha ya kawaida kabisa baada ya kujifunza mbinu za ujasiriamali wamekuwa ni walimu wakubwa kwa wenzao. Wameleta mabadiliko makubwa sana katika Mikoa wa Ruvuma. Kumbe inawezekana. Kwa hiyo, tushuke sasa chini ili tuweze kuwatumia watu wetu vizuri zaidi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme pia kwamba katika *definition* naona imezungumzia *Private Sector* kama *NGO*, kama Makampuni, lakini

simwoni mtu binafsi amejitokeza. Inaweza ikatokea mtu na pesa zake akaamua kuwekeza katika mradi fulani, kwa hiyo, nafikiri waiangalie vizuri namna ya kuweza kumchukua mtu binafsi atakayeamu kuingia ubia katika kuwekeza katika miradi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, kwa kuwa tupo katika kipindi cha mwisho, niseme tu kwamba kwa kweli nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo wa Mkoa wa Ruvuma pamoja na sisi wenyewe wa Viti Maalum kwa jinsi ambavyo tumeshirikiana kwa nia njema ya kuendeleza Mkoa wetu. Ingekuwa amri yangu ningetamani turudi kama tulivyo kwa sababu tumefanya kazi nzuri katika Mkoa wetu. Ruvuma sasa inang'ara kiasi kwamba mmoja akiondoka tunaona kama timu yetu itakuwa imeyumba. Lakini hayo yawapendeze wenyewe wananchi kadri watakavyofanya maamuzi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi, wengi walikuwa wananiuliza Mheshimiwa Manyanya unagombea wapi? Unakwenda Jimboni? Mbona tunaona unatosha? Nenda Jimboni! Nilivyokwenda kule nyumbani, wengine walifikia kulia kwanini hujaja Jimboni. Niliwaambia hapana kwa sababu uongozi ni pamoja na kuwa na subira, pamoja na kuheshimu wenzako walilolifanya. Mimi nimejiridhisha kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Majimbo wamefanya vizuri na kwa bahati nzuri na wanawake wamesema: "Hatutaki uende kwenye Jimbo, ubaki na sisi uendeleze uliyoyafanya."

Kwa hiyo, najisikia furaha kuungana nao kuingia kwenye timu ile ya mashindano. Yawezekana tukavuka wote, tutashukuru. Lakini naamini tutavuka wote kwa sababu kazi tulizozifanya kweli zinaonekana na zinaweza kunadika kwa wenzetu na vilevile ni heshima kwa wana-Ruvuma kusema kwamba wenzetu wamefanya kazi hii, basi tuthamini ule mchango kama ambavyo tunathamini katika ngazi nyininge.

Hiyo inatia moyo na kuwahamasisha Wabunge kwa wanaofanya kazi zao wakijua kwamba tukifanya vizuri tatarudishwa tena. Lakini mtu anapokuwa amefanya vizuri halafu hajarudishwa anakata tamaa na badala yake anakuwa mlafi, anasema kwamba hawa bwana hata ukiwafanyaje hawakumbuki wakati mwingine.

Kwa hiyo, mimi kwa nafasi hii nawashukuru na kuwathamini sana wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa jinsi ambavyo wameonesha heshima kwetu kwa kipindi chote na kutu-*support* wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ahsante sana na nakiombea Chama cha Mapinduzi kishike tena utawala kwa sababu ndiyo chama kizuri chenye sera nzuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya mwisho niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu. Nakutakia kila la kheri katika maisha yako na katika nafasi na jitihada zako za kujitafutia nafasi ya maisha bora hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo huu wa ushirikiano kati ya Serikali na watu binafsi ni mfumo mzuri sana na napenda kusema kwamba ni mfumo ambao umefanya sehemu kubwa ya dunia kufanikiwa kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Muheza tunayo mambo ya kujivunia kati ya ushirikiano huo wa *Public Private Partnership*. Hospitali teule ya Muheza ni moja kati ya mifano hiyo mizuri sana. Zipo Hospitali teule hapa nchini ambazo zinaendeshwa kwa ubia kati ya Serikali na Taasisi za Dini na katika maeneo mengine Serikali na watu binafsi na zinatoa huduma nzuri sana. Hospitali yetu ya Muheza ilikuwa inafanya kazi vizuri sana na ubia ule umekuwa na manufaa makubwa sana. Hata hivyo, tumeona kwamba kazi zimekwenda vizuri katika hospitali ile lakini inawezekana imetokea kasoro kidogo wenzetu katika upande wa pili sasa, hali yao sio nzuri na uwezo wa kuchangia umepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msingi wa makubaliano ya uendeshaji wa pamoja wa hospitali ile, sasa Serikali imechukua jukumu lake kikamilifu. Kwa mfano, sasa mishahara yote ya Madaktari na Manesi wale waliokubali ajira Serikalini inalipwa na Serikali. Haya ni mahusiano mazuri. Vinginevyo mfumko wa Manesi na Madaktari kuondoka katika Hospitali teule pale Muheza ungeendelea kufanyika na pengine leo tungekuwa hatuna Madaktari wala Manesi wa kutosha.

Lakini lipo jambo lingine zuri linaloonesha umuhimu wa ushirikiano huo wa uendeshaji wa shughuli kwa pamoja kati ya sekta binafsi na Serikali baada ya hali mbaya kudorora katika Hospitali yetu hivi karibuni tumewaomba Serikali na imekubali. Namshukuru sana Profesa Mwakyusa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa kukubali ombi la kuisaidia Hospitali ya Muheza sasa kuweka Jokofu kubwa la kuweza kuhifadhi maiti jambo ambalo limekuwa limekosekana kwa muda mrefu kutokana na upande wa pili kuanza kuwa na matatizo ya kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo lingine kubwa ambalo pengine ni vyema nikaliweka wazi, wananchi wa Muheza wakalisikia na Tanzania nzima. Nimejitahidi, tumeweza kufanya mawasiliano na wenzetu wa Marekani na wamekubali kutaka kuisaidia Tanzania katika ujenzi wa barabara. Kitu gani wanakuja kusaidia Tanzania? Sisi tunatumia fedha nyingi sana katika ukarabati wa barabara zetu za changarawe za udongo na changarawe.

Ukipiga mahesabu ya barabara za Mkoa na za Wilaya, fedha tunazozitumia kila mwaka kuzitengeneza barabara hizo ni fedha nyingi sana. Wenzetu wamekuja na teknolojia nzuri ya kutumia lami nyepesi. Kwa hiyo, haitaisaidia Muheza peke yake, itaisaidia Tanzania yote kwa ujumla na leo hapa ninapozungumza tayari wameshakubaliana na *TANROADS* na wataalam kutoka Marekani wanakuja kuanza kutuonesha Watanzania namna ya kutumia lami nyepesi ili tuachane na kutumia fedha nyingi kwa kutengeza kila mwaka barabara za udongo na za changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lini kazi hiyo itaanza? Kwa majiribio katika Afrika Mashariki na ya Kati Wamarekani hao wameichagua Tanzania na wameichagua kwenda kuanza kufanya kazi hiyo ya majaribio katika Wilaya ya Muheza na barabara itakayotoka Muheza kwenda Amani. Ninavyozungumza hapa, malighafi imekwishafika kiwanja cha ndege na wanateremsha malighafi ile tayari kwenda katika eneo wakati wowote kabla ya mwisho wa mwezi huu wa Julai tunaozungumzia.

Lakini hili likifanikiwa, litasaidia Tanzania nzima. Maana yake tutakuwa na uwezo wa kutengeneza barabara zetu za Wilaya kwa kiwango cha lami nyepesi kwa kiwango cha gharama ambayo sio kubwa sana, lakini tutazifanya kuwa imara na kuweza kupitika kwa muda mrefu. *PMMR* Tanga barabara ya Muheza itakuwa ya kwanza kwa Tanzania nzima kwa Afrika Mashariki na ya Kati. Naomba ushirikiano huu uendelezwe kwa sababu ndiyo utakaosaidia kukuza uchumi wa Tanzania. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokwenda Italia mwanzoni mwa mwaka huu, wenzetu kule walituambia wako tayari kutusaidia Tanzania. Wanataka kuja Tanzania ili wajenge kituo kikubwa kuliko vyote katika Bara la Afrika cha kuweza kuhifadhi watoto yatima. Sio kuwahifadhi tu, wanawahifadhi, wanawalea, wanawatunza na wanawasomesha kwa idadi kubwa, hawajawahi kufanya hivyo katika Bara la Afrika, lakini wanataka kuanzia Tanzania na wako tayari na wameshaanzisha *NGO* ambayo tayari imekwishaanza kazi hizo katika Mji wa Tanga. Wanakuja kufanya kazi hiyo na tumewakaribisha Muheza.

Matatizo ni urasimu katika kuwawezesha kupata eneo dogo la kujenga Kituo kile Tanzania. Watoto ni wa kwetu, yatima sio watoto wa kutoka Italia, watachukua watoto wa kwetu, watachukua zaidi ya watoto 1000 wawaweke mahali wawalee, wawasomeshe mpaka wakue, lakini vilevile watawachukua wale walioathirika na madawa ya kulevyu watawatunza mpaka waweze *ku-reform*. Kutoa heka kumi au ishirini au thelathini wajenge eneo hilo, urasimu unatuchukua zaidi ya miezi sita, hatujaweza kuwakamilishia. Lakini naamini ndugu zangu wa Wizara ya Ardhi ambao nimeshazungumza nao watasaidia kuona kwamba jambo kama hili linatekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo niseme tena kuhusu mradi wa umeme ambao sijauzungumzia sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Wizara hiyo ya Nishati na Madini. Mradi wa Umeme wa *MCC* katika Mkoa wa Tanga utaelekezwa pia katika Wilaya ya Muheza ambapo zaidi ya vijiji 17 vitapata umeme. Mheshimiwa Waziri ameshazungumza, *tender* zimefunguliwa jana, lakini vijiji vingi ambavyo viko katika programu hiyo ni pamoja na vijiji vya Tanganyika, Muheza Mjini, Paramo, Pembe, Bwembwera, Semngano, Mpapayo na maeneo mengi ambayo vijiji vyote 17 vitafanikiwa. Hii ni ishara kubwa ya kuonesha mashirikiano yaliyopo kati ya sekta hizi binafsi na sekta za umma.

Fedha hizi zinatoka katika Serikali ya Marekani na inawezekana kabisa sio fedha zilizotoka mikononi mwa Serikali ya Marekani ni fedha zilizotoka katika *Private Sector* za watu wenye uwezo mkubwa kule Marekani ambao wametoa nia ya kuisaidia Tanzania. Watanzania na sisi tuelekeze nguvu zetu, tuimarishe *Private Sector* za kwetu ili

ziweze kuwa na uwezo mkubwa wa kusaidia Watanzania pamoja na mahitaji yetu muhimu katika sekta zetu za afya, ujenzi, umeme na sekta nyingine zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niwashukuru sana tena kwa mara ya pili wananchi wa Wilaya ya Muheza. Tumeshirikiana kwa muda mrefu, tumeanya kazi nyingi, wameona jinsi barabara zinavyopitika, wameona jinsi zahanati zinavyoendelea kujengwa kwa uhakika kabisa na umeona jinsi mambo mengine mengi muhimu na jitihada za maji zinavyoendeshwa vizuri na wameona jinsi sekta ya kilimo na umwagiliaji.

Lakini wameona vilevile na *SACCOS* kubwa tulioianzisha yenyе uwezo mkubwa wa kifedha wa shilingi milioni 800 inavyowasaidia wananchi akina baba, akina mama na vijana na kuwawezesha hata uwezo mkubwa wa kuweza kujitegemea. Wengi wameweza kufanikia kwa kutumia *SACCOS* hiyo kwa kujinunulia pikipiki ambazo sasa zinaitwa bodaboda Muheza peke yake pale ziko zaidi ya 100. Maana yake tumewasaidia zaidi ya vijana 100 kuweza kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Herbert Mntangi - Mbunge wa Muheza na huyu ndiye alikuwa mchangiaje wetu wa mwisho asubuhi ya leo. Sasa naomba niwatangazieni kwamba jioni tutamalizia kwa wachangiaji watano wa mwisho kabla hatujamwomba Mheshimiwa Waziri apitie hoja zetu. Nao ni Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Anastazia Wambura atafuatia na mwisho atakuwa Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya kama mnavyojua Mheshimiwa Mzindakaya amekuwa hapa kwa miaka mmingi atatoa hotuba yake ya kutuaga jioni hii.

Waheshimiwa Wabunge, tunarudia kwa mara nyingine tangazo ambalo tumeshatangaza mara kwa mara la kuhusu tamko la mali na madeni kwa Kamishna wa Maadili kabla au ifikapo tarehe 16 Julai, 2010. Fomu za Tamko hilo zinapatikana katika Ofisi ya Katibu wa Bunge. Tunaomba Waheshimiwa tuzijaze na tuzirudishe kwa wakati. Kisheria zinatakiwa zijazwe kabla au ifikapo kesho kabla ya saa kumi jioni atakapokuja Mheshimiwa Rais hapa.

Tangazo la mwisho ni kwamba nilitangaza asubuhi kwamba Kamati ya Uongozi ya Bunge itakutana saa 7.00. Nirekebishe kidogo kwamba Kamati hiyo ya Uongozi ya Bunge itakutana saa 8.00, ukumbi ule ule wa kawaida Ukumbi wa Spika, lakini pia itakutana pamoja na Tume ya Huduma za Bunge.

Baada ya maneno haya, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Spika (Mheshimiwa Samuel J. Sitta) Alikalia Kiti

SPIKA: *Serjeant-at-arms*, naomba kengele ipigwe, tusubiri dakika tano.

*(Hapa Kengele ilipigwa ili Waheshimiwa Wabunge waliokuwa
nje ya Ukumbi wa Bunge waweze kurejea Ukumbini)*

SPIKA: Basi kwa matazamio kwamba wenzetu wanaendelea kuingia, na bahati njema wachangiaji watatu wamo humu ndani ya Ukumbi tayari.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawatamka wachangiaji wetu wa jioni hii, naomba kwa dhati nishukuru uongozi uliotolewa na Mheshimiwa Job Ndugai katika kuliongoza Bunge na shughuli zake humu ukumbini wakati ambapo Mheshimiwa Naibu Spika alikuwa amepata msiba juzi akaenda Njombe na mimi nilikuwa na sherehe ya ufunguzi wa Ofisi ya Mbunge kule Urambo.

Kwa hiyo, nimerudi leo asubuhi. Wakati wote huo wa siku tatu, mwenzetu Mheshimiwa Job Ndugai ameshikilia shughuli za Kiti kwa ufanisi mkubwa sana. Nampongeza sana. Namshumkuru pia, nina hakika Mheshimiwa Zuber Ali Maulid naye atakuwa ameshughulika katika nyakati mbalimbali, naye tunampongeza sana kwa kazi hiyo. Sio jambo jepesi, lakini wenzetu hawa wameweza kushughulikia kazi hizi bila kutetereka hata kidogo. Ahsante sana.

Sasa, wachangiaji waliosalia watano kwa mpangilio ufuatao:- Mheshimiwa Suleiman Kumchaya naye yupo, Mheshimiwa Rita Mlaki yupo, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa yupo, Mheshimiwa Anastazia Wambura bado na Mheshimiwa Dr. Chrisant nadhani kwa sababu hawa wanafuata baadaye, pengine tutawatarajia hivi punde. Kwa mpangilio huo, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Rita Mlaki na ajiandae Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa. Mna dakika kumi zile tulizokubaliana kila mmoja.

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kwa jioni hii ili na mimi niwezwe kuchangia kidogo. Lakini kabla sijaanza kuchangia, nami ningependa kuchukua nafasi hii kumpa pole Mheshimiwa Naibu Spika kwa kufiwa na kaka yake. Mwenyezi Mungu amweke mahali pema Peponi.

Pia, nichukue nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Spika kwa kufungua ofisi yako. Tumesikia na kwa utaratibu wako ule ule wa viwango. Hongera sana!

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi katika Mkutano Mkuu na Chama chetu cha Mapinduzi kuwa Mgombea wa Urais katika uchaguzi unaokuja mwezi Oktoba mwaka huu, na tunahakika ushindi wa kishindo utapatikana tena kwa mara nyingine.

Pia, nimponeze Mheshimiwa Dr. Mohammed Ghalib Bilal kwa kuwa mgombea mwenza na pia nimponeze Mheshimiwa Dr. Mohammed Shein kwa kuwa mgombea Urais Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hoja hii katika eneo la *empowerment*. Lakini, kabla sijaingia huko, ningependa ninukuu maelezo ya kitabu cha mwelekeo cha Chama cha Mapinduzi ambacho kimetolewa katika Mkutano huu Mkuu uliopita hivi karibuni. Naomba kunukuu: “Katika kitabu cha Mwelekeo wa Uchumi wetu kwa kipindi cha miaka 10 ijayo unatilia mkazo dhamira ya CCM katika uvezeshaji wa wananchi mmoja mmoja au katika vikundi. CCM inasema: “Mkakati mkuu wa uvezeshaji wa kiuchumi wa wananchi ni ule unaohakikisha kwamba wananchi wenyewe wanamiliki na kuendesha uchumi wa nchi yetu ama mmoja mmoja, kwa kupitia vyama huru vya ushirika au kwa kupitia kampuni za wananchi za ubia”

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kunukuu, CCM inasema: “Chini ya utaratibu wa kuwawezesha wasomi, wajasiriamali, wafanyabiashara wa kati na wa juu, CCM inaziagiza Serikali zake kuandaa mkakati wa kibenki ambaa utawezesha upatikanaji wa mikopo kwa makundi yote hayo. Benki nyingi tulizonazo sasa kwa aina ya shughuli zao ni benki za kibiaashara zaidi kuliko zile za kuendeleza sekta za uzalishaji mali hususan kilimo na mambo mengine”.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu wa *PPP*, kama hili halikuzingatiwa hasa katika eneo hili la *empowerment* ambalo lipo katika kifungu cha nne, kipengele cha tano, naomba nisome kwa kiingereza: “*The Public Private Partnership agreements shall endeavor to provide opportunity for empowerment of the citizens of Tanzania as provided for under the National Economic Empowerment Act.*”

Mheshimiwa Spika, ili Muswada huu ama hoja hii ama sheria hii iweze kufanya kazi, eneo hili lazima lizingatiwe kuwawezesha Watanzania kushiriki kikamilifu katika uchumi wao katika nchi yetu hii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya kwa sababu za msingi kabisa. Kama nilivyosema katika mwelekeo wa uchumi uliotolewa na Chama cha Mapinduzi, benki zetu hizi bado hazijawa tayari kumjali mwananchi wa kawaida. Unapokwenda benki kwenda kuomba mikopo, kuna masharti mengi sana ambayo mwananchi wa kawaida hawezi kuyatimiza hata kidogo ili aweze kupata mkopo huo. Matokeo yake, hii *PPP* itafanya kazi kwa wageni zaidi, kwamba mgeni ama kampuni za binafsi kutoka nje zinakuja Tanzania zinashirikiana na makampuni yetu ya umma na zinaendesha uchumi wa nchi yetu na kuwaweka Watanzania pembeni. Hivyo basi, ili *PPP* hii iweze kufanya kazi, ninaomba sana Serikali kwa nguvu zake zote iandae mazingira mazuri ya kuwashirikisha wananchi ili na wao wawe na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika *PPP*.

Mheshimiwa Spika, wenzetu katika nchi nyingine, hili wamelizingatia sana. Leo tunazungumzia nguvu ya kiuchumi ya kichina. Walianza mwaka 1978. Leo hii wameanza kutoa *indicator* kwa nchi kama Marekani ambayo ina uchumi mkubwa katika dunia hii kwa sababu ya kujali kuwawezesha wananchi wake. Kwa hiyo, kwetu sisi hili lazima

tuzingatie, ama sivyo tutakuwa tunapitisha sheria hapa, tunawapitishia wenzetu na siyo Watanzania. Sisi tunabaki kuwa watazamaji tu. Kwa kweli itakuwa haina maana hata kidogo!

Sasa kwa sababu chama kimeshatamka kwamba lazima tujenge mazingira mazuri yatakayomwezesha mwananchi kushiriki kikamilifu katika uchumi. Tunaziomba Serikali zetu mbili kama ilivyosemwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar iende ikaandae utaratibu mzuri utakaowawezesha Watanzania wenyewe kushiriki kikamilifu katika hii *PPP*, ama sivyo, siku zote sisi kazi yetu itakuwa ni kupiga kelele tu. Kazi yetu itakuwa kuja hapa na kutengeneza sheria ambayo haitatusaidia hata kidogo. Kwa maana hiyo, bado tutaendelea ku-*generate* (kutengeneza) maskini katika Tanzania badala ya kutengeneza Taifa lenye watu wenyewe uwezo, Taifa lenye watu wenyewe ustawi.

Mheshimiwa Spika, nchi inajengwa na wananchi wenyewe. Nchi haijengwi na wageni. Walio wengi wanakuja hapa kupata manufaa tu, na itakapofika mahali akiona ameshatunyonya, amefaidika, anafunga virago vyake, huyo, anaondoka! Haya tunayaona.

Juzi tu tulikuwa na Zain hapa, inabadilisha jina hivi hivi kienyeji tu. Tunawauliza, sisi ndiyo wenyewe *share*, mnabadilisha, *share* yetu hiyo inakwenda wapi ama tutakuwa katika mazingira gani?

Mheshimiwa Spika, sasa mambo kama haya lazima tuwe macho ili Watanzania tushiriki kikamilifu katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, nisingependa nipigiwe kengele, lakini naliomba hilo Serikali yetu ilizingatie ili na sisi wenyewe tushiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia Muswada huu wa *Public Private Partnership*.

Mheshimiwa Spika, naomba kabla suaanza, ili kuweka *record* sawa kwa wananchi na pia wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam, imesemekana kwamba sigombe Ubunge kabisa. Lakini naomba kuwatangazia wananchi kwamba bado nitagombea Ubunge kuitia Viti Maalum vya *NGO*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona ni vyema nijikite upande wa *NGO* kutokana na utalaam wangu, kutokana na uzoefu niliuopata kwa miaka 15 katika Bunge na Serikali. Kwa sasa naona naweza zaidi ku-narrow au kujikita katika utalaam kwa kusimamia masuala ya wanawake kwa upande huo wa *NGO*. Kwa hiyo, waandishi wa habari naomba mseme namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nichangie hoja hii ya Muswada uliopo mbele yetu. Kwanza, tunaipongeza sana Serikali kwa kuleta huu

Muswada hapa Bungeni kwa sababu tunaona nchi nyingi ambazo zimeendelea zimesaidiwa sana na Muswada kama huu au *Public Private Partnership*.

Ni vigumu kwa Serikali yenye kuleta maendeleo inavyotaka kutokana na sera zinaweza zikawabana hapa kwamba msifanye biashara hapa na mambo mengine. Vile vile ni vigumu kwa *private* wenye kufanya au kufanikisha kutokana na vikwazo mbalimbali ambavyo wanavipitia vinavyohitaji Serikali.

Mheshimiwa Spika, vikwazo vingi vinawapata sana watu mbalimbali nikianza na mambo na fedha, miundombinu, maeneo ya kufanya biashara zao utaalam na mambo mengine ambayo nitayasema mbele. Lakini kwa kutumia Muswada huu, naona yote yameainishwa kuacha vipengele ambavyo nitapenda nivitaje hapa vile vile. Kwa upande wa *Public* wanaambiwa kwamba watatambua miradi, watafanya tathimini, wataweka hizo sera nzuri na mambo haya kama ya kodi, leseni ambayo ni *legal and regulatory frame work* na *private* wamepewa kazi kubwa zaidi ambayo ndipo ugumu ulipo. Wameambiwa watashughulikia ile *feasibility study* ambayo ni mchanganuo, wata-modernize au watakusanya ile kutafuta fedha na mambo mbalimbali, na utaalam pia watauleta wao.

Mheshimiwa Spika, kitengo maalum kilichowekwa chini ya *TIC* katika Muswada huu naona kisheria hakikupewa neno ama hakikupewa nguvu ya kutosha. Wameainisha vizuri sana mambo yatakayofaywa, kilimo, mifugo, uvuvi, umwagiliaji hata miundombinu ambayo pia ni suala kubwa linalosaidia maendeleo. Lakini pale kwenye meno lirukie moja kwa moja, kwa mfano matatizo haya na/au nione Muswada unalenga kudhibiti yale yaliyokwishatokea kuangalia kwamba kweli wamesema fedha wanazotumia wakati labda wanapoungana watu binafsi pamoja na Serikali, au/na Mashirika ya Kiserikali.

Lakini ningeshauri ili sheria ifanikiwe, kitengo hiki kiweze kupewa meno kwa mfano upande wa kilimo ambao wametaja, wapewe kisheria kwamba wana uwezo wa kusema tunataka hili eneo fulani, litafaa kwasababu ndio wanaobuni miradi, litafaa katika labda kulima kahawa, kulima chai, kulima pamba na kisheria waweze kutwaa hayo mapori ambayo yanatumika visivyo. Miundombinu waruhusiwe kisheria kutoa rai kwa Serikali au kutazama wapi fedha zinaweza kupatikana kupeleka miundombinu katika maeneo ambayo wataainisha kwamba haya yanaffaa kuweza kuweka wawekezaji. Vile vile kwenye kuajiri wataalam kisheria vile vile waruhusiwe na pia wasaidiwe wataalam watakapoletwa hapa nchini wasipewe vikwazo mbali mbali kama inavyotokea hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, vile vile wasaidiwe. Nikisema wasaidiwe nina maana wanawenza wakapewa fedha kusaidia kuandika hata mchanganuo ili kuwawezesha wale watu waweze kufanya biashara. Nitoe mfano wa nchi ya Malyasia, kule kuna kitengo kinaitwa Malasia *Industrial Development Authority*.

Mheshimiwa Spika, samahani naongelea viwanda kwasababu ndiko niliko au ndiko fani yangu, lakini wale wanaopewa kisheria uwezo wa kuweza kupata maeneo, uwezo wa kuweza kumsaidia mwekezaji kuandikisha mradi, uwezo wa kumsaidia

mwekezaji kupata masoko uwezo wa kumsaidia mwekezaji hata kupata fedha. Kwenye sheria hii naona vitu hivyo havionekani kwa uwazi.

Mheshimiwa Spika, tumeona vile vile kwamba sheria hii itashughulikia hayo mambo kwa upande wa *Public* ya *legal and regulatory frame work* ambayo inaonesha mambo kama ya kodi, uandikishwaji wa kampuni, vibali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sheria haikuonyesha wazi: Je, kama wale wanaohusika hawatafanya hivyo wataadhibiwa namna gani? Kwasababu ukitazama katika nchi yetu ile *mind set* yetu bado kasoro ndogo ya kuwajibika au kuna kasoro ambayo inaonyesha watu wamekaa kama kukwamisha vitu, tutafanyaje ili tuweze kufanikisha haya? Tuweke wazi kabisa katika sheria kwamba wewe unayehusika katika *desk* lako kama utakwamisha miradi ya Serikali au ya *Private* utapewa adhabu gani, ikibidi kuwaondoa na kuleta watu wapya tuaondoe iwekwe wazi tuwafundishe watu jinsi ya kufanya haya mambo, sioni mahali pa kuwafundisha watu hawa, tumechukulia kwamba watu wanaelewa na wanaweza wakafanya haya mambo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niseme kwamba sheria iongeze kipengele kwamba katika biashara au katika ubia huu wa Serikali na *Private* na *Public* pale ambapo tunaona amekuja mbia kutoka nje, Serikali ipo na itashirikiana. Kwa mfano, tulipochukua Kampuni ya simu au reli Serikali pale ndani tumeona haiwezi kujikita au kusimamia yenye. Kama Serikali, tuweke Watanzania kwa hiyo, kuwepo kwa mbia kutoka nje awepo Mtanzania na vilevile iwepo kampuni ya *Public*, hapo nina hakika kabisa kwamba tutaweza kuongeza na kudhibidi maslahi yetu na vilevile tutaweza kuhakikisha kwamba ile miradi inaendelea kwa uzuri.

Naomba nimalizie kwa kuwashukuru tena wananchi wa Jimbo la Kawe kwa msaada walionipa nimewaaga na nitawaaga tena kwa sababu kesho Bunge linavunjwa, nitaendelea kuwa Dar es Salaam na Mungu akipenda nitakuwa Mbunge wa wanawake kupitia *NGO* na wanawake wakiamua kuridhia kunipitisha na ninaahidi kuwa nitafanya kazi na wananchi wa Jimbo la Kawe na wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofit*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rita Mlaki na ninakutakia heri katika azma yako hiyo mpya. Ni jambo zuri tu tusipoteze uzoefu. Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na baada yake atakuwa ni Mheshimiwa Anastazia Wambura na wakati huo ajiandae Dr. Chrisant Mzindakaya.

MHE. DR. JUMA A. NGASONGWA: Mheshimiwa Spika, juzi nilipokuwa ninachangia Muswada huu, juzi ile nilipokuwa nachangia Muswada ulioletwa na Waziri au Bajeti ya Waziri wa Fedha na Uchumi nilikuwa na mambo matatu, mojawapo lilikuwa *PPP* lakini kwa bahati mbaya sikuweza kuchangia, leo ndiyo nimepata fursa, ninakushukuru sana. Vilevile ninakupongeza kwa kupata ofisi yako na nina hakika litakuwa la kiwango na kasi. Lakini vilevile na mimi nichukue fursa hii kukushukuru kwa

kazi nzuri uliyoifanya kwa muda wote huu wa miaka mitano katika kuliendesha Bunge hili. Umefanya kazi nzuri sana wewe na Naibu wako na ma-chairmen wetu wote wale ambao walikuwa wanakusaidia katika fursa hii.

Mheshimiwa Spika, lakini na mimi niungane na wenzangu hapa kuwashukuru wapigakura wangu wa Ulanga Magharibi ambao tumefanya nao kazi pamoja vizuri katika miaka mitano hii na nina hakika watanipa tena fursa nyingine ili niweze kuwahudumia. Ingawa nina nywele nyeupe nyingi, lakini siyo mzee na kama mtu anabisha, basi akamwulize Mama Ngasongwa atamweleza vizuri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mzuri sana na umekuja ingawa umechelewa, lakini wakati muafaka kwasababu umefika na malengo yake ni mazuri sana. Kwanza ni kusaidia kuhamasisha uwekezaji ndani ya nchi yetu na hili ni jambo zuri. Unajua hapa tunabishana na Serikali kuhusu ujenzi wa miundombinu. Duniani kote Miundombinu inajengwa na *private sector* kwa kutumia *Road toll*, leo ukienda Bangkok unawenza kwenda *Air port* unapita kwenye *fly over* mpaka ndani ndani ya mji kabisa Hotelini kwako na ile ni *owned by private sector*. Hali kadhalika ukienda Japan utakuta hivyo hivyo, kwa hiyo, suala hili la ubia ni zuri na tulifanyie kazi vizuri. Isipokuwa mimi nina tatizo la *structures*.

Nilipokuwa zamani nafundisha, kulikuwa na mwalimu mmoja sasa ni Marehemu Gilbert Gwassa yeye *critic* yake ilikuwa ni kubwa katika *structures* na akawaita watu wanaopenda sana *structures* kama *structureristics* kwasababu ya kupenda *structures*. Nadhani *structure* kwa maoni yangu ina mambo mawili moja ni *political* ili ifike shabaha za kisiasa maana *structure* haiwi hivi hivi tu, lazima iwe na malengo ya kisiasa. La pili ni *technical* ili kufanikisha mambo yaende vizuri. Sasa hili la kufanya *University band* ili kuifanya kuwa *responsibility* ya Waziri Mkuu ni *constrain*. Kwasababu Waziri Mkuu ana mambo mengi sana. Rafiki yangu Marmo huwa tunazungumza sana mara kwa mara ni *constrain* wa Serikali.

Pili, mratibu wa mambo ya Bunge kwasababu kwanza yeye ndiyo Mratibu halafu aende Jimboni kwake na kadhalika, halafu mwenyewe *background* yake siyo mchumi, ni *lawyer*, *I have respect to lawyers*, mimi binti yangu mmoja ni Mwanasheria, siku zote anasema baba mimi ni *learned* kwasababu *professionally lawyers* wanajiita *Learned Brothers na Sisters*. Mimi nina *Ph.D* ya uchumi nzuri, hawaniiti *Learned* na mimi ninakubali kwasababu najua hili ndiyo eneo lao la *ki-profession*. Lakini ninasema, pale mlipowaweka hata *management* ina kuwa shida. Kwa hiyo, ninasema jambo hili la *structuring liangaliwe* hivyo na ndiyo maana wakati mwingine tulipokuwa Chuo Kikuu tunasema hata *planning* ina *serve politics* kwanza na *number two* ni *technical*.

Mheshimiwa Spika, unawenza kuweka *plan* mahali ambapo haina *effect and you don't see the effect* kwasababu imekaa mahali *wrong*. Maana *structure* lazima iwe na *objective*, kama hapana kuiweka vizuri unaitupa tu hapa inakuwa umeitupa tu. Halafu hii *TIC* pale kama alivyosema Mheshimiwa Rita Mlaki, pale mimi ninamuunga mkono kabisa lazima ipewe meno iwe na *responsibility* ya kufanya na kujitegemea tena siyo *coordinator* angekuwa labda *Deputy Executive Director* kama siyo *Director* mwenyewe

katika Wizara ya Serikali ya kujitegemea kabisa anafanya mambo yake mwenyewe sasa pale *TIC*, pale mimi ninawapenda sana vijana wale lakini ninafikiri kuna matatizo, wakati wa Mzee pale Spika ilikuwa trauma kabisa *to be honest* ndiyo maana mmeanzisha *Investors Complains Bureau* sasa mnaipeleka na yenye huku huku tena mimi ninadhani *is misplaced*.

Mheshimiwa Spika, halafu ibara ya tano ya sheria ina-*define* mambo mengi ya *responsibilities and roles* ya hii *unit*. Kazi ambazo mimi ninashangaa, hii *capacity* wataipata lini ya kuweza kufanya mambo yote haya? Kwa mfano, wale wa akinamimi ninafanya kazi wakati mwengine na Wakorea wanataka ku-*invest Dar es salaam Water Front*, wanataka ku-*invest* Dar es salaam *International Airport* ile ya Bagamoyo na Mbegani na wanaomba hii *request for proposal* miaka miwili sasa hawapati.

Sasa sijui pale mtapeleka *unit* ndiyo mpate hii na kuitengeneza kwasababu *serious investor* mwenye *project* kubwa hawezi kuanza jambo hili bila kupata *request for proposal* kwasababu hii ndiyo *key to him*, kwasababu hii ndiyo inaonyesha Serikali inaunga mkono ule mradi na ana ushahidi wa namna hiyo. Miradi mikubwa kama hii mtu hawezi ku-*invest* bila kujuwa kwamba atapata faida, *its not possible!*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa ninaomba, hii Sheria ni nzuri sana lakini *the way it is arranged*, siamini kama itakuwa na *effect* itakuwa *bogged down* katika *bureau class* ya Serikali na mwisho wake hatutafaidi sawasawa. Kwasababu *private sector* ni muhimu sana sasa katika kuendeleza Taifa letu. Yule Ali Mfuruku, yule *CEO* wa *INFO- TECH* siku moja nimemwona kwenye *Television* akisema nyinyi watu wa Serikali ni watu wa ajabu sana, hamtupi fursa sawasawa sisi na kutuundia mazingira mazuri ya kuweza kufanya *investment* na mtutume sisi *private sector* siyo nyinyi Serikali.

Mimi ninakubaliana naye kwamba *private sector* ndiyo watumwe kufanya mambo haya, siyo sisi. Sisi Serikali hatuna *capacity* hiyo, halafu *traditionally* Serikali ni *Bureaucratic* katika biashara. *Bureaucracy* inaharibu utekelezaji kwasababu *bureaucracy* haizingatii faida, kumbe *key element* katika *private sector* ni *profit making*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hili naomba litazamwe vizuri na ninafikiri kuwa lizingatiwe ipasavyo. Baada ya kusema haya, naona kengele ya pili karibu itagonga, naomba nikushukuru sana na nikutakie kila heri katika uchaguzi ujao na wewe ushinde na uendelee kuwa Spika. Ahsante sana.

SPIKA: Ninakushukuru sana Dr. Ngasongwa kwa kunitakia heri. Ninahitaji salamu za namna hiyo nyingi tu. (*Kicheko*)

Waheshimiwa tunaendelea na ninamwita sasa Mheshimiwa Anastazia Wambura, dakika kumi na tutamalizia na Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya ambaye yeze kwa kuwa leo anatuaga amepewa dakika kumi na tano.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mema yote ambayo

amenijalia mimi, lakini pamoja na Bunge letu Tukufu kwa kweli ametuwezesha kufikia salama kipindi hiki cha miaka mitano. Lakini vilevile kwa namna ya pekee ameiwezesha nchi yetu kuwa katika hali ya amani hadi sasa. Kwa hiyo, ninaendelea kumwomba aweze kudumisha hali ya amani na hivyo tufanye uchaguzi wetu mkuu katika hali ya amani. Kwa hiyo, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, nichukue nafasi hii kukupongeza wewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wetu watatu kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa hali ya kasi na viwango. Kwa wananchi wa Majimbo, Jimbo la Urambo na Jimbo la Mheshimiwa Naibu Spika na Majimbo yote ya Wenyeviti nawaomba wananchi hawa wasijaribu kuchezza shilingi chooni kwa kuwapoteza Waheshimiwa Wabunge hawa. Ninaomba wawarudishe na wawape ushindi wa kishindo kabisa kwasababu wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na shukrani nyingine ninapenda nichukue nafasi hii kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Kikwete kwa kupitishwa kwa kishindo kikubwa katika Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi uliofanyika siku chache zilizopitana, hivyo kumpitisha kuwa mgombea Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi, kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 2010.

Napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Dr. Shein kwa kuwa Mgombea Urais wa Zanzibar na vilevile Dr. Bilali kwa kuwa mgombea mwenza. Ninazo shukrani nyingi sana, lakini ninaona niziseme mwishoni baada ya kuwa nimechangia kidogo kwenye Muswada huu wa *PPP* 2010.

Mheshimiwa Spika, nina maeneo mawili tu ya kuchangia, eneo la kwanza ni sehemu ya pili kifungu cha 4 (1) ambacho kinasema: “*There is an establishment of coordination unit within The Tanzania Investment Centre to be an integral part of the centre.*” Nimekuwa nikijiuliza kwamba hiki ni chombo muhimu na kimekuwa kikitajwa katika maeneo mbalimbali ya kitabu hiki cha Muswada, lakini tofauti na Miswada mingine ambayo tumekuwa tukionta, tumeona vyombo mbalimbali kwa mfano Bodii vikiwa vimeonyeshwa kwamba vitakuwepo, tunaona kwamba kuna *composition* ya hivyo vyombo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na vilevile tunaona kuna vigezo vya kuchaguliwa wale watu ambao watakuwepo kwenye hicho chombo, lakini sasa katika hii sehemu sijaona kwamba hiki chombo *composition* yake ni ipi na vilevile vigezo vya wale ambao watakuwemo katika hicho chombo. Kwa hiyo, ningependa pengine tupate ufanuzi wakati Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho na Kifungu cha 4 (3) katika sehemu hiyo ya pili.

Kwanza ningependa ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Kwa hiyo, nitagusia zile Wizara ambazo tunafanya nazo kazi katika eneo hili, lakini kabla sijazizungumzia hizo, ninaona kuna upungufu kidogo kwani *sector* ya Maendeleo ya Jamii haijaonekana hapa, tunaambiwa kwamba *this is not limited to the following sectors*, lakini ningependekeza hiyo *sector* ya Maendeleo ya

Jamii ingeonekana hapa ingekuwa vizuri ili kuwa- *encourage* wale ambao wako *interested* na *sector* ya Jamii ili waweze kuingia *partnership* na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la nyumba na maendeleo ya makazi, mazingira na masuala ya utalii zinasimamiwa na Wizara ambazo ziko chini ya Kamati yetu. Ningependa kuwaomba sana Waheshimiwa Mawaziri, nina imani kubwa kuwa watarudi na wataendelea kushika Wizara hizo wachangamkie sana kwasababu changamoto ziko nyingi na zina maeneo mapana. Kwa hiyo, wachangamkie sana wabia ili kusudi waweze kuwa na ufanisi katika utendaji wa Wizara zao. Kwa kweli ninawapongeza sana kwa kazi wanazozifanya, ni nzuri, lakini wanafanya kazi katika hali ya *pressure*, kubwa kwa hiyo, naomba wananchi wa Majimbo yao waweze kuwarudisha kwa kishindo kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kutoa shukrani zangu, niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu mzuri, kwa kweli unaonyesha kwamba Serikali ina nia kubwa sana ya kuleta maendeleo makubwa katika nchi yetu, kwa hiyo, imeweza kuona kwamba inahitaji msaada mkubwa zaidi katika *private sector* ili kusudi iweze kufanya kazi katika hali ya ufanisi na hivyo kuwakomboa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nitoe shukrani zangu za pekee kwa akina mama wanawake wa Mkoa wa Mtwara kwa kunipa ridhaa ya kuwawakilisha katika Bunge hili kwa miaka mitano, kazi zao kwa miaka mitano walinipa kura zao na niwashukuru sana. Lakini kwa namna ya pekee ninapenda kuwashukuru kwa kunitia moyo kwa kunihimiza ili kusudi niweze kuchukua fomu na kunihimiza, huku wamefanya kwa kunichangia mchango wa kuchukulia fomu. Kwa hiyo, nasema ahsante sana akina mama wa Nanyumbu, akina mama wa Newala, akina mama wa Masasi, Mtwara vijijini, Tandahimba pamoja na Mtwara mjini, mchango wao ninauthamini sana na ninasema sitawaangusha. Nitachukua fomu hiyo tarehe 19, ahsante sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru familia yangu, mume wangu mpendwa, wanangu, ndugu, jamaa na marafiki kwa kunitia moyo wakati wote na kuwa msaada mkubwa kwangu katika utendaji wangu wa kazi. Lakini kwa namna ya pekee naishukuru au ninakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kikamilifu na mfano tumeuona jana ambapo tume-sign, Wizara ya Maji na Umwagiliaji ime-sign Mkataba wa Maji wa Masasi – Nachingwea jana tarehe 14. Kwa hiyo, ninasema ahsante sana na kwa niaba ya wanawake wa Masasi ninashukuru sana kwa Serikali kuwajali, kuwapunguzia adha ya kutafuta maji katika maeneo ya mbali na hivyo kupoteza muda mwangi wa shughuli za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwatachia kila la kheri Wabunge wote katika kipindi hiki kigumu cha uchaguzi, niitakie nchi yetu hali ya utulivu na amani na Mwenyezi Mungu atujalie ili tuweze kurudi sote katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Anastazia Wambura. Mimi pia nakutakia kheri katika azma ya kurejea Bungeni, bila shaka akina mama wa Mtwara wameshasikia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa mwisho kwa hoja hii ya *PPP* upande wa Wabunge si mwininge bali ni Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, huyu amekwishatangaza kwamba hagombe tena Ubunge, baadhi yetu tumesikitika sana lakini maamuzi haya kila mtu ana maamuzi yake. Tutakuwa mbali kidogo na hekima zake na uzoefu wake mkubwa wa miaka 45 ndani ya Bunge hili, kwa maana hiyo kwa kutumia Kanuni ya Tano Mheshimiwa Job Ndugai aliamua kwamba yeze atakapochangia pamoja na kuwa tulitenga Kanuni Mheshimiwa huyu kwa sababu anatuaga basi yeze apewe dakika kumi na tano. Kwa msingi huo sasa namwita Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. (*Makofi*)

MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA: Mheshimiwa Spika wa Bunge letu, Mheshimiwa Samuel Sitta, kwa jina la Mwenyezi Mungu nakushukuru sana kwa kuniruhusu sasa kuzungumza wakati huu. Pia nashukuru kwa kunipa upendeleo chini ya mamlaka uliyopewa na Kanuni umeongeza dakika ziwe kumi na tano. Nakuthibitishia nitazitumia vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa sababu ulipoingia katika Bunge letu hili ultangaza kwamba utaendesha Bunge hili kwa viwango na *speed*. Mimi nimekuwa Mbunge hapa muda mrefu na nimeshuhudia kwamba kwa kweli umeitekeleza ahadi yako, hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nataka nikupe sifa nyingine kubwa ambayo watu wengi wanaitafuta na hawaipati, nayo ni upendo. Upendo ni kitu cha bure, haununuliwi, wewe umeutoa umeuonesha upendo kwa Wabunge wote wala hukutubagua. Ulijitahidi kutetea maslahi ya Wabunge na ninashukuru kwamba Rais mara zote kwa kukuhestimu na Rais pia kutupenda amekuwa akikubali yale unayomshauri, hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimeshuhudia vilevile kwamba wewe ndiye ulikuwa Mwenyekiti wa *CPA* na Mkutano huu ulifanyika katika historia ya nchi yetu, ulifanyika katika Mkoa wa Arusha. Bunge letu lilifanya vizuri kwa sababu Wajumbe waliohuduria kwa idadi hawajawahi kufikia idadi ile katika nchi yeoyote katika Bara la Afrika au nchi yoyote wanakohuduria. Tulitoka na sifa kubwa wewe mwenyewe na Serikali yetu chini ya uongozi wa Rais wetu. Ahsante sana, hongera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Anna Makinda, mimi namfahamu miaka mingi tumefanya kazi pamoja. Mwaka 1975 Mheshimiwa Anna Makinda alipokuja kugombea mimi nilikuwa *campaigner* wake wakati ule na ninafurahia kwamba ameendelea kuchunga heshima ya Bunge na ni mwanamke mionganoni mwa wanawake wanaoheshimiwa ndani ya Bunge hili hongera sana mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Wenye viti wote watatu, ni vijana lakini wameonesha umahiri mkubwa sana. Jambo ambalo nataka niliseme hapa wazi wazi, tangu Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda alipoteuliwa kuwa Waziri Mkuu tumeshuhudia mshikamano wake yeze na uhusiano wenu ambao umeleta utulivu mkubwa sana ndani ya Bunge letu, upendo umeongezeka na watu tumeheshimiana, kwa sababu ninyi ndiyo mnaotuongozza mkiwa kitu kimoja sisi hatuwezi kuwa na matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi namfahamu Mheshimiwa Mizengo Pinda miaka mingi sitaki kusema sana kwa sababu anatoka Mkoa ninakotoka, lakini nataka niwathibitishie kwamba nimemfahamu Mheshimiwa Pinda toka mwaka 1975 alipomaliza Chuo Kikuu na mionganoni mwa watu waliotulia kikazi, tena kwa heshima na mafanikio makubwa sana pale Ikulu. Amefanya kazi na Marais wote mpaka alipokuja hapa kuwa Mbunge na Naibu Waziri na kule kwetu Rukwa tunamheshimu sana, ndiyo maana mimi suala la kung'atuka au kuamua kuachia Ubunge si mara yangu ya kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa Mkoa wa Rukwa kwa miaka kumi na tano, nikaacha mwenyewe wala sikuondolewa na yeze ndiye akawa Mjumbe wa Halmashauri Kuu, Wabunge tutafurahi pia kufahamu kwamba mimi nilikuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa nikaamua kugombea Ubunge baada ya kuombwa na wananchi. Nikamwandikia Rais anikubalie kugombea, alinikubalia kwa maandishi yanayosema hivi; "Tunakubali ukagombee Ubunge lakini mambo ya kutokuendelea kuwa Mkuu wa Mkoa utuachie baada ya Uchaguzi." (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Rais huyu alikuwa anaondoka baada ya Rais mwingine kuchaguliwa, ambaye alikuwa Rais Benjamin Mkapa, mimi nilimfuata Rais Mkapa kabla hajaapisha Baraza la Mawaziri, wala kuteua Wakuu wa Mkoa, nikamwambia nimekuja kukueleza nimeshaandika barua ya kuacha ukuu wa Mkoa na utakapokuwa unafikiria watu wa kuwapa madaraka mimi usinifiki kwa madaraka yoyote, nakwenda kulima, kwa hiyo, hii ni tabia yangu ya kuondoka mwenyewe katika madaraka, na ninadhani ni jambo zuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ubunge, mimi nimeingia Bunge mwaka 1965 nikiwa na umri wa miaka 25 na sasa naondoka nikiwa na miaka 70 kwa hiyo nina umri mkubwa kuliko nilivyoanza kazi ya Ubunge au siasa. Nimekuwa Naibu Waziri miaka tisa, Wizara moja ya Viwanda na Biashara, Mkuu wa Mkoa zaidi ya miaka 13 na sasa natimiza miaka 44 itakapofika mwezi Oktoba.

Mheshimiwa Spika, kwa maneno hayo na nafasi hizo nilizopewa nimshukuru Mungu wangu kwamba ameniwezesha kufika hapa tulipofika, nimshukuru pia baba na mama yangu walionizaa na kunilea, utakumbuka siku moja nilisema hapa watu wakacheke, nilisema mimi namshukuru Mungu kwamba amenijalia kunipa akili inayonitosha kuishi duniani, hiyo ni kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka kusema jambo moja lililonisaidia kufanikiwa katika maisha yangu, mimi sijapata kushirikiana kufanya kazi na mtu ambaye ana akili kidogo,

hapana hata siku moja! Mimi nafanya kazi na watu wenye akili kunishinda na uwezo zaidi ama tunaolingana. Sasa ukifanya kazi na mtu mjinga atakupotosha, madikteta ndiyo wana tabia ya kufanya kazi na watu wasio na akili sawa. Anataka awagandamize na wampepetee, hiyo ni tabia ya madikteta. Mimi sijawahi kufanya hivyo ndiyo maana nimefanikiwa. Marafiki zangu miaka yote wamekuwa watu wakubwa kwa umri ili wanisaidie katika maisha hapa na wamenifikisha hapa nilipofika.

Mheshimiwa Spika, juzi ulitoa sifa nyingi sana juu yangu wakati napewa Udaktari (Digrii ya Hshima), nakushukuru kwa maneno yote uliyoyasema. Wabunge wengi mlikuja kuniunga mkono nawashukuru Mungu awabariki na wale ambao hawakuja pia mlisema kwa nini hamkuja naomba Mungu awabariki kwa upendo wenu kwangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maneno uliyoyasema siku ile na hata waliokuja kunipa shahada, mimi nilisema sifa ninayopewa, hupewa mtu aliyefariki, lakini nashukuru kwamba nilipewa sifa hizi bado nikiwa hai nasikia mwenyewe. Kwa hiyo, nataka nikushukuru rasmi Bungeni ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe ushauri kwa wenzangu mtakaojaliwa kurudi Bungeni na ninajua mtarudi Bungeni. Nimeshuhudia mwenyewe Urambo unarudi kuwa Mbunge kule Urambo nimeona watu wanakupenda tumeona wenyewe, na mimi nakuombea wakuchague, ile ofisi uliyojenga hukujenga ya Sitta umejenga ya Mbunge wala siyo ya Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mbunge yejote atakayekuja kuchaguliwa baada yake aweke historia na kukumbuka kwa kazi nzuri tulioiona, watu wachache wenye uwezo hufanya mambo ya kesho siyo ya leo, wewe umefanya jambo hili la kesho hata kwa Mbunge ajaye. Nashauri kwamba Bunge lijalo lifanyeni kuwa Bunge la uchumi. Njooni mhangaika na uchumi wa nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sifa ya siasa Watanzania kuwa na siasa tunayo tangu wakati wa Nyerere lakini bado tegemezi. Sifa hii ihamie kwenye uchumi sasa maana yake kama ni siasa tunasifiwa dunia nzima kwamba Tanzania ni nchi ya utulivu, Tanzania ina amani, watu wazuri, lakini mimi nadhani hayo yanatosha kuwa msingi wa kuhamia kwenye uchumi sasa. Rasilimali tulionayo sisi inatusuta tunaposaidiwa na nchi kama Waholanzi. Waliochota bahari wakaifanya ardhi ili walime. Sisi tuna mali zote, vitu vyote alivyotaka Mwenyezi Mungu viwepo duniani kumsaidia binadamu sisi Tanzania vyote tunavyo hakuna tulichopungukiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitakupwa mfano mmoja, Mama yangu Mheshimiwa Anne Makinda ni shahidi, Mwalimu Nyerere aliponipa Ukuu wa Mkao Morogoro alinipa *mission* akasema nenda kaongeze kilimo, tukafanya mpango tukaanza kilimo, siku moja Mwalimu amepita tuko naye ndani ya gari aina ya *Benz*, tumefika pale mvua imenesha na majani yameota sana pale Dakawa akasema Chrisant unaona Marais wenzangu wanagombana ukame, mimi nagombana na rutuba ambayo haina maana, kabla siaondoka nilimpeleka Mwalimu Nyerere akaenda akakuta shamba la wananchi kila mtu

na ekari zake zaidi ya ekari 60,000 ndani ya kile Kijiji, nikamwambia Mwalimu tulipofika hapa ukasema unagombana na mbolea angalia akacheka na akafurahi sana. Kwa hiyo, hakuna kisichowezekana.

Mheshimiwa Spika, nilifanya mpango nikapata trekta mwenyewe Mkuu wa Mkoa siyo za Wizara kutoka *FAO* Ulaya zinakuja moja kwa moja na Mheshimiwa Anne Makinda ndiye alikuja kufungua mradi, na Kigoma hivyo hivyo, na Mikoa yangu hakuna mtu aliyekwenda Wizarani kutafuta ardhi ya kumiliki, wakuu wangu wa idara na mabwana ardhi ndiyo wanakwenda kuwaletea wakulima hati, leo kupata hati alime ni kama kwenda mbinguni, haiwezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Bunge lijalo tumieni sheria hii kuzuia nafasi kati ya matajiri na maskini, kwa sababu nchi hii sasa ina watu kumi tu ndiyo matajiri wa kupindukia na utajiri wote wa nchi hii hao ndiyo wanagawana baada ya Bajeti. Nilisema mara moja hapa ujamaa utakaokuja katika nchi hii utakuwa wa kuumizana, kwa sababu sisi tutasomesha watoto watakwendwa *University* watamaliza madarasa, hawana kazi watakwendwa wapi wakati watu wachache wanamiliki utajiri. Mtapona? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka 15 watakaoiondoa CCM madarakani ni hawa tunaowasomesha, hizi shule za Kata na Sekondari ndiyo moto, kwa sababu hawawezi kusoma bila kazi. Wana ardhi nzuri, kinachotakiwa ni mipango tupangane, hangaikeni kujenga kada ya kati ya uchumi, na kada ya chini ya watu wadogo watakaokula na kushiba na kusaza, hawa wakubwa msihangaike nao inatosha, rudini kwa hao watu wadogo Bunge lijalo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kazi ya kusomesha faida yake ndiyo hiyo, watajua namna ya kutumia mbolea, namna ya kutumia dawa, sasa tatizo litakwisha, rudisheni mawazo na uwezo wenu wote wa uchumi kwa watu wadogo. Hawa wakubwa watahangaike wenyewe, sheria isaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho mimi si kama naaga kwamba naondoka katika siasa, naondoka tu Bungeni, lakini naondoka Bungeni bado nina akili na uwezo wala siondoki kwa uzee. Naondoka kwa sababu nimetumikia hii nchi imetosha. Lakini akili yangu sasa ni nyingi na nzuri kuliko za mwanzo na afya yangu ni kama mnavyoiona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka na mimi nitoke niwe mzee naweza kufoka watu wakanisikiliza, kuliko kusukumwa, mimi naondoka watu wananipenda Jimboni kwangu ningegombea ningerudi Bungeni bila matatizo, lakini nataka niondoke bado watu wananipenda na Bungeni mnaniheshimu bado, ili siku moja nikirudi hata mkisikia nimesemwa kwenye redio mseme yule Mzee siyo Juha, hana akili. Kwa hiyo, nataka niondoke kwa upendo na amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile mimi sitaki migawanyiko ya siku hizi, pia sipo tayari kwenda kutafuta Ubunge kwa pesa, haiwezekani nilishaapa. Nililelewa na Nyerere, tulikuwa tunaingia kwenye gari mnatembezwa wote sawa, kila mtu haki sawa, leo mwenye pesa ndiyo atakuwa Mbunge na wasio na pesa hawatakuja kuwa watetezi wa nchi hii. Hizi taratibu zote mmeweka bado hazitoshi na vyama vyetu wajifunze ustaarabu,

Vyama vyetu vyote hakuna *CUF*, CCM wote tumetumbukia kwenye uchafu wa ovyo wa namna ya kupata viongozi, na jambo hili nalisema *from my heart*, siyo la kusema kwa unafiki. Mimi siwezi kwenda kuwapa Wajumbe...

Mheshimiwa Spika, mimi miaka mitano nimehenya natoa hela mfukoni kuchangia madarasa, halafu nikaanze kutoa shilingi 2,000/= kumpa Mjumbe anipe kura, siwezi. Hata shilingi 2,000/= nilikataa na watu wote waliona, nikasema sitaki Ubunge wenu niacheni niende kwetu wakasema Mzee rudi tutakupa kura. Kwa hiyo, nasema ahsante sana umetuenzi Wabunge wenzako na Wabunge wote ahsanteni sana kwa upendo wenu Mungu awabariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mliniheshimu sana, hakuna hoja nimewahi kuleta Bungeni ikarudi nyuma, kwa sababu ya imani, fanyeni utafiti, kila jambo mnalotaka kuleta Bungeni, ili mkiyaleta mambo Bungeni yaweze kwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba Mungu awabariki Wabunge wote na Bunge letu lidumu ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Dr. Chrisant Mzindakaya na kama kawaida yako wakati wote umekuwa ni muwazi na mkweli, hufichi hisia zako, wewe si mnafiki. (*Makofi*)

Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote nakutakia mafanikio katika shughuli ambazo unakwenda kuzifanya, baadhi ya Wabunge hapa watarudi na baadhi pengine hawatarudi, lakini sote kwa pamoja tutaendelea kukumbuka maneno yako. Uzuri wa maneno ya humu Bungeni yanaishi daima katika *Hansard* na hayapotei. Tunakushukuru sana sana. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kupitia ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuleta Muswada huu ambao kimsingi umekuja kwa kuchelewa. Hata hivyo, nina mambo machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uingiaji/usimamizi wa mikataba. Kwa bahati mbaya sana kati ya mikataba mingi ambayo nchi yetu imeingia hasa katika sekta za madini na mawasiliano, asilimia zaidi ya 70 ni mibovu na mibaya sana. Sasa pamoja na nia nzuri ya Serikali lakini kama usimamizi utakuwa mbaya, hatutapata faida ya kuwa na Muswada huu. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu ahakikishe kwamba mikataba yote inasimamiwa kwa ukaribu sana ili kuepuka kuingiza nchi yetu kwenye mikataba mibovu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18, 19 na 20 ya Muswada, kwa sehemu kubwa sana vimezungumia suala la kusaini makubaliano “*agreements*” wajibu wa “*Accounting Officer*” na marekebisho ya makubaliano. Wasiwasi wangu hapa ni matumizi ya neno makubaliano. Nashindwa kujua ni kipi kitakachoingia kwenye ubia ni makubaliano au mkataba? Je, makubaliano ni sawa na mkataba? Kwa maoni yangu, nadhani neno

mkataba ni zuri zaidi kwa sababu tunaingia mkataba zaidi kuliko makubaliano. Naomba ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada.

MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA: Mheshimiwa Spika, hongera sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watendaji, Muswada huu umekuja wakati muafaka. Napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi utatoa fursa ya kuipunguzia Serikali mzigoto wa kufanya kila kitu katika miradi ya maendeleo na utoaji huduma za jamii. Nimeona mifano mingi ya kuigwa hapa Tanzania na nje ya nchi mfano michache tu ya kuigwa ni kama Shirika la Damu ya Yesu Manyoni limechimba visima vya maji, linaiuzia Mamlaka ya Maji Manyoni na Mamlaka ya Maji inasambaza maji kwa wateja. Huko Vancouver, Canada nimeona mradi mkubwa wa kutoa huduma ya usafiri wa reli na mabasi unaoitwa *Trans – Link*. Mradi huu unachangiwa na Serikali na wawekezaji katika sekta ya usafiri na usafirishaji. Huko India katika Jimbo la Maharashtra, wawekezaji wanajenga barabara kadhaa halafu wanaruhusiwa kukusanya “*Road Toll*” barabarani. Kuna fursa za ubia katika miradi mikubwa ya maji na umwagiliaji. Mamlaka ya kuendeleza Bonde la Mto Rufiji (*RUBADA*), wanaangalia uwezekanano wa kuendesha mradi wa umwagiliaji kwa ubia katika Bonde la Mto Rufiji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ubia utaharakisha maendeleo ya Taifa na kuipunguzia mzigoto Serikali. Mheshimiwa Waziri ukiweza waambie wapiga kura wangu, Jimbo la Buyungu kuwa ubia ni jambo jema na tutaangalia tunavyoweza kutumia mfumo huu kujenga Wilaya yetu mpya ya Kakonko.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wa Sheria kwa kutuletea Muswada huu muhimu kwa maendeleo ya nchi. Ni kweli tumechelewa sana kuuleta maana shughuli nyingi zimekuwa zikishindikana kutekelezwa kutokana na uwezo mdogo wa Serikali yetu. Huu ni mwanzo mzuri sana, naunga mkono hoja hii kila hali.

Mheshimiwa Spika, suala la *PPP* lina uzuri wake lakini na athari zake kwa baadhi ya wananchi. Mfano, ni ule wa ujenzi wa barabara za kulipia au madaraja ya kulipia, je, katika mazingira hayo, Serikali itachukua tahadhari gani ili gharama za kutumia huduma hizo za kulipia zisiwe chanzo cha malalamiko kwa wenye uwezo mdogo wa kuzilipia au Serikali itakuwa tayari kutoa ruzuku kwa baadhi ya huduma?

Mheshimiwa Spika, mradi wa kujenga Mji Mpya wa Kigamboni ambao unaonekana kuwa utaihusu sana Serikali katika kuandaa mazingira sahihi ya kufanikisha azma hiyo. Je, Serikali katika mpango wa *PPP* licha ya kuwa na ubia wa *NSSF*, mpango upi unaoandaliwa kwa makampuni binafsi toka ndani na nje ili kwa pamoja waje kutumia fursa hii ya kuwekeza hapa nchini kwa mazingira mazuri na yenye manufaa kwa wananchi wetu?

Mheshimiwa Spika, ili kuwepo na mafanikio mazuri ya kuleta ufumbuzi wa kuondoa umaskini na kukuza uchumi, ni vizuri sasa Mheshimiwa Waziri aandae utaratibusi mzuri wa kuwawezesha wananchi wenyele ili waingie ubia na wawezeshaji kuliko Serikali kila mahali iwepo. Je, mpaka sasa ni maandalizi gani yamefanyika katika azma hii muhimu ili tusiendelee kuwa watazamaji?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wake wa Wizara, kwa kuandaa Muswada na kuuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu na Sheria hii, itaweza kutusaidia sana kama Taifa ikiwa tu tutakuwa na watendaji wa Serikali walio wazi, wa kweli na waaminifu kuleta mabadiliko na kusaidia Watanzania kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri pia tukajifunza kutoka nyuma kwani Tanzania tuliwahi kuwa na miradi ya ujenzi wa barabara za ubia kati ya Serikali na wawekezaji binafsi na miradi mingi ilishindwa. Ni muhimu tukajua kwa nini, tulishindwa wapi, tulikwama nini na hivyo kuweza kuijandaa vizuri kutekeleza Sheria hii kwa tija na maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza, Kifungu cha 2 kinasema Sheria hii itatumika Tanzania Bara, itakuwaje pale ambapo sekta binafsi zitaingia ubia na taasisi ambazo ni za Muungano?

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili, Kifungu cha 4(3) katika sekta zilizoanishwa, zipo sekta ambazo ni za Muungano ambazo Bara na Visiwani na nyingine ziko kwenye majadiliano ya kuingia kwenye Muungano mfano (*d*) *exploration and mining* na (*g*) *environment and waste management*. Sheria ni ya leo na kesho, hivyo tuingize vipengele ambavyo ni muhimu kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu, Kifungu cha 8 (1) na (2), kinaeleza majukumu ya Serikali na sekta binafsi katika kuendeleza miradi ya ubia. Suala la kufuatilia na kutathmini miradi hiyo ingekuwa ni wajibu wa Serikali ili kuhakikisha Taifa linanufaika na miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 8(2)(e), lazima Serikali ihakikishe tunatoa *Technical Expertise* wenye uwezo wa kutosha, wawe wawazi, wa kweli na wasije wakatumwiwa kunufaisha sekta binafsi kwa manufaa yao wenyele. Wawekezaji na sekta binafsi wao wanataka kutengeneza faida zaidi, sisi kama Taifa tuangalie wananchi wananufaika na miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, umakini mkubwa unahitajika sana, Watanzania wenye uwezo wapewe fursa ya kwanza kwenye miradi ya ubia. Suala la 10% ndilo linawaumiza

wananchi wenye uwezo kukosa nafasi muhimu kwenye miradi ya nchi yao. Tutangulize uzalendo mbele kwa kuinua Taifa letu.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa jinsi walivyoandaa Muswada huu na kuuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikataba, pamoja na hoja kuwa nzuri ya *partnership* kati ya Serikali na *private sector*, nashauri kuwa katika utekelezaji wote kuwe na umakini mkubwa katika utengenezaji wa mikataba. Hii itatusaidia kuepuka matatizo kama tuliyokumbana nayo katika mikataba ya madini.

Mheshimiwa Spika, umaskini wa Serikali, ni muhimu Serikali iwe makini katika kuchagua miradi ya kuingia katika ubia na wawekezaji binafsi. Ichague tu ile miradi yenye maslahi na faida kwa nchi.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji, Serikali itakuwa katika ubia au Shirika la Umma litakuwa katika ubia lazima kufuatilia ili yule mbia asije akafaidika kiziada kwa gharama ya Serikali au Shirika la Umma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ubia wa sekta binafsi katika miradi ya Serikali kupitia mikataba maalum ni mpango mzuri sana utakaosaidia kusukuma kwa kasi maendeleo ya nchi hii. Niseme tu mpango huu (MUSwada) huu umechelewa sana. Nchi nyingi za Mashariki ya mbali walifanya ubia huu na wote tunashuhudia maendeleo walifofikia.

Mheshimiwa Spika, jambo linalosikitisha, suala la uwezeshwaji wa wananchi halikupewa kipaumbele kabisa na kimsingi halipo kabisa. Hili ni tatizo kubwa sana. Katika Kifungu cha 14, kinachompa AG (Mwanasheria Mkuu), kufanya *vetting*. Suala la *vetting*, ni muhimu sana lakini wote tunajua shughuli nyingi alizonazo AG na ofisi yake kwa ujumla. Hivyo inawezekana kabisa ndani ya siku 14 awe hajapitia mikataba. Kwa mantiki hiyo kama AG hatatoa mawazo yake “*opinion*” ndani ya siku 14 na kama hakuna sababu iliyotolewa maana yake ni kwamba AG amekubaliana na mkataba huu. Suala la kujiuliza ni je, *AG office* ina watumishi wa kutosha? Bado haieleweki kwa upande wa ufanisi hasa upande wa Serikali kwani ni wazi kuwa utumishi Serikalini umekuwa wa kusuasua sana ukilinganisha na sekta binafsi, kumekuwa na tofauti kubwa sana katika utendaji kazi. Ni jinsi gani *gap* hii itafanyiwa kazi ili pawe na ufanisi katika ubia huu?

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite mtoa hoja ili aweze kuhitimisha huu mjadala.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja

iliyopo mbele yetu kwa kutoa majibu kwa hoja za Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni na wale waliochangia kwa maandishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, asubuhi nilikuwa nimetoa maelezo mrefu ikiwa ni pamoja na shukrani na pongezi kwa watu mbalimbali ikiwa ni pamoja na wewe na Ofisi yako, nisingependa kurejea yale ambayo nimeyasemea asubuhi, isipokuwa niende moja kwa moja kwenye hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kama desturi naomba niruhusu niwataje Wabunge wote waliochangia hoja hii kwa kuongea hapa Bungeni au kwa maandishi, nawatambua watu hawa lakini pia nawashukuru sana kwa wale ambao hawajachangia hapa pengine wamechangia kwenye semina na kwingineko, kukaa kimya kwao humu Bungeni bila shaka ni ishara kuwa wanaunga mkono Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia Muswada huu kwa kusema hapa Bungeni ni pamoja na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa *Engineer* Mohammed Habib Mnyaa, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, Mheshimiwa Devota Likokola, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Magalle Shibuda, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Anastazia Wambura na hatimaye hivi karibuni Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Godfrey Zambi na hatimaye Mheshimiwa Eustace Katagira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianzie pale ulipomalizia wewe mwenyewe kuhusu Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya. Watu wenyewe asili ya Mzindakaya si wengi sana katika nchi yetu, kwa kweli wanastahili sifa ambazo wanazipata. Kwa bahati mbaya sana mimi sikuwa Dodoma hapa siku ambapo alikuwa anapokea Shahada yake ya *Ph.D.* Kwa hiyo, naomba radhi iwapo nitarejea ambayo yamesemwa wakati huo. (*Makofi*)

Mimi napenda kusema inapofika wakati Bunge linafikia mwisho wake siyo Bunge la Tanzania tu lakini Mabunge mengi duniani kunakuwepo na Wabunge wanaostaa fu Ubunge ambao wamechangia nchi zao na Mabunge yao mambo mengi tu. Huwa wanapewa fursa ya kutoa hoja. Mara nydingi hoja hii inachukua muda mrefu na pengine hujadiliwa. Kwa hiyo, kwa maoni yangu muda umefika sasa kuangalia upya kanuni zetu ili watu wa aina ya Mzindakaya wanetuchotea busara zao hizi kwa kutoa hoja hapa na wangepewa muda mrefu tu na baadaye vizazi vijavyo visome kwenye *hansard* uzoefu wa watu kama hawa na kwamba walikuwepo, walitoa mchango mkubwa kwa mataifa yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mzindakaya tutamkumbuka sana kama ulivyosema kwa vile alikuwa mkweli daima alikuwa anatafiti kabla ya kusema. Alikuwa mshauri kwa Wabunge wageni.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmojawapo ambaye nimefaidi sana busara zake na muda wote alikuwa rafiki yangu. Mara nyingi kila kunapokuwa na Mkutano wa Bunge hapa Dodoma tumetafutana na kula ugali pamoja na muda wote tulikuwa tukishauriana. Mimi endapo nitajalia kurejea hapa kwa kweli nitamkosa sana. Lakini Tanzania hii ni ndogo tutakuwa tukiwasiliana kwa namna moja au nyingine. Mimi pia naomba nichukue fursa hii kumtakia kila la kheri na fanaka tele katika maisha yake. Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu na afya njema. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Mzindakaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusema hayo Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria ya Utawala alitoa ushauri ufuatao wakati akichangia Muswada huu mawazo.

Kwanza alisisitiza umakini katika kusimamia utekelezaji wa sheria hii, pili alisisitiza elimu kwa umma, tatu uwezeshaji wa wananchi, nne, ushirikishwaji wa wadau, tano kutambua nafasi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, tano uharaka wa kuidhinisha miradi, sita matumizi mazuri na tahadhari ya kuwezesha wananchi bila kuathiri mfumo unaopendekezwa wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea maoni na ushauri uliotolewa na Kamati na utatumwiwa katika kukamilisha maandalizi ya sheria na hatimaye kuandaa kanuni na miongozo ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, pia Msemaji wa Kambi ya Upinzani naye alitoa hoja mbalimbali ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo, kwanza Msemaji wa Upinzani Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa alielezea kwamba *PPP* ina hatari ya kuingilia Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Napenda kumhakikishia kuwa kwa kuzingatia miradi yote ya *PPF* hatma yake ni kurejea kuwa miradi ya umma ndio inamfanya Waziri mwenye dhamana ya fedha kuhakikisha kuwa miradi hiyo haina madhara kwa umma na vile vile wananchi wana uwezo wa kulipia ada au tozo inayotakiwa. Kwa hiyo, sheria hii kwa kweli haipingani na dhana yetu ya ugatuaji wa madaraka yaani *D by D*. (*Makofi*)

Pili, alisema kwamba kuwasilisha makubaliano kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kitengo cha fedha maelezo ni kwamba kila taasisi ina jukumu katika miradi ya *PPP*. Kwa kuanzia kila Wizara, Idara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa itabainisha miradi. Aidha, kitengo cha uratibu kitahamasisha, kitafanya uchambuzi na kitatoa ushauri kwa wadau jukumu kubwa la Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kutoa ushauri wa kisheria kwa mikataba na siyo kutoa ushauri kwa miradi.

Tatu, kuweka ukomo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu kutoa ushauri wa Kisheria kwa mikataba (*vetting*). Hapa napenda kueleza kuwa Muswada wa awali ulikuwa umeweka ukomo wa siku 14. Lakini baadaye wadau walitoa rai kwamba tukiweka jambo hili katika sheria lingeleta matatizo na Serikali ilikubaliana na ushauri

wa wadau. Hata hivyo nategemea kwamba Mwanasheria Mkoo wa Serikali atajengewa uwezo kwa kupatiwa vifaa na watalaam kwa ajili ya kusimamia na kutekeleza matakwa ya Sheria hii. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, lakini tukumbuke kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkoo kama zilivyo ofisi zingine za Serikali zina mkataba kwa mteja kwa hiyo, mkataba huu kwa upande wa Ofisi ya Mwanasheria Mkoo unataja kwamba barua zote na ushauri wowote unaohitajika kutoka Idara mbalimbali za Serikali utatolewa katika muda wa siku 14. Hivyo tunatarajia kwamba Mwanasheria Mkoo atatekeleza ahadi hii kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kazi ya kitengo cha uratibu ifanywe na *NDC* kulingana na maana ya maneno yaliyotolewa kwenye sehemu ya kwanza yaani Ibara ya *3 contracting authority means any Ministry, Government department or agency, local government authority or statutory corporation* ambapo *NDC* ni mojawapo ya taasisi hizi. *NDC* inahusishwa kama mtekelezaji wa miradi ya *PPP* na hivyo haiwezi kuwa mhamasishaji na mratibu na wakati huo huo mtekelezaji na ndio maana majukumu ya uhamasishaji na uratibu yanapendekezwa kuwa chini ya *TIC* ambayo majukumu yake ya msingi ndiyo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa pia ameleezea juu ya upembezi na uyakinifu ufanywe na Serikali na siyo sekta binafsi au wawekezaji. Maeleo ni kwamba Serikali ndio inayochukua athari za miradi kwa niaba ya umma. Aidha, baada ya kipindi cha mikataba ya miradi ya *PPP* kurejesha chini ya usimamizi wa sekta ya umma kwa hiyo, ni muhimu kwa Serikali kujihusisha kikamilifu katika kufanya upembezi yakinifu. Lakini hata hivyo sekta binafsi hufanya upembuzi yakinifu ili kujiridhisha kuwa miradi inarejesha rasilimali itakayowekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, injinia Christopher Chiza ambaye ametumwa na Serikali kutembelea maeneo mbalimbali yenyе miradi ya *PPP* ametupa mifano mizuri sana, mimi naomba Bunge hili liweze kutambua mifano hii. Ametoa mifano hapa Tanzania na nje ya nchi. Hapa Tanzania anatuambia kwamba Shirika la Damu ya Yesu la Manyoni limechimba visima vya maji na linaiuzia Mamlaka ya Maji Manyoni na Mamlaka ya Maji inasambaza maji hayo kwa wateja. Huu ni mfano mzuri sana wa *PPP*. Alikwenda huko Canada katika Mji wa Vancouver anasema ameona mradi mkubwa wa kutoa huduma ya usafiri wa reli na mabasi unaoitwa *trans link*, mradi huu unachangiwa na Serikali na wawekezaji katika sekta ya usafirishaji na usafiri. Lakini huko India amesema kwamba katika Jimbo la Maharashtra wawekezaji wanajenga barabara kadhaa halafu wanaruhusiwa kukusanya *road toll*. Hii ndio lengo pia ya sheria yetu hii. (*Makofii*)

Pia anasema kwamba kuna fursa ya *PPP* katika miradi mikubwa ya maji na umwagiliaji ambayo yako katika eneo lake na anasema mamlaka ya kuendeleza Bonde la Mto Rufiji (*RUBADA*) wanaangalia uwezekano wa kuendesha miradi ya umwagiliaji kwa ubia kati ya Bonde la Rufiji na wawekezaji. Mwisho anasema kwamba *PPP* itaharakisha maendeleo ya Taifa na kuipunguzia mzigo Serikali. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maeleo haya na ushauri huu tumeupokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo alizungumzia kuhusu usiri wa mikataba ya *PPP*, maelezo yetu ni kwamba kimsingi mikataba ya *PPP* ni mikataba ya umma na inabidi wadau mbalimbali washirikishwe ili kufanikisha utekelezaji wa miradi ya ubia. Kwa hiyo, mikataba hii haitakiwi kuwa ya siri hata kidogo. Kwa mfano miradi ya *PPP* inawataka wadau kulipa tozo la ada kwa watumiaji wa barabara, madaraja au shule hivyo wanawajibika kufahamu ikiwa wanatakiwa wafahamu haki zao na wajibu wao katika miradi hii.

Pili, sheria ya ununuzi wa umma isitumike katika miradi ya *PPP*. Muswada huu unatambua kuwa kuna miradi mingi inayoweza kutekelezwa kwa kutumia sheria ya ununuzi wa umma kwa kutoa ushindani na kuweka uwazi, utaratibu wa kumpatia mwekezaji na hivyo kuwa na *value for money*. Hata hivyo miradi inayohitaji utaalam wa teknolojia maalum Muswada unatoa fursa ya kushughulikiwa kwa utaratibu wa *unsolicited beat or proposals*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Anthony Diallo, Mheshimiwa Devota Likolola, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Eustace Katagira na wengine wametoa ushauri kwamba kuwe na uharaka wa kupitisha miradi tutumie uzoefu wa nchi nyingine, kanuni kuandaliwa na kutolewa mapema, Serikali ifanye utafiti ili kufahamu rasilimali zake, matumizi ya Balozi zetu kupata taarifa kuhusu uwekezaji kutoka nje, uwezeshaji wa wananchi, kutambua nafasi ya Serikali za Mitaa, elimu kwa umma na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge na utatumia katika kukamilisha maandalizi ya sheria na hatimaye kuandaa kanuni na miongozo ya utekelezaji. Ningependa kutoa taarifa kwamba katika maandalizi ya awali ya Muswada huu watalaam wetu wamechukua mifano ya nchi mbalimbali ikiwa ni pamoja na nchi kama vile Mauritius, Malaysia, Afrika Kusini na India. Lakini pia tumepokea ushauri kutoka Makao Makuu ya Jumuiya ya Madola yaani *CommonWealth Secretariat*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga amezungumzia uwianishaji wa sheria hii na sheria nyingine kama nilivyosema hapo awali kuwa sheria zitawianishwa na sheria hii. Ikumbukwe kwamba sheria hii siyo mbadala wa sheria zingine isipokuwa zinaongezea tu nguvu sheria zingine kwa pale ambapo marekebisho yamependekezwa na sheria hii.

Pia Mheshimiwa Siraju Kaboyonga amezungumzia kitengo cha fedha kuwa na uwezo huru yaani *autonomous*, hili limezingatiwa kwa hiyo, kitengo cha fedha kinatoa

taarifa kwa Waziri mwenye dhamana ya fedha. Ningependa kusema kwamba huu ni mwanzo, hebu tuwe na subira tuone sera hii itachangamkiwa namna gani kwanza na wawekezaji, lakini pia na Watanzania ndipo Serikali inaweza kuamua kupandisha hadi vitengo hivi viwe idara kamili na wengine wakati wa kupata maoni walipendekeza hata Wizara kwa sababu *PPP* inagusa maeneo mengi sana. (*Makofî*)

Pia Mheshimiwa Said Amour Arfi, amezungumzia sana kuhusu masuala ya ardhi hasa hofu yake ya kwamba ardhi ya wananchi itanyang'anya. Tungependa kumhakikishia Mheshimiwa Said Arfi kwamba miradi ya ubia haitatumika kuwanyang'anya wananchi kwa masuala ya ubia kwa masuala ya ubia yatahitaji kuzingatia sheria zetu zilizopo hasa sheria za ardhi. Tunamwelekeza Mheshimiwa Said Arfi kwenye kile kifungu cha 12. (*Makofî*)

Mheshimiwa John Cheyo, Mbunge wa Bariadi Mashariki amezungumzia sana suala la kujenga uwezo wa kufanya majadiliano, napenda kuliezea Bunge lako kuwa umuhimu wa kujenga uwezo na kufanya majadiliano ya ubia umezingatia kwenye Ibara ya 11 (2). (*Makofî*)

Hapa mwishoni Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa ametoa ushauri wa aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na kwamba Ofisi ya Waziri pengine imekuwa pana sana kusimamia maeneo haya ya *PPP* lakini pia hata *TIC*. Mamlaka ya kugawa kazi Serikalini ni mamlaka ya Mheshimiwa Rais atashauriwa. Hata hivyo ikumbukwe kwamba utendaji wa siku hadi siku wa shughuli za Serikali uko chini ya watumishi wa umma, chini ya Makatibu Wakuu. kesho Bunge litavunja sisi sote pamoja na Mawaziri tutakuwa majimboni, hivyo Serikali itaendeshwa na watumishi wa umma na wanafanya hivyo vizuri sana. Kazi ya Waziri ni kusimamia sera na utendaji isipokuwa pale ambapo kunakuwa na ulegelege katika utekelezaji Waziri hulazimika kuingilia kati na hatutarajii mara nyingi hali hii itokee.

Mheshimiwa Anastazia Wambura ameongea sana kuhusu vitengo na watumishi wa vitengo hivi, kwa ufupi vitengo hivi havihitaji kodi kwa sababu ni sehemu ya Idara za Serikali hivyo watumishi watapatikana kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma na sifa zitazingatiwa na ajira nayo itatokana na sifa na zitatangazwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Magdalena Sakaya wamezungumzia umakini katika kusimamia maktaba hii ni muhimu na imezingatiwa kwenye Ibara ya 17.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa kwamba sijawataja baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia pamoja na michango yao moja kwa moja lakini hata hivyo tumeorodhesha majina yao na michango yao yote tumeinukuu, tutatoa kabrasha baadaye ili kutoa maelezo au ufanuzi kuhusu hoja zao zote, hivyo wasiwe na wasiwasi, maoni yao yamezingatiwa yataheshimiwa na yatakuwa sehemu ya mwelekeo wetu wa utendaji katika kuimarisha sheria hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge ambaye ndio mtoa hoja wa hoja hii. Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu Kanuni zetu zinataka tupitishe sheria ya kupitia vifungu naomba Katibu atuingize katika hatua hiyo sasa.

(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)
KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Ubia Kati ya Serikali na Kampuni Binafsi wa Mwaka 2010
(The Public Private Partnership Bill, 2010)

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 2 kinaonekana kwamba huu Muswada ndio una-*apply* kwa *Mainland Tanzania*, lakini kama kutakuwa na mradi ambao unahusiana pamoja na yaani ni suala la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Muswada haujasemea chochote ikiwa wao *private partnership* watakaokuja kwa ajili ya mradi wanaotaka kuwekeza unahusiana na Jamuhuri nzima ya Tanzania. Muswada unasema nini kuhusu hiyo? Naomba Mheshimiwa Waziri atupe ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mheshimiwa Msemaji wa Upinzani katika eneo hili, Mheshimiwa Mnyaa, ikumbukwe kwamba eneo hili la uwekezaji sio suala la Muungano, lakini kama ilivyo desturi yetu ya uendeshaji Wa masuala ambayo sio ya Muungano, huwa Serikali zetu ziko karibu sana, tunakuwa na ushirikiano wa karibu na katika vikao vya masuala ya Muungano ambayo yanajadiliwa chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais. Mara nyingi huwa eneo hili ambalo sio la Muungano huwa yanajadiliwa sana. Kwa hiyo, tutatumia ule utaratibu mzuri kati ya Serikali zetu mbili.

MWENYEKITI: Kwa sababu nilikwisha hoji na mkakubali, aliturudisha kwenye Kifungu cha 2, sasa cha 3.

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 5

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho lakini kifungu cha 5 ukianzia kusoma section “a” yenye inasema; “make an assessment of all projects submitted to it and give recommendations to the Finance Unit for purposes of ascertaining whether the project;” sasa ukienda kwenye (iii) haiungani vizuri. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza ukianza na yale maneno “Whether the project” lile neno kwenye (iii) linaloanza na transfer, liwe transfers pale ukisoma linakuwa na maana iliyokusudiwa kwa sababu “s” imeachwa kwenye hilo neno transfer. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza neno lisomeke transfers appropriate technical, operational and financial risks to the private party.”

MWENYEKITI: Lipo tayari kwenye amendments za Mheshimiwa Waziri, hivyo hivyo unavyosema.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake*)

Kifungu cha 6

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 7

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 8

MHE. JOHN M. CHEYO: Mhehsimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nataka kuulizia tu juu ya namna hizi feasibility studies, zile responsibilities zitakavyokuwa coordinated, kwa sababu katika section hii inazungumzia juu ya public sector ita-cause feasibility study kuwa done. Tutakapoendelea utaona kwenye 8(2) private sector itafanya feasibility study, tutakapofika kwenye section 10, contracting authority itafanya feasibility study. Lakini naona kama vile kuna kitu ambacho kina-miss namna yaku-coordinate hizi three parties zote and more confusion public sector pia maana yake ni Wizara. Kwa hiyo, hapa Wizara imekuwa-mentioned kama vile naona imekuwa mentioned mara mbili. Kwa hiyo, ningependa kupata maelezo exactly hizi feasibility studies zitafanyika vipi, naona kama kuna something is missing. I don't know kama nimeelewaka.

MWENYEKITI: Unalo pendekozo? Kwa sababu....

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nimefikiria kwamba kama labda kabla ya hiyo section 8 (1) na (2) and then (10) kama ingekuwa a description kwamba the feasibility study can be sourced from any of the following, you know ambayo inaweza kuwa public sector, private sector na sioni again why we should

be talking about a contracting authority, which the contracting authority means public sector.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi juu ya *contracting authority*.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, analilosema Mheshimiwa John Cheyo ni sahihi, lakini ikumbukwe kwamba miradi hii inahusisha pande mbili, *public* na *private*. *Sasa feasibility study* ni makubaliano kati ya pande hizi mbili. Inaweza kufanywa na *contractor* ambaye anakubaliwa na pande zote mbili au kila upande ukawa na upembuzi yakinifu wake, hatimaye watakubaliana sana kwa madhumuni ya utekelezaji wa mradi ni *feasibility study* ipi ambayo itakuwa ikitumika. Kwa hiyo, sehemu hii katika utekelezaji hatuoni kama ni tatizo kubwa kwa sababu katika hali halisi ya utekelezaji, hatimaye lazima pande zote zikubaliane. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Yah, nadhani zaidi ni *style* ya uandishi, kwa maana hiyo..

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 9

MHE. SIRAJU J. KABOYONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 9 kwanza nianze na sehemu ya pili; *the contracting authority shall make consultation with the relevant regulatory authorities prior to submission of feasibility study and so on.* Hapa kifungu hiki kimetufunga kweli kweli. Hizi *appropriate regulatory authorities* hapa sheria inakusudia nini? Hilo ni fafanuzi la kwanza ninaloomba nipate. Lakini pili, ni kwamba kumekuwa na mawazo hapa ambayo ni sahihi kabisa kwamba wananchi wa Tanzania wapewe fursa ya kushiriki katika hii *PPP* na njia moja ambayo nilishauri katika mjadala ni kwamba kuwe na utaratibu wa kuziweka hizi *PPP's* kuwa *listed kwenye stock exchange*. Hapa nilidhani ambapo pengine hii *coordinating unit* ingefanya pamoja na hayo *ku-introduce aspect* ya kwamba *the PPP company should be also listed kwenye Dar es Salaam Stock Exchange*, ili kuwapa fursa Watanzania wengine *ku-participate* kwa kununua *shares*. Hicho ni ushauri tu kwamba labda ingekuwa ni moja ya mambo ambayo yanefanya chini ya kifungu hiki, nilikuwa naomba ufanuzi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga ame-raise masuala mawili. La kwanza ni lile la *contracting parties* na mahusiano yake na *regulatory authorities*. Kwenye *interpretation close*, itasoma kwamba *contracting parties* ni Idara za Serikali na Mashirika ya Umma. Ndio *public* yenyewe. Sasa kwa sababu Idara za Serikali zinafungwa na sheria mbalimbali zinazosimamia masuala mbalimbali hapa nchini ikiwa ni pamoja na sheria za *regulatory authorities*, hivyo inabidi Mamlaka hizi yaani *regulatory authorities* ziwe karibu sana katika utekelezaji wa miradi hii. Tuseme mradi

wa usafirishaji ambapo baadaye utatozwa, lazima matozo haya yakubaliwe na *SUMATRA* ndiyo maana yake hasa. (*Makofi*)

Eneo la pili ambalo amelisema linahusu uwezeshaji wa Watanzania. Nadhani Mheshimiwa Siraju Kaboyonga hapa ameharakisha kwenda mbele, haya ni makampuni au watu binafsi ambao wana fedha zao, wanataka kuwekeza kwa utaratibu wa *PPP* na wanafahamu kabisa kwamba sheria hii haina uhusiano kabisa na ule uwezeshaji kama tunavyofahamu sisi, kwa sababu sisi tuna sheria zingine za uwezeshaji hapa nchini, sheria zile zitatumika kadri ambavyo zinagusana na miradi ya *PPP* kama ajira, lakini hatuwezi kulazimisha kampuni zilizoorodheshwa kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange* kabla hazijaanza kuwa na miradi hapa nchini. Kwa kweli hilo sio lengo la makusudi ya sera. Makusudi ya sera ni kuwakaribisha wawekezaji ili kusaidiana na Serikali kuwa na miradi ya haina hii ili kuipunguzia Serikali mzigo wa shughuli zingine ambazo kwa kweli sio shughuli ambazo ni *core activities* za Serikali hapa duniani sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Na kwa vyovyothe vile kama unavyosema Mheshimiwa Waziri, sharti hilo lisingewekwa kwenye hatua ya *feasibility*, kwa sababu hatua hiyo sio tayari una hata kampuni, *feasibility* inasema tu kama kitu hicho kinawezekana kwa gharama na faida za aina fulani.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 10

Kifungu cha 11

Kifungu cha 12

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake*)

Kifungu cha 13

Kifungu cha 14

Kifungu cha 15

Kifungu cha 16

Kifungu cha 17

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 18

MHE.GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hili suala niliandika kwenye mchango wangu, nilitaka tu Mheshimiwa Waziri anifafanulie kwa sababu pale anazungumzia *signing of agreements*, sasa niliuliza tunaingia kwa uelewa wangu *agreement* ni makubaliano, lakini nikafikiri kwamba labda tunazungumzia mkataba ni *contract*, sasa nikataka Waziri atufafanulie ni vyema au busura kuendelea kutumia kwamba tu-sign makubaliano au tuna sign mkataba na kwa uelewa wangu

nafikiri makubaliano ni sehemu ya mkataba. Kwa mimi nafikiri pengine tulikuwa tuna *sign* mikataba zaidi kuliko makubaliano.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ni *some semantics* kwa sababu kile kilicho *agreements* pia *contract* na kwa hiyo, maneno haya yalivyotumika hapa ni sawa sawa tu. Huo ni utaratibu kwamba yale makubaliano ambayo wamekubaliana katika biashara yatakuwa *cleared* na *finance* na *unit* na Waziri anayehusika na mambo ya fedha na yatakuwa *vetted* na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla haujawa mkataba halisi. Lakini matumizi ya maneno *agreement au contract* kwa kweli ni *semantics*.

MWENYEKITI: Nadhani imekaa vizuri tu kwa sababu bado kuna hatua kabla ya kufikia ule mkataba halisi, kwa hiyo, yakubaliwe kwamba ni makubaliano.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 19

Kifungu cha 20

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu cha 21

MHE. JOHN M. CHEYO: Mhehsimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kuelezwu sababu ya kuwa na kifungu cha 21(2) kwa sababu kama mwekezaji au hiyo *project* ina *qualify under Tanzania Investment Act* ambayo *The Tanzania Investment Act* ina *include also incentives* ambazo zina uhusiano na misamaha ya kodi. Ni kwa nini hizi *projects* zisiweze pia zikapata msamaha wa kodi, kwa sababu hiyo *section 2* inaondoa hiyo. *Because it says; “The benefits referred to under subsection (1), shall not apply to tax incentives.”* Kuna *justification* kwa nini hizi ziweze zikapata *tax incentives*?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefikia uamuzi wa kuwa *section 21(2)* kwa kweli ni suala la kisera zaidi, tumefikiria kwa kisera zaidi kukwepa msamaha wa kodi katika miradi ambayo hatimaye itakuwa ya bishara. Hawa miradi ikikamilika watakuwa wakifanya biashara, watarejesha fedha walizotumia katika kuwekeza baada ya kufanya biashara. Kwa hiyo, inaonekana hakuna mantiki ya kuwasamehe kodi. Kwa maana nyingine kwa kweli hili ni suala la kisera na limejadiliwa kwa kina, uamuzi huu umefikiwa baada ya kuangalia *pros and cons*. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Na ukikitazama kifungu chenyewe, lazima useme vizuri, *subsection (1)* inasema ikiwa huo mradi sasa huo mpya, una sifa zinazowezesha ustahili chini ya *TIC* basi utapata. Kwa hiyo, *in my view labda inazuia duplication in fact*, kwa sababu hawazuii ku-*apply for TIC incentives*.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 22

Kifungu cha 23

Kifungu cha 24

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 25

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 26

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 27

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 27 kinahusiana na mambo ya adhabu kwa mtu anaetenda kosa katika sheria hii na adhabu iliyowekwa hapa ni ya faini ya shilingi milioni tano au kifungo cha miaka mitatu. Lakini sasa hayajafafanuliwa na katika maelezo yangu nilitaka ufanuzi, hili kosa la namna gani.

Kwa mfano, watu wameingia mradi upo, lakini *partner* mmoja akajitoa, sasa hii *magnitude* ya shilingi milioni tano na hasara atakayoitia labda Serikali kwa huyo *partner* mmoja kujitoa tutakuwa tumefanya nini? Kwa hiyo, hii adhabu hapa ni *general* tu, imeelezwa *general penalty*, lakini hii adhabu hatuioni kama inategemea lile kosa lenyewe? Naomba ufanuzi. (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano anaoutoa Mheshimiwa Mnyaa sio mfano mzuri sana kwa sababu kujitoa kwa *partner* mMoja hakuwezi kukatafsiriwa kama kosa la jinai. Kifungu hiki kinaongelea zaidi makosa ya jinai. Lakini kama ni kujitoa ambapo baadaye kuna sura ya jinai basi Mahakama ndiyo itaamua uzito wa kosa lenyewe.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Kifungu cha 28

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

Muswada wa Sheria ya Ubia Kati ya Serikali na Kampuni Binafsi wa Mwaka 2010
(The Public Private Partnership Bill, 2010)

(*Kusomwa Mara ya Tatu*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa mwaka 2010 yaani *The Public Private Partnership Act for the year 2010* kifungu kwa kifungu na kuukubali bila ya mabadiliko.

Naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Ubia wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa mwaka 2010 (*The Public Private Partnership Act for the year 2010*) sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge hoja iliyo mbele yetu ni ya kuupitisha Muswada wa Sheria ya Ubia wa Serikali na makampuni binafsi unaoitwa *The Public Private Partnership Bill* wa mwaka 2010, Hoja ya Mheshimiwa mtoea hoja imetolewa kwa kuupitisha Muswada huo na imeungwa mkono. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa mara ya Tatu na Kupitishwa*)

KATIBU MEZANI: Muswada wa Sheria kwa ajili ya kutunga Sheria itakayotekeleza Sera ya ubia kati ya Serikali na Kampuni Binafsi; kuanzisha mfumo wa Kisheria, utakaosimamia miradi ya Serikali na kampuni binafsi kupitia mikataba maalum, kuweka Sheria, miongozo na taratibu zinazohusu manunuzi ya watu na kampuni binafsi pamoja na mambo mengine yanayohusiana nayo (*A Bill for An Act to give effect to the*

public private partnership policy; to provide for Institutional frameworks for the implementation of public private agreements between public sector and private sector entities; to set rules, guidelines and procedures governing public private procurement, development and implementation of public private partnership and to provide for other related matters).

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada huo Umesomwa kwa Mara ya Tatu na kwa hiyo ni uthibitisho kwamba Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeupitisha Muswada huo rasmi. Sasa hatua iliyobaki itafuata kiutaratibu kukamilisha Muswada kumfikishia Mheshimiwa Rais. Nawashukuru sana kwa ushirikiano wenu. Namtakia Mheshimiwa Waziri na Serikali kazi njema ili Muswada huu uwe na manufaa makubwa kwa sisi sote Watanzania.

Waheshimiwa Wabuge, kabla sijasoma matangazo na tukizingatia kwamba huu ni Mkutano wetu, tuseme hiki ni kikao cha mwisho cha kawaida, kwa sababu kesho hatutakaa mkao huu tena. Itakuwa ni kumsubiri Mheshimiwa Rais aweze kuliaga Bunge. Hii *term* ya kuvunja Bunge ina maana tofauti kidogo, kuvunja Bunge ni pale ambapo atakaposaini *Government Notice* katika *Official Gazette*. Kwa hiyo, kesho sio kwamba Bunge linavunjwa, kesho Bunge linaagwa. Naona wengi wanasema kuvunjwa, basi lakini siyo hivyo, kisheria ni kwamba linavunjwa pale ambapo Mheshimiwa Rais atatamka katika *Official Gazette*. Niliona nitumie mamlaka yangu chini ya Kanuni ya 5 kumruhusu au kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu vinginevyo hatutasikia chochote kutoka kwake na pengine yeye kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali anaweza kuwa na mambo ya kusema. Kwa sababu ndiyo kawaida huwa tunamaliza maliza yeye akisema mambo fulani fulani kadri anavyoona. Sasa nilidhani sijui kwa kiasi gani atakuwa yupo tayari, lakini hata ile kumpa nafasi tu nadhani ni ustaaarabu, kwa sababu yeye kesho hataongea, ataongea Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwanza kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi, sikuwa najua kwamba ningeipata na niombe radhi kwamba asubuhi nilishindwa kushiriki kwenye kikao chako kutokana na shughuli nytingine. Lakini naomba nitumie nafasi hii kwanza kukushukuru wewe binafsi pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti ambao wamekuwa wakikusaidia katika kuliongoza Bunge hili Tukufu. Kwangu mimi imekuwa ni kipindi cha kujifunza, na ilikuwa shule kubwa. Lakini chini ya uongozi wako na wasaidizi wako kwa kweli imeniwezesha na mimi kutekeleza majukumu yangu kwa namna ambavyo mimi nimeridhika kabisa kwamba pengine isingekuwa chini ya uongozi wako mahiri, mambo mengi yangeweza na sisi kutupa taabu katika kuyasimamia. Kwa hiyo, kwa hili nakushukuru sana. (*Makofi*)

Lakini nataka vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wake. Sikumbuki vizuri sana lakini ninachokumbuka tu ni kwamba tarehe 8 Februari, 2008 saa za jioni, ukiniuliza ilikuwa saa ngapi, siwezi kukumbuka. Lakini, ulikuja hapa mbele ya Bunge hili ukawa umeshikilia bahasha moja uliyokabidhiwa na Mheshimiwa Rais. Wote tulikuwa tunasubiri kwa hamu kujuu nani atakuwa Waziri Mkuu. Ukasoma, ukanitaja mimi. Bunge hili likashangilia, kitu ambacho kilinipa faraja kubwa sana. (*Makofi*)

Lakini si hivyo tu, siku ile ulikuwa na Wabunge 282 hapa waliokuwa wameshiriki katika Mkutano huo, kura moja iliharibika, kura mbili zilisema hapana na kwa hiyo, nikafanikiwa kupata kura nyingi kwa zaidi ya asilimia 98. Kusema kweli jambo hili kwangu ni kubwa sana. Kubwa sana kwa sababu tafsiri yangu ilikuwa ni kwamba Bunge zima ikiwa ni pamoja na wenzangu wa upande wa Upinzani kwa sehemu kubwa kabisa waliniunga mkono kutokana na uteuzi alioufanya Mheshimiwa Rais mbele ya Bunge lako hili Tukufu. (*Makofi*)

Namaliza kipindi changu cha miaka miwili na miezi kama mitano kwa furaha kubwa sana, kubwa sana kwa sababu ninyi ndiyo mmenifanya nikajisikia muda wote kama mwenzenu na pale palipokuwa na jambo mmenishirikisha kikamilifu na muda wote mmekuwa ni washauri wangu wazuri katika hali mbalimbali. Haikuwa kazi nyepesi kwangu hata kidogo hasa mkizingatia kwamba niliingia madarakani katikati ya kipindi cha miaka mitano na katika mazingira kwa kweli ambayo kidogo yalikuwa magumu, sikuwa na uhakika kama ningeweza. Kwanza nikakubalika, pili nikawa na mimi ni sehemu ya watu ambao wanaweza kuwa na uwezo wa kufanya kazi pamoja na kundi la Waheshimiwa Wabunge katika kipindi hicho. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini kubwa nawashukuruni sana ninyi ambao mmeweza kunikubali na kwa kweli kunisaidia kwa kiasi kikubwa sana. Ahsanteni sana na Mwenyezi Mungu kwa kweli awabariki sana, sana tu wote kwa ujumla wenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wenzangu Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri. Tumefanya nao kazi kwa kipindi chote hiki cha miaka miwili karibu na miezi mitano kwa pamoja kwa ushirikiano mkubwa na kwa mshikamano mkubwa sana. Katika kipindi hiki kumbe nimeona kwamba kuongoza ni kazi kubwa. Inabidi ujitalahidi sana, uwe msikivu kwa yale yote utakayokuwa unashauriwa na wewe uwe mwepesi vile vile kutoa maoni yako na kwa kiasi utakachowenza kuwaambia kwa lugha ya staha pale unapokuwa unatofautiana nao; wamenisaidia sana, wamelisaidia Bunge kwa kiasi kikubwa kwa kazi zile ambazo tulitakiwa kwa pamoja kuzifanya hapa Bungeni. Nataka mbele ya Bunge lako Tukufu nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri sana waliyoifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo kundi moja ambalo nisiposema jambo juu yao sitakuwa nimewatendea haki. Ni Wenyeviti wa Kamati zako za Kudumu. Sababu mimi nimekuwa na ushirikiano wa moja kwa moja nao hasa nilipokabiliwa na mambo mazito ambayo yalitaka pengine nizungumze nao moja kwa moja. Viongozi hao kwa ujumla wao kwa maana ya Kamati zote, wamekuwa ni rafiki zangu wa karibu sana, sana tu. Tena bila kujali kwamba huyu anasimamia Kamati ipi na anatoka Upinzani. Mzee Cheyo, Mzee Slaa na wengine wote walikuwa ni watu waliotoa ushirikiano mkubwa na wa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, niliona nilitaje hili kwa sababu ni vyema kwa kweli kuweka katika kumbukumbu jambo ambalo unaona limekugusa na limekuweza kufanya kazi kuwa nyepesi kwa kiasi kikubwa sana. Mimi nawashukuru sana wote kwa ujumla wenu Wenyeviti. Nataka niwahakikishie kwamba mimi kwa upande wangu namaliza kipindi

hiki cha miaka miwili na miezi mitano nikiwa na moyo mkunjufu sana kwenu kwa kuwa kwa sehemu mlitusaidia sana upande wa Serikali katika kushauriana. (*Makofi*)

Hawa ndugu zangu wa Upinzani hawa, wanastahili neno vile vile la kusema. Pamoja na maswali yao yote ya kunitegea maana kazi yao wakati mwingine ilikuwa ndiyo hiyo, hasa rafiki yangu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Lakini nimefarijika sana kwamba tulikurupushana mbele ya kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo au kwenye hoja mbalimbali. Lakini tulipotoka nje bado tuliendelea kuwa marafiki wa karibu sana na tumefanya kazi kwa pamoja bila tatizo hata kidogo na wakati mwingine nilikuwa nashindwa kujua sasa kama Bunge lina wapinzani au hapana mpaka unaporudi ndani hapa ndiyo unakumbuka kwamba eeh, kumbe wapo. (*Makofi*)

Lakini vinginevyo tumeshirikiana vizuri na mimi nataka niwashukuruni sana kwa ushirikiano huo. Mungu awabariki, muendelee kuisaidia nchi, lakini ni imani yangu kwamba katika mambo yote yanayogusa maslahi ya nchi tutashikamana na tutakuwa pamoja. Maana hilo ndiyo jambo la msingi sana na nataka nitumie mfano halisi, juzi wakati tunapitisha Bajeti hapa nilimuuliza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed safari hii kweli mnataka kutoka nje tena? (*Makofi/Kicheko*)

Lakini nilimuuliza makusudi tu, kwamba jambo kubwa kama la Bajeti ya Taifa mkitoka mmekasirika, mnasema mnatoka, kwangu mimi inanipa taabu. Kwa sababu mwisho wa yote mtatumia Bajeti hiyo hiyo kuendesha shughuli zenu. Kwa hiyo, katika mambo makubwa haya ni vizuri mkatusema, mkacharuka kweli kweli, lakini kwa hili ambalo ni la Taifa ni vizuri watu tukasema pamoja na mengine yote tuliyoyabaini lakini tutafanya kazi pamoja kwa sababu tuko hapa kwa ajili ya maslahi ya Watanzania, maana kuna wakati nilimtania, sasa rafiki yangu unataka nifanye nini, niache kuleta fedha kwenye jimbo lako maana umenikatalia?

Lakini siwezi kufanya hivyo kwa sababu wote ni Watanzania wale. Kwa hiyo, katika jambo kama hili ni vizuri tukashirikiana wote kwa pamoja. Kwa hiyo, kwa ujumla nasema ahsante sana na nimshukuru Katibu wako, Bwana Thomas Kashililah na wasaidizi wake wote ambao wamejitalidi katika kipindi hiki kufanya kazi kwa namna ya pekee sana kuisaidia Serikali yetu lakini vile vile Bunge zima kwa ujumla. Wote hawa nasema ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningeweza nikaamua kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali pembeni. Lakini nimeona nalo niliseme hapa hapa. Mwanasheria Mkuu ametusaidia sana. Mimi namsifu sana, namsifu kwa sababu akisimama, bahati yake mbaya sana hajui kutumia lugha ya kumpendezesa mtu, lakini ujumbe umekuwa ukitufikia tena ujumbe chanya muda wote. Kwangu imenipa nguvu sana na ndiyo maana wakati mwingine nikikaa hapa hata kama kuna jambo kubwa najua Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo atalishikilia vizuri, na tutalimaliza vizuri. Kwa kweli AG nakushukuru sana kwa sababu pamoja na kwamba ni sehemu ya Baraza la Mawaziri, lakini una nafasi yako kama Mshauri Mkuu wa shughuli zote za Serikali na Sheria za nchi. Kwa hiyo, nilitaka niseme ahsante sana kwa nafasi hiyo uliyokuwa umeitumia vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kulisema hili basi niwatakie kila la kheri, nawatachia Wabunge wote pamoja na wewe Mheshimiwa Spika kila la kheri, tutakapomaliza jukumu hili kesho niwatakie safari njema. Kwa kweli niwaombee kwa Mwenyezi Mungu ikiwezekana wote kabisa mshinde na mrudi tena Bungeni na kwa wale ambaao kwa bahati mbaya pengine tutawakosa, *Inshallah*, siyo mwisho wa kila kitu. Maana juzi wakati Mheshimiwa Rais anaanza kutengeneza mkakati wake wa mambo haya wa kugombea katika vikao vyake viwili, nilifurahi sana. Anawaambia Mheshimiwa Mheshimiwa Dr. Mohammed Gharib Bilal na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha pale kwamba aah, hapa imeshindikana lakini siyo mwisho wa mambo, bado nafasi zipo nyingi tu nchini hapa na imetokea hivyo hivyo kwamba angalau Dr. Mohammed Gharib Bilal sasa ni mgombea kwenye nafasi nyingine nzuri. Kwa hiyo na hata Wabunge hawa kwa umahiri niliouona bado mnaweza mkasaidia Taifa hili kwa njia nyingine nzuri zaidi katika maeneo mbalimbali kwa kadri itakavyowezekana. (*Makofi*)

Maadam umenipa nafasi hii Mheshimiwa Spika, basi nimalizie na jambo moja kubwa, kubwa kwa maana tu kwamba Serikali hii bila kuwa na watalaam ambaao huwa wanakaa wamefichama fichama kule kwenye vidirisha, sisi hapa ndani mnaotuona Mawaziri ni kazi bure, hatuwezi kufanya kitu.

Kwa hiyo, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi mbalimbali, viongozi wa taasisi, vyombo vyaa dola na wengine wote kwetu sisi Serikalini lakini naamini hata kwa Bunge lako hili Tukufu wamekuwa na mchango mkubwa ingawa hapa Bungeni leo hawapo lakini kwa sababu umenipa nafasi hii ni vyema nikasema nawashukuru sana kwa namna walivyotusaidia sisi Serikalini. Lakini vile vile Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vyombo vyaa habari kwa upande mwingine lazima tuendelee kuwashukuru nao. Kuna sehemu wameweza kuteleza kidogo, lakini mimi nasema kwa ujumla wake, vyombo hivi vimesaidia sana kutoa na kupeleka habari kwa Watanzania ili waweze kujua kinachoendelea Bungeni ni kitu gani. Wamefanya kazi kubwa na nadhani wanastahili pongezi. Kwa hiyo, niliona nao ni vizuri niseme ahsante kwa kazi ambayo wameifanya. (*Makofi*)

Niendeleee kumshukuru Rais kwa kunipa heshima hii kubwa, niendeleee kuwashukuru wasaidizi wake wakuu kwa maana ya Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar na Waziri Kiongozi kwa upande wa Visiwani ambaao kwa namna moja au nyingine tumefanya kazi nao kwa karibu sana. Hali kadhalika, Mawaziri wote wa upande wa Zanzibar, kwani tumekutana nao kwenye vikao vingi sana ambavyo vimetukutanisha kati yangu mimi na wao au kati ya Mawaziri wangu na wao. Na yote haya tuliyafanya katika kujaribu kuleta mshikamano, kujenga umoja mionganii mwetu na kuwezesha pande hizi mbili tujione kama wamoja ambaao jukumu letu ni kuwasaidia Watanzania waweze kupata maendeleo. Naomba nitumie nafasi hii kusema ahsante sana kwa hayo yote ambayo yamejitokeza ndani ya kipindi hiki cha miaka miwili na miezi mitano, lakini kwa vile nimechukua jukumu hili kutoka kwa mwenzangu kwa kweli ninazungumza kwa niaba ya miaka yote mitano. Ahsante sana na ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili nimeona nilichomekee hapa tu kwa sababu sina mahali pengine pa kulisema. Kwa sababu ni siku ya mwisho, nilifikiri ningepata nafasi nikalisema. Wakati tulipotoa maelezo kuhusiana na maeneo mapya ambayo Mheshimiwa Rais ametoa baraka kwamba yaingie katika mchakato rasmi wa kuanzishwa, yapo maeneo ambayo hatukuyasema.

Sasa nimeona leo kwa sababu nimepata fursa hii, niyaseme na siku ile niligusia kwamba alikuwa ameacha eneo moja la Mkoa mpya wa Katavi, kwa kuwa alitaka kwanza tumalize hali ambayo ilitaka kidogo suluhu kati yake. Hatimaye, juzi ameridhia kwamba Mkoa wa Katavi na wenyewe utakuwa ni mionganoni mwa ile mikoa minne na utaanzzishwa pamoja na mikoa hiyo mingine. Mkoa wa Katavi sasa unaugawa Mkoa wa Rukwa katika maeneo makubwa mawili; kwa hiyo sasa tutakuwa na Mkoa wa Katavi, ambapo tutakuwa na Wilaya ya Mpanda, Wilaya mpya ya Mulele na tutakuwa na Wilaya mpya ya Kaliua, nitalieleza hivi punde. Kwa hiyo, huo Mkoa nao ni sehemu ya ile mikoa minne. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye Wilaya, amekubali kwamba Wilaya ya Urambo, igawanywe katika wilaya tatu badala ya mbili. Kwa hiyo, lile lililokuwa Jimbo sasa la Kaliua, ambayo tulikuwa tumeamua iwe ni Wilaya moja yenye ukubwa wa zaidi ya kilometra za mraba 15,000 na zaidi, na lenyewe sasa ligawanywe mara mbili; kwa hiyo, sasa tutakuwa na Wilaya ya Kaliua na Wilaya ya Ulyankulu. Sasa Ulyankulu itabaki Mkoa wa Tabora, Wilaya hiyo ya Kaliua nimewaomba wenzangu wa Tabora, basi watumegee kule Rukwa ili iingie kwenye Mkoa wa Katavi na bahati nzuri wameridhia, wamekubali. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa upande huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na uamuzi huo wa Rais, sasa imebidi vilevile akubali Tarafa mpya zifuatazo zijitokeze; Tarafa ya Uyumbu, Tarafa ya Usoke, Tarafa ya Songambele na Tarafa ya Ukondamoyo kwa upande wa Wilaya ya Urambo. Vilevile amekubali kwa upande wa Wilaya ya Kaliua, iwepo Tarafa ya Kazaroho, Tarafa ya Ukumbinsiganga na Tarafa ya Igagala. Kwa upande wa Wilaya mpya ya Ulyankulu, kutakuwa na Tarafa ya Kashishi na Tarafa ya Muongozo; sasa hiyo itakuwa imekamilisha kiporo ambacho kilikuwa kimebaki.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kaliua itakuwa na Halmashauri yake, Wilaya ya Ulyankulu nayo itakuwa na Halmashauri yake na Urambo itabaki na Halmashauri yake. Tofauti mtakayoiona hapa ni kwamba kwa kufanya hivyo maana yake ni kwamba sasa Wilaya mpya ya Ulyankulu ni lazima tuiombe Tume ya Uchaguzi ikubali vilevile liwe ni Jimbo la Uchaguzi. Kwa sababu hakuna namna nyingine na hauwezi ukawa na Mbunge mguu mmoja uko Tabora na mguu mwengine upande wa Mkoa wa Katavi; kwa hiyo, pale itabidi tuwaombe watukubalie iweze kukaa hivyo. Lakini vilevile sasa amekubali kwamba Manispaa ya Arusha, itakuwa ni Halmashauri ya Jiji la Arusha. Sasa nadhani itasaidia katika mtazamo mpya wa Makao Makuu ya Afrika Mashariki na nadhani hii itaongeza chachu kubwa zaidi katika eneo lile. Yapo mabadiliko kidogo tutayafanya kwenye Kata ili kuongeza eneo katika Jiji hilo la Arusha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapa kitakachofuata ni taratibu zetu za ndani kwa maana ya kuunda vikundi kazi sasa kuhakiki mipaka ya maeneo hayo yote. Itafuatiwa na zoezi la kuandaa maelezo ya mipaka hiyo vizuri (*boundary descriptions*) na baada ya hapo tutaandaa rasimu ya *Government Notice* ambayo itatoa utaratibu mzima na mipaka yake kikamilifu na tukishaisaini ile, itarudi kwenye maeneo husika. Kama bado kuna mtu ana mashaka, atakuwa huru kuweza kueleza chochote.

(*Hapa Waziri Mkuu alinong'onezwa jambo*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, ooh! Ananikumbusha kweli, vilevile Mheshimiwa Rais amekubali Wilaya ya Karagwe igawanywe mara mbili; kwa hiyo, pale kutakuwa na wilaya mbili. Samahani sana, nimepitiwa tu. Kwa hiyo, hiyo nayo imeingia pale. Kwa hiyo, hizi zote sasa zitaingia katika utaratibu wa sheria, tutawauliza wananchi kama wameridhika, watatuambia makao makuu yakae wapi? Na mimi ninataka niwaombe Watanzania, msichukue muda mwingi sana kuvutana juu ya makao makuu; wakati mwingine tutajichelewesha bure tu, kubwa ni kwamba mmepata mkoa, kubwa ni kwamba mmepata wilaya, makao makuu si hoja kubwa ya kutupotezea wakati. Kwa hiyo, nadhani hilo tukilifanya litaharakisha, matarajio yetu ni kwamba wakati tunamaliza shughuli hizi za uchaguzi, mambo yote haya yatakuwa yamekamilika. Kwa hiyo, tunaamini hakutakuwa na migogoro katika kuweka mipaka na hatimaye kujua Diwani anakwenda kata gani na ni Mbunge gani anakwenda jimbo gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema niliona nichomekee hapa hili jambo kwa sababu sina mahali pengine pakuveza kufanya hivyo. Niwie radhi kama pengine nimekuondolea ratiba yako ulivyokuwa umeipanga. Vinginevyo Mungu awabariki sana, Mungu ibariki Tanzania, awabariki Watanzania wote, ahsanteni sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa taarifa zote hizo na pia kututakia mema. Sisi Wabunge, tumefaidika sana na namna Mwenyezi Mungu alivyokupa utilivu, jinsi alivyokupa ujaribu wa kulielewa jambo kabla ya kuamua na hatimaye unapoamua linakuwa ni la dhati. (*Makofi*)

Mimi binafsi niseme nimefaidika sana na ushirikiano wako na aah, niseme tu katika nafasi moja ambayo mimi ninavyoamini, haya ni mawazo yangu na sio ya Wabunge wote ni mawazo yangu mimi, ikiwa mambo yatakwenda kama tunavyodhania Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Kikwete akachaguliwa tena na wewe ukapita jimboni, sioni kwamba Rais huyu ana mtihani mkubwa sana mwezi Novemba, 2010 kumpata Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mimi mnanijua, mimi ni muwazi tu. Sasa mtu amefanya kazi nzuri namna hii, halafu uwe na mtihani, atafakari, aulize, mimi nadhani nafasi moja ambayo Rais Kikwete hana taabu nayo hata kidogo, wiki ya kwanza ya Novemba mwaka huu, ni Waziri Mkuu, kwa sababu tayari tunaye. Namuomba radhi Mheshimiwa Rais kama nitamkwaza kwa matamshi kama haya, lakin nadhani mpaka sasa ameshanizoea. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge,

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, samahani kidogo...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, samahani sana, naona narudi mara mbili mbili. Nimemuona bwana mkubwa amenifuata, amegundua kuwa nimeisahau kuitaja wilaya yake.

Mheshimiwa Spika, katika orodha hii licha ya Karagwe kugawanywa mara mbili kwa maana ya kuwa na Wilaya ya Kyerwa, vilevile amekubali Wilaya ya Magu, lile Jimbo la Busega, liwe ni Wilaya na lihamie kwenye Mkoa mpya wa Simiyu; nilisahau sana kutamka hilo. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dr. Chegeni, unavunja Kanuni; Spika akisimama, wewe ni lazima ukae. Ninakusamehe kwa sababu una furaha sana. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, hiki ndicho kikao chetu cha mwisho cha kawaida. Kwa hiyo, ninamuomba sasa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa sababu ya utaratibu nitakaouulezea kesho, basi atoe hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 136(1), ili tuweze kutengua Kanuni. Kwa sababu kesho itabidi waingie watu ambaio sio Wabunge. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema kesho ni siku muhimu sana katika historia ya Bunge hili. Kutakuwa na wageni wengi ambaio wengine hawatakuwa kwenye *gallery*, itabidi waingie ndani ya Bunge. Hivyo hoja ninayotaka kuwasilisha ni hoja ya kuwaruhusu viongozi ambaio si Wabunge, kukaa katika Ukumbi wa Bunge, wakati Rais atakapokuwa akilihutubia Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 136(1) na ile Kanuni ya 150 ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2007, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, litoe idhini ya viongozi wafuatao kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge, ili waweze kujumuika na Waheshimiwa Wabunge, katika kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, viongozi hao ni kama ifuatavyo; kwanza ni Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pili ni Waheshimiwa Majaji wawili, Jaji Mary Shangali na Jaji Mwanaisha Kwatiko wa Mahakama Kuu Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, nafiki. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Bunge liliafiki utekelezaji wa hoja iliyotolewa)

SPIKA: Kesho Bunge litaanza saa 9.00 alasiri. Dua itasomwa na nitatoa taarifa ya ujio wa Rais, baada ya hapo nitasitisha shughuli za Bunge kwa muda. Saa 9.50 alasiri maandamano ya Majaji na Katibu Mezani yataingia ndani ya Ukumbi. Saa 9.55 alasiri maandamano ya Mheshimiwa Spika na Rais yataingia Bungeni. Maandamano hayo yataongozwa na *Serjeant-At-Arms* na kufuatiwa na Spika, Rais na nyuma Katibu wa Bunge. (*Makofi*)

Baada ya hapo nitamkaribisha Rais, kwa niaba yenu na ataanza kuhutubia saa 10.00 alasiri; ndio maana ya kuingia saa 9.55 alasiri. Kwa hiyo, ataendelea kwa kadri alivyojiandaan na kwamba mwisho nitamshukuru kwa maneno mafupi sana, nimeandikiwa hapa. Kwa sababu nisipoandikiwa, ninaweza kusema mengine. Kwa hiyo, hapo itakuwa ndio mwisho; kitakachobaki sasa itakuwa ni ghafla ya jioni ambayo itaanza saa 1.30 usiku kesho. Mgeni Rasmi ni Rais. Hafla yetu itakuwa pale pale mahala pa burudani pale, uwanja wetu wa maonesho saa 1.30 usiku mavazi ni *smart casual*, sio lazima kuwa rasmi sana. Ila ningomba mahudhurio yawe mazuri kwa sababu Mheshimiwa Rais, atatutunuku vyeti; hili ni jambo la mara ya kwanza kutokea, utumishi ule wa miaka mitano ndani ya Bunge. Tumeandaa vyeti ambavyo kila Mheshimiwa Mbunge, atakuwanacho cheti kilichotiwa sahihi na Spika na Katibu wa Bunge, ila cheti cha Spika, kimetiwa sahihi na Waziri Mkuu na Katibu wa Bunge. Eeh ndio, sasa huwezi kuweka cheti ambacho sahihi ni yako mwenyewe, ukasema na wewe, eeh! (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, kwa uwakilishi maalum na watu wataitwa kwa majina kwa kweli inakuwa ni ukosefu wa nidhamu pale linapoitwa jina, haupo na sababu haijulikani; kwa hiyo, tujitahidi tuwepo pale. Kila kitu kitakuwepo, chakula kizuri, muziki, mambo yote yanayokwenda na shughuli kama hii. Kamati yetu ile ya tafrija, inaendelea kuwasiliana na taasisi mbalimbali za sanaa ili kuwe na mchanganyiko unaozingatia Utanzania wetu. Taarab, akina Marlaw, Ali Kiba na nani hao na muziki wa dansi na kadhalika. Kwa hiyo, baada ya hapo, nimeruka mambo machache tu ni kwamba kesho tutapiga picha na Rais; baada ya ile hotuba yake, tutapiga picha na Rais mbele ya jengo kwa makundi. Wabunge Wanawake, Wabunge Walemavu, kama tulivyo yaani ule uwakilishi tulivyo Kitanzania nao utazingatiwa na nadhani baada ya hapo, hafla rasmi mwisho itakuwa ni saa 5.00 usiku lakini haizuwii wale ambao bado ni vijana kuendelea hadi pale watakapochoka wao. Tunakusudia kwamba Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Spika, waweze kuondoka saa 5.00 usiku ili yale mengine yanayofuatia yafanywe kwa uhuru mpana zaidi. (*Makofi/Kicheko*)

Leo tulipoongea katika Kamati ya Uongozi, kulitokea wazo kwamba watu wakae kwa itifaki na nini kwamba labda *Steering Committee* wakae sehemu yao na Tume ya Huduma za Bunge. Mimi nikali-veto, nikalikatalia kabisa hilo, kwa sababu nakueleweni vizuri. Baadhi yenu baada ya kazi ngumu huwa mnataka kustarehe na starehe nyingine

inafaa iwe ni ya faragha, ndio! Maana mtu anaweza kuwa amekuja lakini *partner* wake akawa sio rasmi sana. Sasa ukiwapanga watu kwa itifaki, unaleta taabu. Kwa hiyo, hatutakaa kwa itifaki yoyote, lakini tunapoitwa sasa, *Steering Committee* basi tunasimama tunakuja kushikana mkono na Mheshimiwa Rais. (*Makofi/Kicheko*)

Nadhani hayo yanatosheleza, kikubwa ni kwamba kesho saa 9.00 alasiri Bungeni. Matangazo mengine tu ni Waheshimiwa Wabunge, tunawaomba Waheshimiwa Mawaziri kwa zile ahadi zote walizotoa za kutoa majibu kwa maandishi, tafadhalini sana ikiwezekana ndani ya siku hizi mbili, tatu yapatikane. Kwa sababu hayo majibu mengine ni msaada mkubwa sana kule Jimboni. Kule Majimboni mtu akiulizwa, sasa kama hata jibu hajalipata kutoka Serikalini, inakuwa ni shida. Kwa hiyo, tunaomba sana majibu ya maandishi na majibu mengine ya barua ambazo Waheshimiwa Wabunge waliuliza kuhusu miradi mbalimbali, tuwe na ushirikiano mzuri tu, tupate majibu ili yatusaidie katika shughuli za Jimboni. (*Makofi*)

Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo mukutane kesho saa 4.30 asubuhi, nadhani ukumbi utakuwa ni ule wa 231. Kwa hiyo, *PAC* saa 4.30 asubuhi Ukumbi wa 231. (*Makofi*)

Naomba kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, hili ni tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwamba leo saa 6.00 usiku ndio mwisho wa kusajili simu. Sasa kama ulizubaa tu, utaamka asubuhi simu yako haina maana yoyote ni kama karatasi tu. Kwa hiyo, sijui sasa kama kuna nafasi ya kueleza hapa kama kuna fursa kati ya sasa na saa 6.00 usiku kusajili? Nadhani ipo *electronically*? Anaoneshha kidole, ipo au ni vizuri nimpe nafasi atueleze vizuri maana ni hatari sana Mbunge ukiamka kesho, simu haifanyi kazi, haitoi *calls* haina sauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani kwa kunipa nafasi ya kutoa maelezo ya ziada. Napenda kukumbusha tu kwamba uandikishaji wa simu na *sim cards* ulianza tarehe 1 Julai, 2009 kwa lengo la kuusitisha tarehe 31 Desemba, 2009.

Lakini baada ya kuona kwamba maendeleo ya uandikishaji ulikuwa bado haujakamilika, ikaongezwa miezi sita mingine mpaka tarehe 30 Juni, 2010 na hata ilipofika hiyo tarehe bado tena walionekana watu wengi hawajajiandikisha na kwa kibali maalum tukaongeza majuma mawili ambayo yanaisha leo saa 6.00 usiku na baada ya hapo zile ambazo hazijasajiliwa zitazimwa. Lakini kati ya sasa na saa hizo, kule kwenye sehemu yetu ya ukumbi ule ambako tunafanya sherehe kesho, wapo watu, *operators*, bado wanaandikisha, lakini vilevile unaweza kujandikisha *electronically*.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo simu itazimwa na zitakaa katika *black list* kwa muda wa miezi mitatu na baada ya hapo simu hiyo inafutwa kabisa na haitatumika tena. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa tangazo hilo, nadhani sote tutazingatia. Waheshimiwa Wabunge, mimi sina hotuba ya kuwaaga kwa sababu kwa imani yetu sisi Wanyamwezi, kuagaaga sana ni nuksi. Kwa kuwa, nina makusudio ya kurudi hapa, mimi siwezi kuwaaga. Kwa hiyo, ninaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 9.00 alasiri. (*Makofi/Kicheko*)

(Saa 7.00 mchana Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 16 Julai, 2010 saa 9.00 alasiri)